ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

WIMBO WA TAIFA WA ZANZIBAR

Kikao cha Kwanza - Tarehe 22 Januari, 2014

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za (SMZ) (Kny/Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais, naomba Kuwasilisha Mezani nakala zote za gazeti rasmi la serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 21, Disemba 2013.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Waziri wa Kilimo na Maliasili naomba kuweka mezani uwasilishaji wa Mswada wa Sheria kuanzisha sheria ya Hati Miliki za wagunduzi wa aina ya mbegu mpya za mimea na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny/Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba kuweka Hati Mezani ya hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, kuhusu Mswada wa kuanzisha sheria za hati miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 15

Nafasi ya Zanzibar Katika Changamoto Zinazoibuka EAC

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 3

Vianzio vya Mapato ya Baraza la Manispaa na Mabaraza ya Miji

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:-

Kwanza Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kuungana nami katika Msiba wa mama yangu bibi Waride Thereya Khamis, kilichotokea tarehe 18. Nawashukuru wajumbe wote ukiwemo na wewe Mhe. Spika.

Vile vile, nakishukuru Chama changu cha CUF kwa kushiriki katika mazishi haya kuanzia Wilaya mpaka Taifa. Vile vile, nikishukuru Chama cha Mapinduzi, kuleta ujumbe wake kushirikiana nami katika mazishi hayo. Mhe. Spika, sasa naomba swali langu Nam.3, lijibiwe.

Kwa kuwa Mabaraza ya Miji hufanya kazi zake kwa kutegemea sana vyanzo vya mapato kutoka kwa wananchi wa maeneo yao na kwa kuwa kutegemea mapato kutoka kwa wananchi pekee ni kujilemaza na kupunguza ongezeko la mapato ya vyanzo vyengine.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuyaendeleza mabaraza yetu ya miji kwa kuwapa mbinu za kujitafutia mapato tofauti na mbinu wanazozitumia hivi sasa.

(b) Je, kwa kiasi gani vyanzo vya mapato vya Mabaraza haya vinapata idhini na baraka ya Madiwani.

(c) Je, utaratibu gani unaotumika katika kuhakikisha kwamba, vyanzo hivyo vya mapato vinakusanywa ipasavyo bila ya kuwepo udanganyifu kwa wakusanyaji wa mapato hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ -Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 3 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo :

Mhe. Spika, msingi mkubwa wa kujitegemea ni kuweza kuzalisha mahitaji yetu makubwa na fedha za kuendeshea shughuli zetu sisi wenyewe. Ingawaje hii haizuii kutumia mbinu nyengine kama uwekezaji na misaada ya wahisani. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM na mipango yetu ya maendeleo imeweka mkazo suala la kuwahamasisha wananchi kushiriki katika kusukuma kazi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika maeneo yao.

Pia, katika wahisani wengi hupenda kusaidia pale ambapo wananchi wenyewe wameonyesha nia ya kushiriki katika kuanzisha miradi ya maendeleo. Hivyo, kupitia Serikali za Mitaa ambapo Mabaraza ya Miji ni sehemu ya Serikali za Mitaa wananchi wana wajibu wa kuchangia mapato yatakayosaidia maendeleo ya Mji husika.

Mhe. Spika, tusipochangia wenyewe katika maendeleo yetu tutajikuta tunaathirika sisi wenyewe kwa kukosa huduma muhimu na miji yetu itazidi kuwa michafu. Kote duniani miji inachangiwa kwa kiasi kikubwa na wakaazi wa Miji hiyo na wananchi hawasubiri mtu aje kutoka nje kuwapatia fedha za kuendesha shughuli zao.

Baada ya maelezo hayo sasa, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

a. Mhe. Spika, serikali kwa sasa inaendelea na mageuzi katika mfumo wa uendeshaji wa Serikali za Mitaa, ambapo Sera ya Serikali za Mitaa imeshapitishwa na Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa utawasilishwa katika Baraza lako Tukufu muda si mrefu katika kipindi kijacho.

Aidha, mfumo wa ukusanyaji mapato unaimarishwa kwa kutumia mbinu za kisasa za ukusanyaji wa mapato, kuajiri wataalamu hasa maafisa mapato na wahasibu wenye taaluma, Halmashauri na Mabaraza ya Miji. Pia, ruzuku za Mabaraza ya Miji zimeangaliwa upya na miradi ya wahisani hasa *ZUSP*, inachangia kuimarisha huduma na kupitia mifumo ya fedha kwa Mabaraza ya Miji.

b. Kwa mujibu wa sheria zinazotawala Mabaraza na Halmashauri zetu Sheria namba 3 ya mwaka 1995 na Sheria namba 4 ya mwaka 1995, makadirio yao yote ya mapato na matumizi hayatoweza kuwa halali kabla ya kupitishwa na Kamati husika, Baraza la Madiwani na kuidhinishwa na Waziri husika anaeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na hili linafanyika katika Mabaraza yote na Halmashauri zote.

c. Mabaraza katika ukusanyaji wa mapato hutumia vitabu vya risiti ambavyo vyote huwa na vielelezo mahususi na vyenye kutambulika na pia ukaguzi wa mara kwa mara hufanyika ili kuondoa udanganyifu. Utaratibu wa utoaji wa risiti kwa sasa ndio unaotumika ukisaidiwa na uwepo wa *"database"* la vyanzo vya mapato kwa kila Serikali ya Mtaa na uwekaji wa kumbukumbu vizuri.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi moja ya nyongeza kuuliza swali hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa Mabaraza yetu takriban mengi yana mapungufu ya utunzaji wa fedha. na kwa kuwa wananchi wanahitaji kutunziwa fedha zao kwa umakini.Je, Mhe. Spika, ni utaratibu upi unaofanywa ili kuona Mabaraza yanapata maafisa au watendaji wenye sifa za uhasibu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kama atafatilia katika majibu yangu ya swali mama nilisema kwamba, hivi sasa Wizara yangu imeshafanya utaratibu wa kupeleka wahasibu wenye taaluma na wachumi wenye taaluma katika taasisi karibu ya zote za Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Miji. Hivi sasa zoezi hilo linaendelea katika Halmashauri zote, wapo wataalamu wenye sifa za uhasibu na wachumi wenye lengo la kukuza mapato katika Halmashauri zote. Zoezi hili linaendelea mpaka pale Mabaraza yatakapopata wataalamu wa kutosha kulingana na mahitaji yalivyo sasa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hapo kabla Mabaraza ya Miji, Manispaa pamoja na Halmashauri zilikuwa na vyanzo vingi vya kutosha vya mapato, baada ya kuona mradi wao una legalega, kuanzia sasa wanaimarisha watendaji wenye taaluma na wenye uwezo. Wakisha kukamilisha hilo, vile vyanzo vya mapato vilivyokuwa chini ya taasisi hizi, vitarejeshwa kule kule.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi. Kwamba moja kati ya sababu zilizosababisha baadhi ya vyanzo vya mapato

vya Mabaraza ya Halmashauri kupelekwa kwenye serikali kuu ni upungufu wa wataalamu kuweza kuvifanyia kazi. Ndio maana sisi tumeshakamilisha utaratibu wa sera na tunakuja na sheria zinazohusu serikali za Mitaa ambazo zitazingatia hayo masuala ambayo yatarejesha vianzio vya mapato. Katika Halmashauri hasa kwa kuzingatia wakati huo, tutakuwa tayari na wataalamu wa kutosha.

Lakini kuna utaratibu mwengine pia wa kuweza kufanya hata kwa vile vianzio ambavyo vitaonekana kwamba haviwezi tena kurudi katika Halmashauri kuna utaratibu katika nchi nyingi za nje, kuna utaratibu wa kuweka asilimia maalum inayokusanywa na Serikali Kuu kurejeshwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri, mwishoni alieleza kuwa wapo mbioni katika kuleta Sheria za Tawala za Mikoa. Lakini suala hilo Mhe. Waziri, imekuwa ni gumzo kubwa na muda umekuwa mrefu.

a) Je, Mhe. Waziri, huoni ku-*delay* muda mrefu ni kuvunja sheria ambazo huko nyuma tayari zimekuwa zinatakiwa zifanyiwe kazi kutokana na wakati tuliokuwa tunao.

b) Mhe. Waziri, utanikubalia kwamba sheria za nyuma ambazo wewe mwenyewe umezieleza za mwaka 1995, ni sheria ambazo hivi sasa zimeshapitwa na wakati. Ni lini utaweza kutuletea hapa katika Baraza lako tukufu ili tukaweza kubadilisha mfumo huo wa nyuma na tukaleta mfumo mpya ambao tunaokwenda nao wakati huo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nataka nikubaliane na Mheshimiwa Mjumbe, kwamba sheria tulizonazo zimeshapitwa na wakati. Sheria pia kutokuletwa katika kipindi cha muda mrefu kweli inachangia katika kuleta ufanisi wa utendaji na serikali na Mabaraza ya Miji.

Lakini nataka nimuhakikishie kwamba sheria hizi tunazotaka kuzileta katika kipindi kijacho cha Baraza la Wawakilishi zipo tayari. Hatua inayofuata sasa ni kuzipeleka kwa wadau na tukimaliza tutazileta kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kupata maoni yao na hatimaye utaratibu wa kiserikali utafanyika.

Mhe. Spika, kutokana na jambo hili kuzungumzwa sana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nitakuomba wakati utakapofika, kwenye mkutano

wa Bajeti ambao huwa si aghlabu kufanya kazi za kutunga sheria kwa umuhimu wa sheria hizi. Tutaomba tuje tuzilete kwa hati ya dharura, ili tuweze kuzipitisha na Mabaraza na Halmashauri ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Hilo ni ombi ambalo linaweza likaletwa baadaye na Wajumbe itabidi mje mnikubaliye jambo hili hasa kutokana na umuhimu huu.

Kama nilivyokwisha kusema kwamba sheria kweli zilizokuwepo sasa zimeshapitwa na wakati. Ndio maana tumefanya juhudi ya kutunga sheria ya Serikali za Mitaa ambayo tunataka tuilete ndani ya Baraza hili.

Nam. 9

Tatizo la Mlundikano wa Mahabusu

Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Aliuliza:-
Kumekuwa na idadi kubwa sana ya mrundikano wa mahabusu *(Remandees)* katika Chuo cha Mafunzo cha Kilimani. Mrundikano ambao kwa kiasi kikubwa huchangiwa na mapungufu ambayo yanazikabili Mahakama zetu kucheleweshe kesi na hivyo kusababisha ugumu katika uendeshaji wa Chuo hicho. Kutokana na gharama kubwa zinazohitajika kuhudumia mahabusu hao sambamba na wanafunzi wa Chuo hicho.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuona kwamba kadhia hii inapatiwa ufumbuzi huku tukiamini kuwa kucheleweshe haki ni sawa na kuikataa haki *(Justice delayed is Justice denied).*

(b) Sheria inasemaje kuhusiana na ukomo wa muda ambao mtuhumiwa hutakiwa kukaa Rumande.

(c) Serikali haioni kwamba ni muda muafaka sasa wakaanzisha adhabu/ hukumu mbadala kama vile kuitumikia jamii kwa watu wanaotuhumiwa kwa kesi ndogo ndogo, ili kuondokana na msongamano wa Mahabusu katika Vyuo vya Mafunzo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 9 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo. Lakini kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, mrundikano wa mahabusu *"remandees"* katika Vyuo vya Mafunzo Zanzibar hakuchangiwi na mapungufu ambayo yanazikabili

Mahakama pekee yake. Kwani suala la utoaji haki hushirikisha taasisi nyingi kama vile jamii wenye wajibu wa kufika Mahakamani kutoa ushahidi pale wanapoitwa, jeshi la polisi lenye jukumu la kufanya upepelezi kwa wakati, kuwepo kwa zana na wataalamu wa kutosha wa kufanya kazi zinazohitaji utambuzi wa kitaalamu n.k.

Siku zote anapofikishwa mtuhumiwa yeyote Mahakamani jambo la awali linalozingatia ni kumpatia mtuhumiwa dhamana kwa yale makosa ambayo Kisheria yanaweza kutolewa dhamana. Hata hivyo kuna changamoto mbali mbali ambazo huzifanya Mahakama kutompa dhama mtuhumiwa kama vile washtakiwa kushidwa kutimiza masharti yanayotolewa na Mahakama na hivyo kusababisha mtuhumiwa huyo awepo kizuizini hadi kesi yake itapomalizika.

Baada ya maelezo hayo sasa namjibu kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, hatua zinazochukuliwa na serikali kuona kwamba suala la mrundikano wa mahabusi unapungua ni kuongeza elimu kwa raia wake ili kuepuka kufanya makosa ambayo yatawasababishia kushtakiwa Mahakamani. Vile vile, kuchukua hatua nyengine za kisheria ambazo zinaweza zikasaidia mrundikano huo Mahakamani.

b) Hakuna ukomo uliowekwa wa kisheria kwamba mtuhumiwa kukaa rumande, hata hivyo kwa mujibu wa kifungu Nam. 209 (2) cha Sheria Nam.7/2004 kimeelezewa kwamba kesi yeyote ambayo sheria imeweka dhamana inatakiwa iwe imeanza kusikilizwa ndani ya miezi minne, vyenginevyo mtuhumiwa anatakiwa kuachiliwa na Mahakama. Lakini bado kumetoa ruhusa kwa upande wa mashtaka kumfikisha tena Mahakamani pale ambapo upelelezi wao sasa utakuwa umekamilika.

c) Mhe. Spika, tayari serikali imeanzisha adhabu mbadala kwa wakosaji wa makosa madogo madogo kutumikia jamii. Hata hivyo sharti mojawapo ili mtuhumiwa kutumikia adhabu hiyo ni kukubali mwenyewe kwa hiyari yake kwamba amefanya kosa hilo na hapo sheria kwa mujibu wa kifungu cha 318 cha adhabu kinaweza kikakubaliana na Hakimu ili kumpa adhabu mtuhumiwa huyo katika kutumikia jamii.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa amekiri kwamba suala la utoaji wa haki linahusisha taasisi mbali mbali. Tunafahamu kwamba kuna *quorum* ya pamoja baina ya

polisi, Ofisi ya *DPP* na Mahakama ili kuona pale panachangamoto katika *process* ya kutoa haki, *quorum* hii hukaa na kuzifanyia kazi changamoto hizo ili haki iwe inatendeka kwa wakati.

Mhe. Waziri, ni kwanini *quorum* hii haijakaa kwa muda mrefu sana sasa. Inasemekana kwamba Idara ya Mahakama ndio wakuu ambao wanakwepa *quorum* hii.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ni kweli kuna kamati inayoitwa Kamati ya Kusukuma Kesi. Kamati hii kweli imeundwa na *DPP*, Polisi, Mahakama na Ofisi yetu pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Kamati hii imeshawahi kukaa na mimi ndio niliyoi-*chair* hivi karibuni. Baada ya kukaa tukaona matatizo mengi yaliyokuwepo, tukatoa maelekezo na kukubaliana kwamba kamati kama hii ikutane Pemba ili tupate kutoa maamuzi ya pamoja katika suala hili ili liwe limejumuisha Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kweli Pemba hatujawahi kwenda kwa sababu kulikuwa na kipindi kigumu hapo nyuma, kulikuwa kuna hili suala la sherehe. Kwa hivyo, watu wengi walikuwa wana shughuli mbali mbali. Naamini kwa sababu sherehe tumeshaimaliza vizuri *Alhamdulillahi*, hivi karibuni tutafanya safari hiyo ili na wale wenzetu wa Pemba tukae nao ili tuweze kujua matatizo yao ni nini ili kwa pamoja tuweze kujua tutayatatua vipi matatizo hayo ya Unguja na Pemba. Kwa hivyo, hiyo ndiyo hatua ambayo hivi sasa imefikia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya mwanzo kabisa kabla ya kuuliza swali hilo, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyotuwezesha tukawa hai na kuvuta pumzi zake alizotuazima, ingawa hatujui wakati gani anaweza kuzichukua, dakika gani au saa gani.

Kwanza nataka nitoe pole kwa Mhe. Fatma Mbarouk Said wa jimbo la Amani, kwa kufiwa na mwanawe kwa kifo cha uzazi, Mwenyezi Mungu amlaze marehemu mahali pema Peponi. *Amin.*

Pia, nataka niwaombe Wajumbe wenzangu pamoja na wananchi wa jimbo la Makunduchi na wananchi kwa jumla, tumuombee dua Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma), mwanzo alikuwa kalazwa hospitali ya Mnazi Mmoja na baadaye akapelekwa Muhimbili na hivi sasa yupo Afrika ya Kusini. Mwenyezi Mungu amjaalie hali yake iendelee vizuri na ampe afya njema.

Baada ya hapo Mhe. Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Ofisi ya *DPP* kwa kushirikiana na Polisi walianzisha mpango wa kukamata watuhumiwa baada ya kukamilika kwa uchunguzi. Madhumuni yake makubwa ni kupunguza mrundikano wa Mahabusu katika gereza letu.

a) Je, mpango huu unaendelea au umekufa.

b) Upo ushahidi wa kutosha wa watu wanaowekwa Mahabusu kwa muda mrefu kuliko hata adhabu wanazostahiki kupewa. Ikiwa kama wanapatikana na hatia, kwa nini Mahakama zetu hawana muda wa kukamilisha haraka suala hili kwa kushirikiana na polisi. Utamkuta mtu yupo Rumande anatumikia miaka miwili au mitatu baadae anaachiwa kwamba hana kosa. Je, muda wote aliokuwemo mle analipwa fidia mtu yule.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika,

a) Ofisi ya *DPP* na Polisi, kwa kushirikiana na Wizara yangu, mpango huo ni kweli tulikuwa nao na tunao. Lakini utaratibu huu ni lazima uchukue mazingira ya nyumbani. Huwezi tu moja kwa moja kufanya hivyo kama wanavyofanya wenzetu ambao wamepiga hatua kubwa katika masuala haya. Tunachofanya hivi sasa kwamba anapofanya mtu kosa, kwa usalama wake na kwa usalama wa taifa anahifadhiwa kidogo. Huwa tunatizama ile kesi yake pamoja na lile tendo ambalo amelifanya. Tukihisi kwamba linaweza likamfanya kwamba abakie nje wakati uchunguzi unakwenda, hiyo tunafanya. Na ni kesi nyingi ambazo tunazifanyia hivi.

   Lakini pale tunapohisi kwamba haiwezekani kumuweka nje wakati uchunguzi unakwenda kutokana na sababu mbali mbali.Kwa hivyo, hapo bado mtuhumiwa yule atabaki Rumande wakati uchunguzi unaendelea. Mara nyingi hutia wakili na pale wakili wanapofika Mahakamani huzungumza mbele ya Mahakama na Mahakama ikiona kwamba sababu zao ni nzuri, basi anaachiwa kwa dhamana.

b) Ni kweli Mhe. Spika, inaweza ikatokea kwamba mtu yupo mahabusu kwa kipindi kirefu, lakini hatimaye pengine akaachiliwa. Kutokana na sababu ambazo nimezieleza katika swali lako la mwanzo. Hii tumeona kwamba inaweza ikaleta athari kwa mshtakiwa au mtu humiwa. Inapotokea hivyo

mtuhumiwa bado ana haki ya kisheria, kwenda Mahakamani na kudai kuwekwa Rumande kinyume ya utaratibu. Anaweza akadai fidia na anaweza akadai haki nyengine mbele ya Mahakama.

Kutokana na hayo kwa sababu tunajua kwamba mtu anaweza akadai tunajitahidi sana kuyaepuka haya isipokuwa pale tu ambapo tunahisi kwamba kumuweka ndani mtuhumiwa yule na wakati kesi inaendelea kuchunguzwa itakuwa ni kwa faida ya serikali na kwa faida ya taifa. Lakini watuhumiwa wengi sasa tunawaachia kwa dhamana na kesi zao zinaendelea wakati wao wako nje ya Rumande.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini na mimi nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa miongoni mwa upatikanaji wa haki ni Mahakama kuweza kuwa na fedha za kutosha ili kuweza kuwaita mashahidi ili waje kutoa ushahidi katika kesi. Lakini tumeshuhudia kwamba mara nyingi Mahakama hazina fedha za kutosha ili kuweza kuwapata mashahidi kuja kutoa ushahidi wao. Je, serikali imejipanga vipi kuona inaziwezesha Mahakama ili ziweze kufanya kazi zake na ziweze kuondoa kadhia hii ya mrundikano wa mahabusu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, uendeshaji wa kesi una maeneo mengi, moja ni kupata mashahidi na unapomwita shahidi ni kweli unahitajia fedha za kumlipa, kumkimu. Fedha ilikuwa ni kikwazo kidogo, lakini ninashukuru serikali katika kipindi cha mwaka uliopita tumepata fedha za kiasi si kwamba zinatosheleza, lakini ni za kiasi za kusaidia sehemu kubwa.

Lakini pia, mashahidi wetu wanaokuja wengi tunajaribu kuzungumza nao na wanatoa ushahidi bila hata hizo fedha za kukimu, lakini tunawaomba na tunapotiliwa fedha tunawalipa. Ninashukuru safari karibu asilimia sabiini ya wale ambao waliokuwa wanadai tumeshawalipa kwa mpango huo. Kwa hivyo, bado tunaendelea na tunashukuru serikali imepata fedha za kusaidia sana katika suala hili na mashahidi wetu tunawaita kwa misingi hiyo na wao tunawashukuru wanatusaidia katika kutekeleza wajibu wetu.

Kwa hivyo, sasa tuna utaratibu huo na katika bajeti inayokuja pia tumeliona suala hili na tumeomba fedha zaidi ili kuwamalizia fedha zao wale ambao wanaotudai na kuwa na akiba ya fedha za mashahidi ambao tutawaita katika kesi mbali mbali.

Nam.12

Upekuzi wa Gari katika Hospitali Mnazimmoja

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 1

Ahadi ya ZAWA kupeleka maji Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwanza nataka niwape pole wananchi wa Jimbo la Muyuni ikiwemo Pete, Jozani, Muongoni, Kitogani, Muyuni 'A' 'B' na 'C' na Bwejuu kwa kukosa maji muda mrefu pamoja na jitihada anazochukua Mwakilishi huyo.

Wananchi wa Jimbo la Muyuni, Shehia za Kitogani, Muungoni, Jozani na Muyuni kwa muda mrefu wanahangaika kupata huduma ya maji. Jitihada kubwa imefanywa kupitia Mwakilishi wao kushirikiana na Mamlaka ya Maji (ZAWA), ikiwemo kuchangia fedha zake mfukoni bila ya mafanikio yoyote.

Wananchi wa Muyuni wameshapeleka malalamiko yao ZAWA bila kusikilizwa na hakuna hatua za maana zinazochukuliwa kutatua suala hilo.

a) Wananchi wa Muyuni wameikosea nini ZAWA mpaka ishindwe kuwapelekea huduma ya maji kwa muda mrefu, licha ya juhudi na kilio chao na Mwakilishi wao.

b) Kitendo cha ZAWA kuchukua muda mrefu kutatua shida ya maji kwa wananchi wa Muyuni, licha ya mashirikiano ya hali na mali na Mwakilishi wao, siyo sawa na kuwadharau wananchi hao.

c) ZAWA imepungukiwa na nini mpaka leo inachelewa kutekeleza ahadi yake kushirikiana na Mwakilishi wa Muyuni kumaliza kero ya maji kwa wananchi wa Muyuni.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 1 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, Shehia za Kitogani, Muungoni, Jozani na Muyuni ni miongoni mwa vijiji vilivyopata huduma ya maji safi na salama kupitia mradi uliosaidiwa na serikali ya Abudhabi iliyojengwa katika miaka ya 1990 na

kuanza kutumika rasmi katika mwaka 1990. Mradi umekuwa ukifanya kazi zake vizuri muda wote tokea ulipoanza hadi leo. Kutokana na ongezeko la watu na mahitaji baadhi ya vijiji huduma hiyo haipatikani vizuri.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji inaendelea na jitihada mbali mbali za kuwasambazia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Pamoja na jitihada hizo kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo hilo Jaku Hashim Ayoub pamoja na wananchi wa jimbo hilo.

Mhe. Spika, miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na zile za hivi karibuni ambazo wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji imefanya ukaguzi wa pango la Kitogani ili kuangalia uwezekano wa kulitumia pango hilo kama ni kianzio cha maji ili kuongeza kiwango cha maji katika jimbo hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kutokuwa na afya na hayakidhi swali la msingi kama nilivyoliuliza, lakini anavyoanguka ndivyo anavyochinjwa, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri, hili swali lilikuwa katika kikao kilichopita, lakini bahati limekuja muda huu, swali ambalo limekuwa wananchi wa Jimbo la Muyuni, baada ya kushughulikia kilimo, muda wao mrefu unapotea kwa kuhaha kwa maji na jitihada ninafikiri umezisikia zilizofanywa na Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni sina haya ya kujisifu. Baada ya kumaliza kikao hiki utakuwa uko tayari kufuatana na mimi mguu kwa mguu kama ikiwezekana leo hata kesho, lakini unipangie muda kwa gharama zangu mimi mwenyewe kwa kushirikiana na Mbunge wangu. Je, uko tayari kufuatana na mimi unipe muda ambao wananchi wanasikiliza Jimbo la Muyuni kujua kadhia hii yao inayowasumbua kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, lakini kabla sijamjibu nirejeshe shukurani kwa wananchi wa Jimbo la Muyuni kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji na kuhakikisha kwamba Muyuni na Kitogani wanapata huduma hiyo ya maji safi na salama. Mhe. Spika, nasema kwamba nitashirikiana na Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni kwa hali na mali na niko tayari kufuatana nae kwenda kuangalia tatizo hilo na kulishughulikia kama inavyostahiki.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ismail: Nataka kumuuliza anambie lini leo, kesho au keshokutwa wananchi wanasikiliza kule.

Mhe. Spika: Hiyo mtapanga Mheshimiwa. Hebu pangeni wakati muafaka ambao mtaona mwende huko.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kabla ya yote nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika katika kikao hiki kwa afya njema na salama.

Lakini kabla sijenda kwenye swali Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutimia miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini pia nisiwe mwizi wa fadhila nichukuwe nafasi hii niipongeze Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu wao waliokuwa waandalizi wakubwa sana na kwamba niseme tu kwamba sherehe hizi za miaka 50 zilifana vizuri sana na wananchi waliitikia wito na wakahakikisha kwamba wanasherehekea uhuru wao wa mwaka 1964. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, sasa naomba kuuliza swali kama hivi ifuatavyo:-

Atakubaliana nami Mhe. Naibu Waziri, kwamba kwa maelezo yake mama ya tokea mwaka 1998 kuhusu habari ya ZAWA, je, atakubaliana nami kwamba kuna haja ya kuangalia ni maeneo yepi na yepi ambayo hayajapatiwa maji kwa sababu tumeona sehemu nyingi sasa kuna mradi huu wa maji, lakini unaona kuna manung'uniko ya hapa na pale, je, atakubaliana nami kwamba ni vyema sasa Wizara hii husika ika-*survey* vizuri kuhakikisha ni kijiji gani na gani ambacho hakijapatiwa maji mpaka hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, naomba nikubaliana na wazo la Mhe. Mwakilishi, la kupitia hapa na pale vijiji vyote kujua kijiji gani ambacho hakijapata huduma hiyo na kuwafikishia. Lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama nilivyoeleza hapo awali ni kuhakikisha kuwasambazia wananchi wa mijini na vijijini huduma ya maji safi na salama. Katika kupitia kuangalia ndani ya vijiji hivyo ni moja ya juhudi na jitihada za kutaka kuwapelekea wale wananchi ambao hawajaipata huduma hiyo. Kwa hivyo, niko pamoja na Mwakilishi kwa wazo hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri, swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwamba kama kuna Mwakilishi analalamika kuhusu matatizo ya maji jimboni, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anaongoza kwa mwaka na yuko mstari wa mbele kutoa hata mchango wake kwa ajili ya kusaidia Mamlaka ya Maji (ZAWA).

Naomba Mhe. Naibu Waziri, anambie kimsingi tatizo la ZAWA ni nini. Kwa nini wananchi wa Muyuni wanakosa maji wakati Mwakilishi wao anaongoza kuchangia fedha taslim kwa ajili ya ZAWA, naomba unambie tatizo nini.

Lakini pili, kama mmeshindwa kuwapatia maji wananchi wa Muyuni, utakubaliana na mimi kwamba sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Zanzibaar hawakufaidika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naomba niseme rasmi kwamba wananchi wa Jimbo la Muyuni hawana ukosefu wa maji wana tatizo la upungufu wa maji, lakini maji safi na salama yanapatikana, si kama hakuna kabisa kabisa, isipokuwa kuna upungufu huo. Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji, tumeshaliona na tunafatilia.

Kwa sababu sasa hivi lipo pango ndani ya Shehia ya Kitogani ambalo tayari Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji wameshafika hapo,wameshafanya utafiti na wakati wowote kuanzia muda huu Mamlaka ya Maji itarudi tena hapo kwa kwenda kumwaga maji hayo kujua kiwango chake kilivyo na baadae kuyaunganisha kwa wananchi.
Swali la pili, naomba Mhe. Mwakilishi, ulirejee kidogo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ni kwamba juzi tu wananchi wamesherehekea sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Zanzibar yetu na moja kati ya msingi wa sherehe zile za Mapinduzi ni kupata maji safi na salama. Wananchi wa Muyuni hawana maji ingawa wewe unasema kwamba kuna upungufu, wananchi wa Muyuni wana upungufu wa maji. Swali langu ni kwamba utakubalina nami kwamba wananchi wa Muyuni hawakufaidika na sherehe za miaka 50.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija, swali lake la nyongeza. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri, kwa majibu yake ya kusema kwamba wananchi wa Jimbo la Muyuni hawana tatizo la ukosefu wa maji, wana tatizo la upungufu wa maji. Na matatizo haya ya upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo yetu yapo na serikali inaikubali kwamba changamoto hii ni moja kati ya changamoto kubwa ambayo tunakabiliana nayo Zanzibar.

Na serikali haikukaa kimya katika kulifatilia hili tatizo la upungufu wa maji na ndio maana inahangaika na kutafuta mbinu mbali mbali za kuweza kukabiliana na changamoto hizi.

Sasa kuwepo kwa changamoto haimaanishi kwamba hakuna mafanikio ya miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, yapo mafanikio mengi na makubwa ambayo yamepatikana katika kipindi cha miaka 50 hii. Sasa mimi nadhani tukubaliane nae kwamba kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, kwamba Mamlaka ya Maji sasa hivi inalishughulikia hilo suala la upungufu wa maji katika Jimbo la Muyuni.

Na mimi bado sijafahamu kigezo cha Mwakilishi ambaye anayefatilia kwa kiwango kikubwa kuchangia maji kwa wananchi wake. Nadhani labda tuseme tu kwa sababu wengine hatusemi sasa kigezo kinaweza kikapatikana baada ya hasa kujulikana nani hasa anatoa fedha nyingi kwa ajili ya kuwashughulikia wananchi wa jimbo lake kuhusu matatizo ya maji.

Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi, akubaliane na sisi kwamba serikali tunalishughulikia jambo hili, lakini upo ushahidi kwamba kufikia miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, yapo mafanikio makubwa sana katika nchi yetu ya Zanzibar.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria za Haki Miliki za Wagunduzi wa aina Mpya za Mbegu za Mimea na mambo mengine yanayohusiana na hayo

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Idara Maalum za SMZ: (Kny. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, naomba kuwasilisha mswada wa sheria ya Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria za Haki Miliki za Wagunduzi wa aina Mpya za Mbegu za Mimea Zanzibar, yaani *plant breeders right act.*

Mhe. Spika, Utangulizi kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu mswada wa sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa aina Mpya za Mbegu za Mimea Zanzibar ya mwaka 2014, sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea zimetayarishwa ikiwa katika hatua ya kutambua umuhimu wa kuwaenzi na kuwazawadia watafiti na wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kutokana na kazi ngumu naya miaka mingi.

Mwaka 1961 nchi kadhaa za Ulaya zilikutana mjini Paris na kukubaliana kuwa na mfumo wa aina yake ya kipekee yaani Suwi *Generic System* wa kutoa na kulinda haki miliki kwa ajili ya wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Mwaka huo nchi hizo zilipitisha mkataba wa kitaifa wa kulinda haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mimea.

Mhe. Spika, mkataba huu ambao unasimamiwa na Shirika la Kimataifa la haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea yaani *the international union for the protection of new varieties of plan*, yaani *UPOV*. Lengo kuu la uanzishwaji wa mfumo huo ni kuhakikisha kuwa nchi zinaridhia zinakua na utaratibu wa haki miliki unaofanana na hivyo kuwawezesha kushirikiana katika kulinda haki miliki na hasa katika kuendesha majaribio yanayomuwezesha mgunduzi kupata haki miliki pamoja na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje, kutafiti mbegu bora na hivyo kuleta Mapinduzi ya Kilimo hapa nchini.

Mhe. Spika, kutokana na manufaa yanayopatikana ya kuwa mwanachama wa Shirika la *UPOV* hususan kufikia Mapinduzi ya Kilimo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari 2010 limeridhia mkataba ya Shirika hilo. Ili Tanzania iwe mwanachama wa Shirika la *UPOV* linatakiwa kuanda sheria ambazo zitakwenda sambamba na mkataba wa *UPOV*.

Kwa kuwa Tanzania Bara tayari wameshapitisha sheria ya haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea Zanzibar inalazimika kuwa na sheria kama hivyo kwa ajili ya kujiunga na shirika hilo.

Madhumuni ya kutungwa kwa sheria ya haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, madhumuni ya kutungwa kwa sheria ya haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ni hizi zifuatazo.

Moja kuweka mfumo ambao utakuwa unawatambua na kuwalinda wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea yaani *plant breeders* walioko na wanaokuja nchini na kulinda haki miliki zinazowahusu wagunduzi hao ili kuongeza hamasa katika ugunduzi wa mbegu mpya zinazokidhi mahitaji ya wakulima na masoko na hivyo kuongeza uekezaji kwenye sekta ya kilimo.

Tatu, kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika uzalishaji na biashara ya mbegu hapa nchini.

Nne, kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu ikiwa ni pamoja na matokeo ya majaribio ya kitaalam yanayowezesha upatikanaji wa haki miliki. Aidha

kuwa mwanachama wa *UPOV* kutawezesha upatikanaji wa teknologia mpya za utafiti za ugunduzi wa mbegu mpya kutoka nchi zinazoendelea.

Tano, kutungwa kwa sheria hapa Zanzibar pamoja na sheria kama hiyo ambayo imeshatungwa Tanzania Bara zinaendana na mkataba wa *UPOV* wa 1991 kutawezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza masharti ya kujiunga na Shirika la *UPOV* na kupata manufaa yanayotokana na uanachama huo.

Mambo muhimu yaliyozingatiwa katika mswada wa sheria. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, mambo mengi muhimu yaliyozingatiwa katika mswada huu ni haya yafuatayo:

Kuanzishwa Ofisi ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea.

Ofisi ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea imependekeza kuanzishwa kama ilivyotajwa katika kifungu namba 3 cha mswada wa sheria ikiwa ni chombo kikuu kitakachokuwa na jukumu la kusimamia kwa karibu utekelezaji wa sheria hii, kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea zinalindwa ndani ya Zanzibar kwa wakati wote. Rajisi itakuwa na msimamizi wake mkuu ambaye ni Mrajisi wa Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina mpya za Mbegu za mimea.

Pili, kuwanzishwa kamati ya ushauri ya Haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea yaani *plant breeders right adviser recommity*. Kamati ya Ushauri ya Haki Miliki ya Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea itakuwa ni chombo cha ushauri kama ilivyopendekezwa kuanzishwa katika kifungu namba 9 cha Mswada wa Sheria ya Haki Miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Majukumu makuu ya kamati ya ushauri ni kumshauri waziri juu ya utekelezaji wa sheria hii, kupokea ripoti za maombi kutoka kwa Mrajis na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mrajis juu ya utoaji wa haki miliki.

Kuanzishwa kwa Bodi ya Rufaa yaani *Appeal Board*, Mswada wa Sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea umependekeza kuanzishwa kwa Bodi ya Rufaa ambayo itakuwa na wajumbe watano. Wawili wakiwa ni wataalam katika masuala ya sheria na watatu ni wataalam katika fani ya sayansi ya kilimo, ambapo Waziri anayehusika na masuala ya kilimo atakuwa na uwezo wa kuteua mmoja kati ya wajumbe kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Rufaa.

Bodi ya Rufaa itakuwa na uwezo wa kutayarisha kanuni na taratibu zake kuitisha na kulinda mashahidi wanaohudhuria katika Bodi, kulazimisha uwasilishaji wa nyaraka na kusimamia kiapo kwa shahidi.

Nne, kuweka utaratibu wa kuwasilisha maombi pamoja na kushughulikia maombi ya usajili wa haki miliki za ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina mpya za Mbegu za Mimea umeweka utaratibu wa kuomba haki miliki wa aina mpya za mbegu za mimea kama inavyoonekana katika kifungu namba 19 cha mswada huu, ambapo muombaji atalazimika kutoa jina lake kamili pamoja na anuani yake. Jina analotaka kulitumia kwa aina hiyo mpya ya mbegu kuwasilisha *sample* ya mbegu inayoombewa haki miliki na taarifa za ziada ambazo zinahusiana na aina hiyo mpya ya mbegu.

Pia, sehemu ya tano ya mswada wa sheria imeweka utaratibu wa kushughulikia maombi ya usajili wa haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Aidha mswada umeelezea ubatilishaji wa haki iliyotolewa kama inavyoonekana katika kifungu namba 37 cha mswada ambapo Mrajis anaweza kutangaza kuwa haki aliyoitoa imebatilishwa. Pia, Mrajis anaweza kusitisha hati aliyoitoa kwa mgunduzi wa haki miliki ya aina mpya ya mbegu za mimea kama inavyoonekana katika kifungu namba 38 cha sheria hiyo.

Hata hivyo sheria imempa uwezo mgunduzi ambaye ameshapatiwa haki miliki kuisalimisha haki hiyo kwa kuandika *notice* kwa Mrajis kama inavyoonekana katika kifungu namba 40 cha mswada wa sheria hii.
Tano, kuanzishwa mfuko wa maendeleo ya haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria wa Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea umekusudia kuanzisha mfuko wa maendeleo ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina mpya za mbegu za Mimea ambapo Waziri anayehusika na fedha, baada ya kupokea maombi kutoka kwa waziri anayehusika na masuala ya kilimo anaweza kuanzisha mfuko huo.

Lengo kuu la mfuko ni kuendeleza na kukuza wagunduzi wa aina za mbegu za mimea kama inavyoonekana katika kifungu namb 47 cha rasimu ya mswada huu. Pia, sheria hiyo imeweka utaratibu wa uundaji wa hesabu, usimamizi na ukaguzi wa mfuko huo.

Mapendekezo, Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Baraza lako tukufu lijadili na hatimaye liridhie na kupitisha sheria ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina mpya za mbegu za mimea ya mwaka 2014 ambayo imependekezwa.

Kuanzishwa kwa Rajisi ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina mpya za Mbegu za Mimea.

Pili, kuanzishwa kwa Kamati ya Ushauri ya Haki Miliki za Wagunduzi wa Aina mpya za Mbegu za mimea.

Tatu, kuanzishwa kwa Bodi ya Rufaa.

Nne, kuanzishwa mfuko wa maendeleo ya haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Hitimisho Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe kama nilivyosema hapo mwanzo waijadili na hatimaye wairidhie.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo naomba kusoma maoni ya Kamati kuhusu Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi kwa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na mambo mengine yanayohusina na hayo.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Utukufu na mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii ndani ya Baraza lako tukufu, kwa madhumuni ya kujadili Mswada wa Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Pia, nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Mswada huu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak, Katibu Mkuu,

Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji mbali mbali wa Wizara hii bila ya kuwasahau Wanasheria wa Serikali na wale kutoka Ofisi yetu ya Baraza la Wawakilishi, kwa mashirikiano yao na Kamati. Michango, miongozo na ufafanuzi wao juu ya mambo mbali mbali yaliyojitokeza wakati wa kuupitia Mswada huu yameweza kuisaidia sana Kamati yetu na kuifanya kazi yetu iwe nyepesi.

Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa wadau mbali mbali kutoka katika Sekta ya Sheria na Kilimo, kama vile Jumuiya ya Wanasheria wa Zanzibar (*ZLS*), Jumuiya ya Tiba za Asili (JUTIJAZA) pamoja na watafiti wa kilimo kwa mashirikiano yao na kuweza kutoa maoni na mapendekezo yao kwa Kamati yenye lengo la kuufanya Mswada huu wa Sheria uwe bora zaidi. Tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo ilifanya kazi kubwa ya kuujadili Mswada huu, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kutokana na mashirikiano yao wakati wote wa Kamati ilipokuwa ikipitia Mswada huu. Napenda kuwatambua Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu Haji - Mjumbe
4. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
5. Mhe. Hamad Masoud Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
7. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Mjumbe
8. Ndg. Haji Khatib Haji - Katibu
9. Ndg. Fatma Omar Ali - Katibu

Mhe. Spika, pia nachukua nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Kilimo na Maliasili pamoja na serikali kwa ujumla, kwa kuona umuhimu wa kuleta Mswada huu hivi sasa. Ni wazi kuwa Mswada huu utawanufaisha sana watafiti na wagunduzi wetu wa mbegu za mimea hapa nchini kwa kuweza kulindwa haki zao, kuongeza kipato, ari na motisha ya kazi zao.

Aidha, ni jambo la faraja pia kuona kuwa Mswada huu utawajengea uwezo wagunduzi wetu wa mbegu za mimea kwa kuongeza ujuzi na uzoefu wao, kwani kupitishwa kwa Mswada huu kutaweza kufungua milango mipya ya kuwawezesha wagunduzi wetu wa mbegu za mimea kupata fursa za kimafunzo katika nchi mbali mbali duniani. Wanachama wa Shirika la Kimataifa la Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*UPOV*) ambalo ndio chimbuko la Mswada huu.

Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo imesikitishwa sana na kasoro mbali mbali zilizobainika katika rasimu ya awali ya Mswada huu, zikiwemo kukosekana kwa mpangilio mzuri wa vifungu pamoja na kukosekana kwa vifungu muhimu; mambo ambayo yamepelekea kuchapishwa upya kwa Mswada huu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali, Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo ilipata fursa ya kukutana na wadau mbali mbali wa Sekta ya Kilimo na Sheria ili kupata maoni na mapendekezo yao juu ya Mswada huu wa Sheria ya Biashara Zanzibar. Na hii inatokana na fursa iliyotolewa na Kanuni ya 83(5) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Kwa ujumla wadau wote walitoa maoni mazuri yaliyolenga kuifanya Sheria hii tunayoiandaa iweze kutekelezeka kwa kufuata misingi ya haki, uwazi, ufanisi, uwajibikaji na utawala bora ili kuleta mafanikio katika suala hili la Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu Mpya za Mimea.

Miongoni mwa maoni yao yalikuwa kama ifuatavyo:

1. Katika kifungu cha kwanza, kuwekwe muda maalum ambao Waziri atatakiwa awe ameshaitangaza sheria hii katika Gazeti Rasmi la Serikali ili kuepusha kuchelewa kuanza kutumika kwa sheria hii,

2. Katika kifungu cha 9 (2) (a) wadau walishauri kuwa Wajumbe wa Kamati ya Ushauri wa Hakimiliki waachiwe wenyewe wamchague Mwenyekiti wao ili kukuza demokrasia katika Kamati hiyo na kuepusha Waziri kumteua mtu mwenye maslahi naye,

3. Wadau walionesha wasiwasi wao juu ya ugumu wa kutekelezeka kikamilifu kwa sheria hii kwa kuwa baadhi ya Jumuiya zilizoainishwa katika kifungu cha 9(2) (b) na 9(2) (c) hazipo hapa Zanzibar kwa sasa, ikiwemo Jumuiya ya Wagunduzi wa Mbegu Mpya za Mimea iliyosajiliwa na Jumuiya ya Wafanyabiashara wa

Mbegu iliyosajiliwa. Aidha, wadau walipendekeza kuongezwa kwa wawakilishi katika Kamati hiyo ya Ushauri wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu ambapo mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wazalishaji wa Mbegu na mmoja kutoka Jumuiya ya Tiba za Asili (JUTIJAZA),

4. Katika kifungu cha 55 kinachompa uwezo Waziri kuingia katika makubaliano na nchi mbili au zaidi na Mashirika ya Kimataifa au Masihirika yasiyo ya Kiserikali ili kurahisisha ushirikiano katika majaribio. Wadau wanaona kuwa mashirikiano na nchi za kigeni kunaweza kupelekea kuwa wagunduzi wa ndani kukosa Hakimiliki hasa pale unapotokea ulazima wa kupeleka mbegu kwa hatua zaidi za kiutafiti katika nchi hizo.

Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeupitia kwa kina Mswada huu, ambapo kimsingi inakubaliana na mapendekezo ya Mswada huu. Hata hivyo, kwa kuzingatia maoni ya Wajumbe wenyewe wa Kamati pamoja na maoni ya baadhi ya wadau, Kamati yetu imefanya marekebisho ya kimsingi na ya maandishi kwa lengo la kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi.

Mhe. Spika, naomba nieleze baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo Kamati yetu inaona yangefaa kufanyika

Mhe. Spika, kwanza katika kifungu cha 1. Kamati iliunga mkono maoni ya Wadau kuwa ni vyema kungewekwa muda maalum ambao utamfanya Waziri awe ameshaitangaza sheria hii ili kuepusha uchelewaji wa kutumika kwa sheria hii. Hivyo, Kamati ilipendekeza Waziri awe ameshaitangaza Sheria hii katika Gazeti Rasmi la Serikali ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kutiwa saini na Rais.

Katika kuifanya Kamati ya Ushauri wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu kuwa yenye ufanisi zaidi, Kamati ilipendekeza kuwa kifungu cha 9 (2) (a) kifanyiwe marekebisho ili kuipa nafasi wizara kutoa mwakilishi mwenye ujuzi na uzoefu mkubwa katika masuala hayo ya Kilimo. Aidha, ilipendekezwa Kifungu cha 9 (2) (g) kirekebishwe kwa kuingizwa mwanasheria wa wizara ambaye kwa vyovyote vile atakuwa ana uzoefu na masuala haya ya mbegu na kilimo kwa ujumla badala ya mwakilishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, kutokana na uzito wa majukumu ya Bodi ya rufaa, Kamati ilipendekeza marekebisho katika kifungu cha 44 (1) kwa kuongezwa idadi ya

wajumbe wa Bodi hiyo na kufikia hadi watano ambapo wajumbe wawili watakuwa ni wataalamu wa masuala ya kisheria na na wajumbe wengine watatu watakuwa ni wataalamu waliohitimu katika Sayansi za Kilimo.

Aidha, ilipendekezwa pia kuongezwa kwa kifungu cha 44 (3) (e) kitakachowapa uwezo wajumbe wa Bodi kuteua katibu miongoni mwa wajumbe mwenye utaalamu wa Sheria. Kamati pia ilipendekeza kuwa akidi ya kikao cha Bodi ya Rufaa isipungue wajumbe watatu.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali**,** kwa kuwa Mswada wa mwanzo ulihitaji kufanyiwa marekebisho mengi na ya msingi, Serikali iliamua kuuchapisha upya Mswada huo, na katika kufanya hivyo, serikali iliona pia ni vyema kuyazingatia kabisa maoni ya Kamati katika Mswada huu uliochapishwa upya ili kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi na kurahisisha mjadala wa Mswada huu katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yakiwemo ya kimaandishi na uchapaji yameshachukuliwa na wanasheria wetu kama yanavyoonekana katika karatasi ya mapendekezo ya marekebisho ya Kamati.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaunga mkono Mswada huu na inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote waungane nasi kwa kutoa maoni kadri watakavyoona inafaa na hatimaye kuunga mkono na kuupitiha Mwada huu muhimu**.**

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kutia baraka mswada huu ambao ni adhimu.

Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa uzima wako na afya pamoja na familia yako. Pia, niwashukuru Wajumbe wote kwa asubuhi hii Mwenyezi Mungu kutupa afya nyema na kuweza kukutana hapa kuzungumza kwa pamoja, huu ni wakati muafaka wa kuja mswada huu ambao kilio changu sana huwa nasema kuwa, sheria zilizokuwa zishapitwa na wakati basi watuletee sisi Wajumbe na kuweza kuchangia. Hilo nashukuru sana kwa mawaziri kutuletea miswada kama hii.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Waziri mwenyewe pamoja na Katibu wake, Naibu katibu, Naibu waziri wake na wataalamu nisiwasahau, lakini Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba niseme jambo moja ambalo napenda kulisema sana, suala la kutuletea miswada hii na kuunda mambo muhimu kwa mujibu wa sheria halafu wizara au waziri akawa yeye ndiye mkubwa zaidi

kuliko kile chombo kilichopitisha hapa. Mhe. Spika, hilo ni moja ninalolisema kwa sababu naona mambo mengi sana hapa tunayapitisha halafu baadae yanakuwa hayaendi katika utaratibu kama tulivyotoa katika Gazeti Rasmi.

Mhe. Spika, mimi nianze na ukurasa wa mwanzo kabisa kwa kuingia ndani lile jina fupi tu, lakini Mheshimiwa kuna mambo humu ambayo nimeyaona nataka Mhe. Waziri na wataalamu wake wanisaidie. Kwa sababu Mhe. Spika, lugha ni lugha, sheria ni sheria, sasa isifike pahala tukaja tukapingana ikawa hawa Wawakilishi wamepitisha bila ya kuangalia sasa hili kidogo linanitia wasiwasi.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa huu kama nilivyosema chini hapa kuna neno "muombaji". Ningeomba kidogo nikiseme ili kuweka sawa hayo tunayokusudia. Muombaji maana yake ni mgunduzi mwenye haki ya kufanya maombi ya kupatiwa hakimiliki za ugunduzi kulingana na maana ya "mgunduzi" kama ilivyofafanuliwa katika sheria hii.

Mhe. Waziri, naomba sana kwa kuwa mimi nakaa Kaskazini hebu anisaidie hii lugha mantiki yake hasa, au Kiswahili chake kilivyo. Kabla sijaanza kukiridhia naomba niweze kunufaishwa nisije nikapitisha jambo kumbe ikawa tafsiri yake nyengine kabisa tofauti na nilivyofahamu mimi.

Mhe. Spika, nikiendelea na tafsiri hiyo hiyo, ni mtu ambaye anayegundua au amevumbua na kuendeleza aina za mimea. Hapa mimi nimefahamu kidogo, kwanza ningemuomba sana Mhe. Waziri, tutapopitisha sheria hii tushuke chini kwa makusudi kwenda kuwapa taaluma wananchi wetu. Hili ni moja ambalo huwa tunalikosea halafu wananchi wanakuwa wanatusema kule nje, mmepitisha sheria lakini sisi hatuijui ufafanuzi wake ukoje. Mimi naomba sana Mhe. Waziri, anaye-*act* hapa hebu kwa makusudi aoneshe mfano, tukimpitishia sheria hii aende kwa jamii awaelimishe jinsi ya sheria hii ilivyo.

Wagunduzi au Wavumbuzi tunao wengi sana hapa katika kisiwa chetu, kwa kuwa sheria hii nimejaribu kuangalia sana kwa urefu na mapana nina wasiwasi ambao utakuwa badala ya kuwa mgunduzi huyu au mvumbuzi kuwa Mzanzibari baadae akaja akatokea Mzungu akawa na haki. Sasa sijui kama kifungu hicho kipo kinachomlinda Mzanzibari hapa, ingawa naendelea lakini kuna mambo mengine lazima nianze kuuliza mapema. Naomba hilo kama kipo kifungu hicho ni sawa na kama hakipo naomba tukiongeze katika kusaidia kuweka sheria iwe nzuri zaidi.

Kwa sababu nina uzoefu kuwa mambo mengi sana tunatunga hapa kwa kumjaalia yule mtu mwenye neema, lakini mwenye kile kisiwa chenyewe

anakuwa haneemeki, na kuneemeka watu wa nje ya kisiwa sasa inakuwa bure yao hiyo.

Mhe. Spika, sasa nije katika ukurasa wa 369. Ukurasa huo Mheshimiwa pana kitu "Mfuko", maana yake ni mfuko ulioanzishwa chini ya kifungu cha 47, sasa mfuko huo wa aina gani? Ningeomba hapa niwekwe wazi kabisa huo mfuko wenyewe hasa wa aina gani utakaokuwa unachangiwa na hawa wagunduzi au mfuko ambao watakuwa wanatoa wizara katika masuala yake haya ya kuwainua hawa wavumbuzi. Sasa ningeomba hapa mfuko huu kidogo nisaidiwe Mheshimiwa.

Lakini vile vile, hapa chini yake tunaambiwa "Mwakilishi wa Kisheria". Mwakilishi wa Kisheria maana yake ni msimamizi au mpokeaji wa kampuni, usimamizi wa mali ya marehemu mwakilishi ambaye atakayepewa *power* ya kuweza kusimamia hili suala au mwakilishi wa kisheria atakuwa wa aina gani? Hapa naomba kidogo kama yupo mwanasheria aje kuniambia kama mtu atakayepewa *power* katika aidha makampuni au wanafamilia, sasa huyu Mwakilishi wa Kisheria atakuwa ni yupi ambaye amekusudiwa katika sheria hii. Mimi naomba kidogo hapa niwekwe sawa ili niende sambamba na Mhe. Waziri.

Kwa sababu mambo mengi ameyaainisha humu, usimamizi wa marehemu , mwakilishi wa mtu ambaye ameshindwa kulipa deni, mambo mengi sana hapa, lakini hajamuweka vizuri na ndio hiyo *attention* yangu iko hapo. Sasa hivi naogopaogopa sana, siku hizi nakuwa mufti kidogo hivyo naogopa mambo mengine kukubali moja kwa moja tu.

Lakini nishuke chini hapa Mhe. Spika, kwenye hili neno "Rajisi" na "Mrajisi"; mana hapa tukienda mbele kuna mrajisi halafu unakuta rajisi. Mhe. Spika, nimejaribu kutafuta katika *dictionary* yangu ya kichwa rajisi bado sijapata taaluma yake. Sasa ndio kama ninavyosema kwamba kila mtu anakuwa anapenda kutafsiri alivyoona yeye kichwani mwake. Mhe. Spika, naomba sana kusema kwamba hapa chini rajisi maana yake ni rajisi ya kuwa na hakimiliki ya ugunduzi wa aina mpya ya mbegu , lakini mrajisi maana yake ni mrajisi wa hakimiliki ya ugunduzi.

Sasa naona hizi sentensi mbili hivi Mhe. Spika, ningeomba kwa sababu lazima niwe muangalifu, lakini kuna herufi kubwa ya R sasa sijui ni nini. Mhe. Waziri, naomba hapo anitanulie akili kweli kweli hapa si kitu cha mchezo nifahamu hii kitu urajisi una mantiki gani.

Nikiendelea Mhe. Spika, katika ukurasa wa 370 hapa anakwambia kwamba, Kuelezewa kwa sifa zinazotokana na asili au mchanganyiko wa asili.

Mheshimiwa, mantiki ya sentensi hii inatokana na aina ya mbegu, maana yake ni kundi la mbegu liliopo katika sehemu moja inayotambulikana iliyogaiwa bila ya kuzingatia masharti ya utoaji wa hakimiliki za ugunduzi wa kutimizwa yaweza kuwa. Sasa hapa chini wametuonesha hiyo.

Lakini (b) kutofautiana kutokana na aina yoyote ya kundi la mmea kwa maelezo ya sifa. Mimi hapa kwa nilivyofahamu kwamba hizo mbegu zenyewe ambazo zilikuwa zinataka kwa aliyekuwa mbunifu au mgunduzi aliyezigundua kuwa ziwe sifa fulani ambazo ziendane na sifa zenyewe, lakini hii asili ya kuwa labda ile mbegu nilivyofahamu mimi au atanifanyia *correction* labda na ile mbegu yenyewe aliyegundua kuwa imetokana na asili gani. Mhe. Spika, hapa Waziri anisaidie, nimesema mara hii Kiswahili changu kinanipa tabu kidogo.

Kwa hivyo, naomba sana kuwa anifahamishe kuwa, je, asili ya kuwa imetoka na nchi nyengine, asili ya ule ugunduzi wenyewe kuwa ile mbegu kaigundua kutokana na shamba jengine, hapa kidogo naomba nifafanuliwe Mheshimiwa. Mhe. Spika, nikirudi chini Sehemu ya Pili, uanzishwaji kwa ile ofisi yenyewe. Hapa mimi sina tatizo kwa sababu ni kitu ambacho kitakuwa kipya na hasa kutokana na wizara yenyewe husika ambayo ni ya kilimo, lakini namtafuta mrajisi.

Mheshimiwa hapa kutakuwa na mrajisi mwenyewe, lakini nikiangalia mrajisi waziri vile vile anaweza kumteua, na kwa sababu kutakuwa na mrajisi kwa mantiki ya kuwa ni mrajisi, na kutakuwa na naibu mrajisi ndivyo nilivyofahamu sentensi hii, lakini hizi sifa nazo japo kuwa huko mbele nimeziona naona limetiwa na neno sheria, sasa sijui sheria ile itakuwa inahusiana na ugunduzi au uvumbuzi. Tutafika huko Mhe. Spika.

Sasa hapa chini yake tumeambiwa kuwa madhumuni ya kifungu hicho vigezo vitakavyotakiwa vitajumuisha shahada ya kwanza. Hili nakubaliana nalo sina tatizo, lakini sasa hii sheria ni sheria ya aina gani iliyokusudiwa. Sheria ina upana mkubwa sasa sijasikia kama kuna sheria ya ugunduzi au sijui ndio kwanza tunataka tuitunge. Naomba Mhe. Waziri anisaidie kuwa iko sheria hiyo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria katuletea? Hapa ningeona kuwa huyu mtu ana fani ya sheria gani labda ningezidi kuona sheria ya aina gani.

Tunaambiwa ni sheria inayofanana, inayofanana nini? Tunakwenda *direct* kwenye mambo ya kilimo tutaambiwa vipi inayofanana na sheria hiyo. Sasa hapo naomba Mhe. Waziri, anisaidie hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, nikiingia katika nambari tano; kazi za mrajisi zitakuwa kutoa hakimiliki za ugunduzi wa aina mpya za mbegu na kusimamia rajisi. Narudia

pale pale hili neno rajisi ningeomba sana nipewe semina Mhe. Waziri ili kutaka kujua hii rajisi. Tungepewa semina mimi na Wawakilishi wenzangu tukalifahamu hili neno pamoja na wananchi. Bado mimi linanipa tabu sana hili neno.

Nikiingia ukurasa wa 371, naomba niende mbio mbio ili kuweza kuwapa nafasi na wenzangu. Mhe. Spika, hapa tumeelezwa kuwa kifungu cha (d) (i) yanahitajika na Sheria hii au Sheria nyengine yoyote kuingizwa katika rajisi. Sawa Mhe. Spika, hata na mimi naweza nikakwambia nina sheria yangu naweza nikaitoa, lakini kama nilivyokwambia kuwa nisije nikakosa uhondo nitapokuja kujibiwa pengine nitaweza kusimama kwa kutaka kuingiza sheria yangu ambayo niliiona katika rajisi baada ya kupata upeo wa hii rajisi kwa upana zaidi.

Hivyo na mimi naiweka pembeni sheria yangu kidogo ya kuweza kusaidia katika kifungu hiki baada ya kuleta sheria na kuongeza sheria. Hiyo mimi naomba hapo nikuachie ili nije kuweka sawa huko katika majibu yako mazuri sana na mimi nakujua wewe ni mtaalamu.

Mhe. Spika, ukurasa wa 372 tunaigundua hiyo hiyo rajisi na hakuna tatizo lolote kama nilivyosema kuwa mimi nakubaliana nalo baada ya maelezo nitakayoyapata kwa Mhe. Waziri, lakini nikiingia katika undani wenyewe wa kamati, wajumbe wa kamati watateuliwa na Waziri kushirikiana na mamlaka, angalau watatu miongoni mwao wawe wanawake na watakaojumuisha hali halisi.

Mhe. Spika, sasa hivi wanawake wamepiga hatua, kamati hii mimi ningeomba tusiseme angalau kuwapa nafasi kinamama. Kinamama sasa hivi wamesoma sheria, kinamama sasa wana fani nyingi tu. Sasa mimi nawapigia debe kuwa tusiseme angalau, ina maana tukisema angalau tumesha-*specialize h*ii nafasi iwe tatu ndio hao hao kinamama tutawanyima haki, pengine na wao wana mawazo mazuri sana ya kitaalamu tukaja tukafika pahala tukamkosa kwa watu watatu, lakini ukiongeza ukisema angalau *quorum* iwe nusu bin nusu ibakie baba na mama basi kidogo ingesaidia mawazo mazuri sana.

Mhe. Spika, naomba hilo, na wenyewe kumbe wanajijua wanajisikia. Ninaomba hivyo hili neno sijalikubali Mhe. Waziri, naomba sana hii lugha bado kwenye akili yangu haijanipa mantiki. Nasema angalau watatu miongoni mwao wawe wanawake, mimi sentensi hii sijakubaliana nayo Mhe. Waziri, naomba sana kuwe na *space* kubwa na wao kinamama ili waweze kujisikia.
Lakini ukurasa huo huo katika kifungu cha 10(d) katika kazi za kamati zitakuwa kama zinavyosomeka:

Kusimamia matumizi, ndio ile niliyosema mfuko wa aina gani wa fedha. Sasa hii kama nilivyosema kuwa nangojea jibu ule usimamizi wa mfuko wa fedha zenyewe zinatokana na uhalisia wa aina gani ili niweze kuja kuuchangia zaidi na hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, mimi niseme kwa leo sitokuwa na mengi sana lakini kwa kumalizia tu naomba sana sheria tunazozipitisha hapa basi zifuate mkondo wake. Kwa sababu mara nyingi sana tunatunga sheria, lakini hatimaye sheria zile hazifanyiwi kazi.

Mhe. Spika, wale wahusika ndio wazifanyie kazi. Sheria, haiwezi ikatoka kabisa, lakini wale wahusika ndio watoke waifanyie kazi ile sheria. Sasa mara nyingi sana Mhe. Spika, sheria nyingi tunazitunga hapa lakini mwishowe hazifanyiwi kazi. Naomba sana wahusika Mawaziri muwasimamie sana hawa watendaji wenu, mnatuletea sheria na hatimaye sheria zinakuwa zinakaa kwenye meza hazifanyiwi kazi. Sheria haziwezi kukaa tu muhusika ndiye aende akatekeleze wajibu wake.

Mhe. Spika, hili suala linasikitisha sana kutokana na hali halisi ilivyo. Kwa sababu kutokana na sheria nyingi zinakuwa nzuri, lakini hatimaye zinaishia kwenye *brief case* hazifanyi kazi kwa mujibu wa taratibu.

Naomba sana Mhe. Spika, kwa leo nifikie hapa niunge mkono pamoja na mapungufu niliyoyasema hapa niyapunguzie kidogo 99% kasoro moja naomba Mhe. Waziri, uje kunijibu ili wananchi wangu kule waweze kufurahika na suala hili.

Mhe. Spika, sheria nzuri na *alhamdulillah* nashukuru sana, sasa vijana wetu kupata ajira ya ugunduzi wa kutuletea mimea ambayo inakwenda na wakati, hivi sasa na kubadilisha muelekeo wa kilimo na kuleta mabadiliko mazuri sana. Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumtaja na kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima, na kwa mara nyengine tena kukutana katika chombo hiki muhimu ambacho kinapasa kulinda maslahi ya Zanzibar.

Pili, Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mchangiaji wa pili asubuhi hii wa Mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea na Mambo yanayohusiana na hayo.

Tatu, Mhe. Spika, nampongeza Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili kwa kuwasilisha mswada huu leo hii hapa Barazani. Ameuwasilisha vizuri na kimsingi umefahamika Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi naomba la mwanzo kabisa kulichangia katika mswada huu niseme kama kuna kengele ya kuwaamsha Wazanzibari kwa mara nyengine tena juu ya haja ya kuutizama upya mfumo wa Muungano na kurejesha katika mamlaka ya Zanzibar masuala yanayohusu Mambo ya Nje na Ushirikiano wa kimataifa, basi ni kuletwa kwa mswada huu katika Baraza hili Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mswada huu ni kielelezo chengine cha vipi Zanzibar inashindwa kujisimamia katika uwanja wa kimataifa hasa kwa mambo ambayo siyo ya Muungano. Mhe. Spika, kilimo si suala la Muungano lakini leo mswada huu umekuja kunithibitishia kwamba Zanzibar ikiingia katika uwanja wa kimataifa haiwezi kujisimamia hata katika masuala ya kilimo.

Ni mfumo mwengine kama ule wa suala la michezo kwamba si suala la Muungano lakini mpaka leo Zanzibar inashindwa kuwa mwanachama wa Shirikisho la Kimataifa la Mchezo wa Soka duniani (*FIFA)*.

Mhe. Spika, naomba niende kwenye madhumuni na sababu ili kufahamika hoja yangu. Madhumuni na sababu ya mswada Mhe. Spika, inasema na naomba nizinukuu baadhi ya sehemu.

Mwaka 1961 nchi kadhaa za Ulaya zilikutana mjini Paris na kukubaliana kuwa na mfumo wa aina ya kipekee wa kutoa na kulinda hakimiliki kwa ajili ya aina mpya za mbegu za mimea, mwaka huo nchi hizi zilipitisha mkataka wa kimataifa wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mimea. Mkataba huu ambao unasimamiwa na Shirika la Kimataifa la Hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea, uliboreshwa katika miaka ya 1972, 1978 na 1991 na nchi zilizoridhia zikawa zinaongezeka.

Sehemu inayofuata Mhe. Spika, ya madhumuni na sababu inasema kwamba:
Kutokana na manufaa yanayopatikana ya kuwa Mwanachama wa Shirika la *International Union for the Protection of New Varieties of Plants* (***UPOV)*** hususan kupitia Mapinduzi ya Kilimo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari mwaka 2010 liliridhia mkataba wa shirika hili. Ili Tanzania iwe mwanachama wa shirika la *UPOV* inatakiwa kuandaa sheria ambayo itakwenda sambamba na mkataba wa *UPOV,* kwa kuwa Tanzania Bara tayari wameshapitisha sheria ya Hakimikili za wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea. Zanzibar inalazimika kuwa na sheria kama hiyo kwa ajili ya kujiunga na Shirika la *UPOV*. Kwa upande wa Zanzibar Wizara ya Kilimo

na Maliasili imeandaa rasimu ya sheria kama hiyo ili iweze kujiunga na masuala ya *UPOV*.

Mhe. Spika, mbele zaidi katika madhumuni na sababu ya kutungwa kwa mswada inasema katika kifungu namba 3

> "Kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza masharti ya kujiunga na *UPOV* na kupata manufaa yanayotokana na uanachama huu"

Naomba niishie hapo kwa kunukuu kutokana na muda.

Sasa Mhe. Spika, hii inadhihirisha kwamba Baraza letu limetakiwa kutunga sheria hii mwaka 2014 leo, miaka minne baada inayoitwa Tanzania Bara kuridhia mkataba huu mwaka 2010 mwezi Februari, na madhumuni inasema kwamba sababu yake kuu ni kuiwezesha Jamhuri ya Muungano kuwa mwanachama.

Lakini suala langu Mhe. Spika, hivi inavyokwenda kuwa mwanachama wa Shirika la *UPOV* ni Jamhuri ya Muungano au ni Tanzania Bara kama kawaida yake kwa kutumia mgongo wa Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Spika, haya ndio yaliopo, hivi tukienda katika michezo unaambiwa kuwa Mwanachama wa *FIFA* ni Jamhuri ya Muungano, lakini inayofaidika ni Tanganyika, tukienda katika Shirika la Afya duniani *WHO* mwanachama tunaambiwa kuwa ni Jamhuri ya Muungano lakini anayefaidika ni Tanganyika, tukienda katika Shirika la Chakula duniani *FAO* mwanachana anaambiwa Jamhuri wa Muungano, lakini anayefaidika ni Tanganyika na mengi mengine Mhe. Spika.

Haya Mhe. Spika, tumekuwa tukiyahoji mara nyingi humu Barazani na kutoa na mifano kiasi gani misaada ya kisekta na misaada ambayo inakwenda moja kwa moja katika yale mambo yanayosimamiwa na Mashirika ya Kimataifa ambayo ati Jamhuri ya Muungamo inaambiwa kuwa ni Mwanachama, lakini manufaa yale kiasi kikubwa yanakwenda kwa Tanganyika kwa kutumia mgongo wa Jamhuri ya Muungano.

Sasa Mhe. Spika, natamani sana na naona fahari kwamba utajadiliwa mswada huu, lakini najiuliza kwamba, je, ilivyosema sababu kuwa haiwi kwamba ni kuwezesha tu hiyo inayoitwa Jamhuri ya Muungano iingie ambayo kimsingi kwa sababababu haiwakilishi suala la Kilimo, natarajia vile vile kwamba Waziri atakayekuwa na dhamana kutuwakilisha kule atakuwa ni Waziri wa Kilimo wa Tanganyika, lakini anaitwa wa Jamhuri ya Muungano kwa sababu suala la kilimo si suala la Muungano.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nasema hii ni kengele ya kuwaamsha tena Wazanzibari kwamba bila ya kuwa na udhibiti wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Zanzibar itaendelea kuwa haifaidiki kama ambavyo miaka yote imekuwa haifaidiki katika masuala yote ya Muungano ambapo Jamhuri ya Muungano inaambiwa kuwa ni mwanachama lakini faida zote zinaelemea upande wa Tanganyika.

Mhe. Spika, na hayo ninayoyasema yanadhihirika katika vifungu mbali mbali vya mswada huu. Mhe. Spika, ukiangalia kifungu cha 9 (2i) kinazungumzia;

"Kamati ya Ushauri wa Hakimiliki za Wagunduzi"

Sasa katika kifungu cha 9 (2i) kinamuorodhesha Mrajisi wa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea Tanzania Bara.

Mhe. Spika, haya mambo makubwa, hii sheria ni ya Zanzibar kuwa suala la kilimo si suala la Muungano kunaundwa chombo cha kumshauri Waziri mmoja katika Mjumbe wake ni Mrajisi wa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu na mimea ya Tanzania, lakini kuonesha nani ni mwenye mamlaka Mhe. Spika, Mrajisi mwenzake wa Zanzibar yeye anakuwa Katibu wa Kamati na sote tunajua ukiwa Katibu mabosi wako ni Wajumbe wa chombo kile ambacho wewe ni katibu.

Kwa hivyo, hiki chombo kilichoundwa kamati ya Ushauri wa Hakimiliki za Wagunduzi kwa vyovyote utakavyohisi ambayo wewe unamshauri Waziri wajumbe wake ni pamoja na Mrajisi wa Tanzania Bara lakini wa Zanzibar yeye ni Katibu. Naishia hapo Mhe. Spika.

Tukienda katika kifungu cha 23(1) na 23(2) kina kazi moja Mhe. Spika, kinasema kwamba.

> "Mgunduzi yeyote ambaye amefanya mambo kwa ajili ya Ulinzi wa aina ya mbegu ambaye ni mmoja wa wanachama wa Jumuiya ya Kimataifa inayohusiana na Mambo ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama atafaidika na haki ya kipaumbele kwa kipindi cha miezi kumi na mbili. Kipindi hiki kitaanza kuhesabiwa kuanzia tarehe iliyofanywa maombi ya mwanzo, siku ya maombi haitajumuishwa katika kipindi kijacho"

Lakini 23(2) inaendelea;

"Muombaji atalazimika ili afaidike na haki ya kipaumbele katika maombi ya baadae ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalazimika kudai ndani ya miezi kumi na mbili kipaumbele kwa maombi ya mwanzo"

Mhe. Spika, tutoke hapo twende kwenye kifungu cha 33 (1) Mhe. Spika, kinasema;

> "Hakimiliki za Wagunduzi hazitatolewa kwa matendo yanayohusiana na aina yoyote za mbegu zinazolindwa au aina yoyote za mbegu zilizokwishaainishwa katika sehemu ya kijifungu cha 31(5) ambazo zilizokwishauzwa au kinyume chake kufanyiwa biashara na Mgunduzi au kwa ridhaa yake katika eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, au bidhaa yoyote inayotokana na bidhaa inayotajwa isipokuwa matendo hayo yaliyotajwa katika kifungu hiki"

Kuhitimisha hoja yangu hii Mhe. Spika, naomba tukiangalie kifungu cha 56(1) kinasema;

> "Iwapo Mgunduzi si mkaazi au katika hali ya ushirika hana ofisi iliyosajiliwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalazimika kuwa na wakala ambaye ni mkaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"

Sasa Mhe. Spika, kama nilivyosema vifungu hivi kadhaa vinaonesha Mmiliki wa sheria hii nani.

Mhe. Spika, sasa nimetoa mifano hii ili kujenga ile hoja yangu niliyoianza mwanzo kwamba Zanzibar hata katika mambo yake ambayo si ya Muungano inakosa umiliki kwa sababu tu ya kukosa udhibiti wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Kwa sababu sheria hii chanzo chake imetokana na mkataba wa Umoja wa Mataifa au Kimataifa.

Sasa Mhe. Spika, naomba mimi nisaidiwe katika kifungu cha 78 (1) cha Katiba ya Zanzibar Mhe. Spika, kinasema nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

Lakini Mhe. Spika, kwa upande mwengine kifungu cha 64 (1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 kinasema:

> "Mamlaka yote ya kutunga sheria juu ya mambo mengine yote yanayohusu Tanzania Bara yatakuwa mikononi mwa Bunge"

Sasa Mhe. Spika, najiuliza hivi vifungu mbali mbali ambavyo vimo katika mswada huu ambavyo vinafanya rejea kwa Jamhuri ya Muungano na kuzifunga haki za Wagunduzi walioko Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano. Baraza la Wawakilishi kutunga sheria hii kwa mujibu wa kifungu cha 78(1). Je, tunayo mamlaka hayo.

Naomba nisaidiwe Mhe. Spika, kwa sababu mamlaka ya Baraza la Wawakilishi yaliyotajwa ndani ya Katiba ya Zanzibar kifungu cha 78(1) yanazungumza nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi.

Sasa najua suala la kilimo si suala la Muungano. Kwa hivyo, hapa Mamlaka tunayo, lakini inazungumzia katika Zanzibar, sasa unaziunganisha haki hizi ndani ya Jamhuri ya Muungano Baraza hili lina Mamlaka nilikuwa naomba hili Mhe. Spika, nisaidiwe.

Lakini Mhe. Spika, hapo hapo katika kuendelea kuwanasihi wananchi wa Zanzibar kupitia chombo hiki Mhe. Spika, niombe tena kwamba kama kuna kitu tujifunze tena katika mswada huu Wazanzibari ni kitu kinachoitwa kuridhia mikataba ya kimatafa. Kwa sababu Mhe. Spika, mfumo wetu wa Muungano uliokuwepo sasa una matatizo sana, una mambo ambayo si ya Muungano na una mambo ya Muungano, lakini hiki kifungu kwamba haya mambo yasiyokuwa ya Muungano yanapoingia katika uwanja wa kimataifa aliyekuwa na mamlaka ni nani.

Vifungu vya Katiba vinaonesha wazi kwa Zanzibar yenye mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano ni Baraza la Wawakilishi na Bunge limepewa mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo ambayo si ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara. Lakini inapokuja mikataba ya kimataifa hata ile inayohusu mambo yasiyo ya Muungano chombo hiki cha kutunga sheria cha Zanzibar hakijapewa nafasi yoyote ya kupokea na kuridhia mikataba ile kwa niaba ya Zanzibar.

Imekuwa Bunge la Muungano linaridhia mikataba ile kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano. Vile vile, kwa pande zote. Na Mhe. Spika, niseme kwamba suala hili niliwahi kulizungumza ndani ya Bunge katika kipindi kifupi pale nilipotumikia mwaka 2010 na nilikielekeza wakati ule tulikuwa tukizungumzia masuala ya Afrika Mashariki tena ndugu yangu Mhe. Mohammed Aboud alikuwa Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, nikauliza nini nafasi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar kuridhia mikataba hii ya kimataifa ambayo inahusu mambo yasiyo ya Muungano ikishachapishwa hapa kwenye Bunge la Muungano? Nani na nani anaifunga Zanzibar? Nani mwenye ridhaa kwa niaba ya Wazanzibari katika kuwafunga katika mambo ambayo yasiyokuwa ya Muungano?

Nadhani hayo ndio mambo ambayo tunapaswa kuyatizama sana katika kipindi hiki ambacho tunapitia hatua za kuandaa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano ambayo mategemeo yangu Wazanzibari tutaamka na tutaona haja

ya kulinda haki zetu na kuonesha katika mamlaka yetu katika yale mambo yanayopaswa kuwa yetu.

Mhe. Spika, hili lilikuwa ni suala moja kubwa sana ambalo nilitaka nilizungumzie na kuwanasihi Wazanzibari kuona mapungufu ambayo tunayo katika mfumo wa Muungano hata kwa mswada huu ambao uko mbele yetu.

Mhe. Spika, nikiacha hili na nikitegemea kwamba nitapewa majibu ya kuridhisha katika suala hili hili. Naomba sasa nichangie baadhi ya vifungu lakini zaidi itakuwa katika njia ya masuali.

Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nizungumzie kifungu cha pili cha mswada kinachohusu ufafanuzi. Kuna neno limetumika mimi nimefahamu maana yake kwa sababu limeekewa tafsiri vile vile, lakini neno hili kidogo katika kipindi kifupi nilichokaa Baraza la Wawakilishi, naona kama tumeleta neno jipya neno Rajisi.

Sasa Mhe. Spika, niliwahi kuzungumza mara moja kwamba hatuna utaratibu unaoeleweka wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa na mfumo wa kuzitafsiri sheria kila siku tutabuni maneno mapya kwa sababu kila atakayetaka kutafsiri mswada hana kiongozi cha kumuongoza cha kuweka maneno anabuni neno lake mwenyewe.

Mhe. Spika, mimi nimefahamu kwamba Rajisi kakusudia *Register*, lakini imeshaletwa miswada hapa neno hilo hilo limetafsiriwa kwa Kiswahili limeandikwa Regesta, umeshaletwa mswada hapa neno hilo hilo *Register* limetafsiriwa kuwa ni daftari ambalo mimi nafikiri ndio neno sahihi zaidi la Kiswahili na mifano iko Mhe. Spika. Hata daftari la kudumu la wapiga kura kwa Kiingereza linaitwa *Permanent Voter's Register* .

Mara nyingi inapoletwa miswada inaitwa madaftari, sasa hii nilikuwa nasema najua sheria itatungwa ya Kiingereza, lakini malengo ya watunga sheria yatizamwe katika lugha ya Kiswahili, hili ni suala tunalolijadili hapa. Sasa hili neno Mrajisi linatukumbusha kwamba kuna haja ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuwa na kiongozi wa tafsiri wa maneno isiwe kila mmoja anayepewa kutafsiri mswada anakuja na maneno yake.

Lakini la pili, Mhe. Spika, ni kifungu cha 4(3) kimezungumzia sifa za mtu ambaye anapaswa kuteuliwa Mrajisi au Naibu Mrajisi; na hapa imesemwa kwa madhumuni ya kifungu hiki vigezo vinavyotakiwa vitajumuisha angalau shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu kutoka katika taasisi yoyote inayotambulika katika fani ya Sayansi ya Kilimo, Sheria au fani inayofafana pamoja na uzoefu wa kazi usiopungua miaka 5 katika fani husika.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka kusaidiwa tu kwamba je, watunzi wetu wa mswada huu wameridhika kwamba Shahada ya Kwanza ya Sheria na uzoefu wa miaka mitano kwa Zanzibar na hali tunavyoiona ya wahitimu wetu inatosheleza kumpa mtu dhamana ya kuwa Mrajisi katika suala hili. Maana yake angalau Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, hapa kauliza suali lina fani gani ya sheria katika Shahada ya kwanza hakuwezi kuwa na *Specialization* unaweza kuanza kiwango cha pili na kwenda juu. Sasa ingelikuwa Shahada ya pili angalau tungesema labda ambaye ana Shahada ya Sheria ambayo inejikita katika suala la Hakimiliki angalau tungesema kwamba inaingia akilini, lakini sasa si rahisi kupata Shahada ya kwanza ya Sheria ambayo imejikita hapo. Kwa hivyo, nilikuwa nasema hili kidogo naomba nisaidiwe.

La pili ,Mhe. Spika, na mimi niulize kama walivyouliza Kamati, kwenye kifungu cha 9. Kifungu hiki kinazungumzia Kamati za Ushauri wa Hakimiliki za Wagunduzi. Mhe. Spika, kifungu 9(2) kinawataja hawa Wajumbe wake, lakini 9(2) (b na c) kinataja Wawakilishi kutoka Jumuiya ambazo hivi sasa hazipo.

Sasa nilikuwa nauliza kwamba je, ikiwa hazikuundwa kwa sababu Jumuiya hizi za hiari hawa Wawakilishi hawa watapatikana vipi, hawa wengine naelewa lakini pia naomba maelezo kama nilizungumza mwanzo juu ya 9(2i) kwamba kwa nini aingie Mrajisi wa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu na mimea Tanzania Bara katika chombo ambacho ni cha Zanzibar.

Mhe. Spika, halafu naomba ,vile vile, nisaidiwe maelezo kuhusiana na kifungu cha 23. 23(1) kinazungumzia mgunduzi yeyote ambaye amefanya maombi kwa ajili ya ulinzi wa aina za mbegu ambaye ni mmoja ya wanachama wa Jumuiya ya kimataifa inayohusiana na mambo ya Hakimiliki za wagunduzi wa mbegu mpya za mimea.

Kwa hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama atafaidika na haki ya kipaumbele kwa kipindi cha miezi 12. Sasa kule mbele kunakofaidika ile haki kubakia kwa miaka 20 lakini hapa imetajwa miezi 12, hii miezi 12 Mhe. Spika, hebu tungewekwa wazi ni ya kipindi kutoka Ugunduzi mpaka kuandikisha ama vipi halijakaa sawa kwa kifupi.

Lakini kama nilivyouliza pale mwanzo vile vile kwamba sheria hii inapofanya rejea kwa Jamhuri ya Muungano inatupa matatizo sisi tunaotunga sheria kwa Zanzibar kwa sababu kifungu cha 23(2) kinasema;

> "Muombaji atalazimika ili afaidike na haki ya kipaumbele katika maombi ya baadaye ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atalazimika kudai ndani ya miezi 12 kipaumbele kwa maombi ya mwanzo"

Sasa suala langu lilikuwa haya maombi yanahusu Jamhuri ya Muungano ama yanahusu Zanzibar, kwa sababu sheria hii inaanzisha mfuko ambao utahusiana na masuala haya kwa Zanzibar. Sasa hizi hati na maombi yake yanahusika Zanzibar kwa sheria ya Zanzibar au yanahusu kwa Jamhuri ya Muungano? Na kama yanahusu Jamhuri ya Muungano kama nilivyouliza ni yepi mamlaka yetu Baraza la Wawakilishi kuitungia sheria Jamhuri ya Muunguno kwa ujumla wake.

Mhe. Spika, jengine dogo la uandishi tu kifungu cha 30. Kifungu cha 30 nimeangalia yote tafsiri ya Kiswahili na ya Kiingereza. Pale mwisho kabisa imefanya rejea na naomba kuinukuu;

"Kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 30"

Sasa kifungu cha 30 ni ndio hiki kifungu chenyewe, na ninavyofahamu mimi mara nyingi lugha za uandishi wa sheria ilikuwa inasema kama ilivyoelezwa ndani ya kifungu hiki, kwa sababu hapa kinazungumza kifungu cha 30 ambacho ndicho chenyewe hapa kuliko kutaja kifungu cha 30 ambacho ndicho hicho chenyewe si taratibu nzuri za uandishi wa sheria.

Halafu Mhe. Spika, naomba maelezo vile vile katika kifungu cha 31 hasa cha 31(3). Mhe. Spika, hapo naomba ninukuu sehemu ya kuanzia tu ili nijenge hoja yangu inasema hivi;

> " Chini ya vifungu vya 31 na 32 mambo yaliyoainishwa katika sehemu ya 'a' mpaka 'g' ya kijifungu cha kwanza yanayotokana na vuno ikijumuisha mimea kwa ujumla na sehemu za mimea"

Hapa panazungumzwa kwamba pana haki ambazo atapewa huyu mgunduzi, lakini rejea kijifungu hiki cha 31 (3) imefanywa na kijifungu cha 31(1). Sasa 31(1) Mhe. Spika, kimetaja mambo 7 haya ambayo ndio kwenye hakimiliki kapewa haki.

(a) Kuzalisha au kuongeza uzalishaji,
(b) Masharti kwa malengo ya usambazaji,
(c) Kutoa kwa mauzo,
(d) Kuuza au kufanya biashara,
(e) Kusafirisha,
(f) Kuingiza, na
(g) Kuhifadhi na madhumuni yoyote yaliyotajwa katika sehemu ya (a).

Sasa hapa hapakutajwa mavuno, lakini huku kwenye kifungu cha 3 kumefanywa rejea kwenye yaliyotokana na vuno. Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba hizi hati zinasimama vipi unapofanya rejea kijifungu hiki kwa

kifungu hiki. Mswada huu ni wa kitaalamu sana Mhe. Spika. Kwa hivyo, nahitaji kueleweshwa vizuri ili turidhike na hayo ambayo yamekusudiwa.

Mhe. Spika, kijifungu chengine ambacho naomba maelezo ni kifungu cha 32 (1b) na (c). Mhe. Spika, kifungu hichi kinasema Hakimiliki za Wagunduzi hazitatolewa kwa:

(b) Kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya kiutafiti na (c) Kwa kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya ugunduzi wa aina nyengine za mbegu na isipokuwa pale ambapo maelezo ya kifungu cha 31(5-7) kitatumika, kazi zilizoainishwa katika kifungu cha 31(1) mpaka (4) kulingana na aina nyengine za mimea. Sasa hii nilikuwa naomba kuuliza kwa nini kazi zilizofanywa kwa madhumuni ya kiutafiti ikiwa mtu kagundua mbegu asiweze kupata hakimiliki nilikuwa naomba kusaidiwa hilo.

Kwenye hichi cha (c) nilikuwa naomba maelezo vile vile kwamba kwa nini ikiwa madhumuni ya ugunduzi yaliyotajwa katika vifungu vilivyotajwa kwa nini kama kaweza kugundua hapo asiweze kupata hakimiliki. Nilikuwa naomba hilo Mhe. Spika, anisaidie.

Kifungu cha 31(1) nilikuwa nimeshakitaja pale mapema naomba maelezo kwa sababu inazungumzia Jamhuri ya Muungano wakati sheria hii inahusu Zanzibar. Mhe. Spika, naomba vile vile katika kifungu 40 (1) kinasema;

> "Mmiliki yeyote wa Hakimiliki za Wagunduzi anaweza kwa notisi ya maandishi kwa mrajisi kusalimisha haki za wagunduzi"

Huyu ni mmiliki anaambiwa kuwa anaweza kwa *notice* ya maandishi kusalimisha haki za wagunduzi. Haki za wagunduzi wepi ambazo atakuwa anazo yeye huyu mmiliki wa haki yake nilikuwa naomba pia kupewa ufafanuzi hapa.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni kifungu cha 44(1) kwenye Bodi ya Rufaa. Kimesema Waziri atateua Bodi ya Rufaa itakayojumuisha Wajumbe watano ambao Wajumbe wawili watakuwa ni wataalamu wa masuala ya kisheria na Wajumbe watatu wengine watakuwa ni Wataalamu waliohitimu katika Sayansi za Kilimo.

Mhe. Spika, kwenye kilimo au Sayansi za Kilimo pametajwa wataalamu waliohitimu, lakini hatukuambiwa wa kiwango gani na vile vile kwenye wataalamu wa masuala ya kisheria ambao katika Kiingereza wameandikwa *expert legal sector*. Sasa huyu *expert* kwa mujibu wa tafsiri ya sheria hii ni yupi? Maana yake anaweza kuwa pengine mtu ana diploma tu, au *certificate*

katika mambo ya sheria. Je, huyu anatosheleza kuitwa mtaalamu na kuweza kuingizwa katika Bodi ya Rufaa.

Nimesema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu yapo haya ya kuchaguliwa watu ambao kitaratibu za fani bado hajatambulikana lakini kwa sababu tu ana pengine kiwango cha chini cha fani ile wanaingizwa katika vyombo kama hivi.

Mhe. Spika, mawili ya mwisho haraka haraka, kwanza ni kifungu cha 47 hapa panazungumzwa Mfuko wa Maendeleo ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mimea. Sasa 47 (1) inasema;

> "Waziri wa Fedha atalazimika baada ya kupokea maombi kutoka kwa Waziri kuanzisha mfuko utakaojulikana kwa jina la Mfuko wa Maendeleo ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mimea ambao fedha zake zitapatikana chini ya sheria hii zitahifadhiwa katika akaunti maalum"

Nilikuwa naomba kusaidiwa kama kuna taratibu nyengine za Serikali zinazozuia Waziri mwenye dhamana ya sekta hii kuanzisha mfuko huu. Kwa hiyo, nauliza kwanini atakiwe Waziri wa Fedha kuanzisha mfuko huu au kuna sheria nyengine ambazo labda sisi hatuna uelewa nazo ambazo zinalazimisha kwamba Waziri wa Fedha tu ndio mwenye mamlaka ya kuanzisha mfuko wa aina hii.

La mwisho, Mhe. Spika, kama nilivyosema katika mawili ya mwisho ni kifungu cha 55. Mhe. Spika, kinasema;

> "Waziri anaweza kuingia katika makubaliano na nchi mbili au zaidi na Mashirika ya Kimataifa au Mashirika yasiyo ya kiserikali ili kurahisisha ushirikiano katika majaribio"

Sasa swali langu Mhe. Spika, linarudi pale pale nilipoanzia. Kwenye Mashirika ya Serikali sina matatizo sana, lakini katika kuingia makubaliano na nchi mbili au zaidi na Mashirika ya Kimataifa. Je, katika taratibu za sasa Mhe. Spika, tunaweza kufanya hilo bila kibali cha Jamhuri ya Muungano.

Kama hatuwezi kutunga sheria hii katika kifungu hiki hakitakuwa ni kujifurahisha tu kama ambavyo tulijifurahisha katika maeneo mengine? Lakini baadae tukazuiwa kwa hoja kwamba Waziri wa Zanzibar hana *instrument.* Mhe. Spika, Mawaziri mbali mbali wamewahi kutupa mifano hapa ambapo wamekaa mpaka juu ya meza kutaka kutia saini mikataba, wakaambiwa mikataba hiyo rasimu zake hazipo kwa sababu wao hawana *instrument* za kusaini mikataba ya kimataifa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nasema nasita kusema kwamba nauunga mkono mswada huu mpaka nitakapokinaishwa kwa zile hoja ambazo nimezitoa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu, na mimi kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar hususan wale wa Jimbo la Magomeni nitoe mchango wangu katika mswada huu muhimu sana unaohusiana na suala zima la Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu na Mimea. Unajua Mhe. Spika, maana ya kusema muhimu sana ni kwamba zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar ajira yao ni kilimo.Kwa hivyo, mswada huu umegusa jamii kubwa sana ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili, Mhe. Haji Omar Kheir, kwa uwasilishaji wake wa mswada huu amewasilisha vizuri na kwa kweli sote tumemuelewa. Lakini pia nimpongeze kwa niaba ya Mwenyekiti Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kwa kuwasilisha Maoni ya Kamati vyema na ni matumaini yangu kwamba yameeleweka.

Mhe. Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wa Zanzibar wote kwa ujumla kwa kuweza kushiriki kikamilifu katika sherehe muhimu sana za nchi hii za kutimiza miaka 50, nusu karne ya Mapinguzi yetu Matukufu ya Zanzibar. Mapinduzi ambayo yamewatoa wananchi wa Zanzibar katika unyonge wa kutawaliwa kwa muda mrefu.

Pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kusimamia kikamilifu sherehe hii zikawa nzuri zenye sifa na kila mmoja akaweza kuzipongeza nje na ndani. Dkt. Shein kweli ni mwanamapinduzi. Sherehe hizi kwa kweli Mhe. Spika, zilikuwa nzuri na za aina yake, na bila ya ushujaa wake basi sherehe zile zisingeweza kufikia kiwango kama kile. Kwa hivyo, tunampongeza sana Dkt. Shein.

Mhe. Spika, tunampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, kwa sababu ofisi yake ndio iliyoratibu masuala yote. Kwa hivyo, tunampongeza sana Balozi kuweza kuzipanga sherehe zile na zikawa za mfano.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati iliyosimamia mswada huu, kupitia Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ambayo Kamati yangu imeupitia. Na mimi Mhe. Spika, mara zote ninapopata mswada huwa naangalia madhumuni ya kuwasilishwa mswada huu. Haidhuru madhumuni yanakuwa ya mwisho lakini mimi huwa ninafukuzia kwanza kule

mwisho, hivi madhumuni ya kuwasilishwa mswada huu ni nini? Ninapofika pahala nikaelewa basi ninakuwa sina tabu.

Na kwa sababu tunatunga sheria hapa katika chombo hiki kwa sababu mbali mbali, ama sheria iliyopo imeshapitwa na wakati, kwa hivyo ina mapungufu inahitaji kufanyiwa marekebisho, ama tunatunga sheria mpya ili iendane na wakati ulivyo hivi sasa.

Mhe. Spika, nilipopitia madhumuni na sababu ya kutungwa sheria hii mimi mwenyewe nimetosheka na wenzetu wameeleza wazi, wameeleza chimbuko lakini wakaeleza pia na sababu. Chimbuko la sheria hii ni kutokana na mikataba ya kimataifa, ambapo nchi zipatazo 71 zimeingia katika mkataba wa pamoja ambao wameanzisha sheria au taasisi *UPOV* ambayo inasimamia Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina za Mbegu. Kwa hivyo, kwa kuwa yameonekana kuna manufaa ambayo yametajwa, na sisi Tanzania hatukuwa na haja ya kuacha kujiunga katika kitu kama hiki muhimu.

Kwa hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipofika mwezi Februari, 2010 kwanza iliridhia huu mkataba wa kujiunga katika taasisi hii na huo ndio utaratibu. Na baadae Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likapitisha sheria. Na kama maelezo yalivyoelezwa humu, sheria zinazotawala katika nchi hizo zinatakiwa ziwe hazitofautiani sana kwa sababu shabaha na malengo yao ni mamoja.

Kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio maana tumelazimika tuanzishe sheria hii ili tuendane sambamba na dunia. Na kama tunavyofahamu kwamba shughuli za kilimo si jambo la Muungano, ndio maana na sisi tumeanzisha sheria inayoambatana na haya.

Mhe. Spika, tukubali kwamba kuna mambo ya Muungano na kuna mambo yasiyo ya Muungano. Masuala ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa haya tumekubaliana kwamba ni mambo ya Muungano, na Serikali ya Jamhuri ya Muungano lazima ichukue nafasi katika mambo yale. Suala la kuingia katika mikataba ya kimataifa ni suala la Muungano. Sasa Mhe. Spika, mimi nashangaa sana kutokezea Mjumbe anatofautiana na wazo hili.

Kwa hivyo, sisi tuna wajibu kama Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano kushirikiana na Jamhuri ya Muungano katika kufanikisha hili. Mimi sioni kama kuna kosa hata kidogo, kama kosa labda kuridhia huu Muungano, lakini kama hatutaki Muungano basi tuseme tu kwamba sasa hatutaki Muungano. Lakini kama kuna mambo tumekubaliana kwamba haya ni mambo ya Muungano kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa Sheria.Kwa hivyo, Sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano lazima ichukue nafasi.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba kilimo si suala la Muungano, lakini hivi tujiulize Zanzibar hatufaidiki na miradi ya kilimo ambayo inasimamiwa na Jamhuri ya Muungano? Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia Kilimo, kuna miradi kadhaa wa kadhaa ambayo Zanzibar tunapata fedha nyingi ambazo zinakuja moja kwa moja Zanzibar na zinalipwa fedha hizo na Jamhuri ya Muungano, sisi hatutoi hata shilingi moja, lakini tunapata sehemu ya fedha zile za miradi ya kilimo na uvuvi.

Mradi kama wa *ASP* na *ASPL* ni miradi ya kilimo ambayo inasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tumepata *billions* kwa *billions* hapa za pesa kwa ajili ya kuendeleza kilimo hapa. Mradi kama wa *PADEP billions* kwa *billions* zimeingia Zanzibar na ni miradi inayosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini wanaofaidika hapa ni wakulima wetu. Ni miradi ambayo imepata mafanikio makubwa. Pia, mradi wa *MIVAS* ni mradi unaosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, lakini tunaofaidika ni Wazanzibari (wakulima na wavuvi wetu).

Mradi kama wa *MACEMP* ni mradi uliokuwa na *billions of billions* ya fedha ambazo fedha zile zinalipwa na Jamhuri ya Muungano lakini umetunufaisha hapa, na mengine kadhaa wa kadhaa.Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nadhani katika eneo hili tusijaribu kulipotosha au tukalibabaisha. Na sisi Zanzibar tunayo nafasi ya kuitumia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jambo hili zuri.

Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba jambo hili lina manufaa. Na kwa sababu watafiti wetu wamekuwa wakigundua mbegu, wakivumbua mambo, wakigundua mimea, lakini walikuwa hawafaidiki na chochote. Na ugunduzi wao wanaoupeleka katika Taasisi ya Kilimo, na Taasisi ya Kilimo kushirikiana na taasisi nyengine, badala ya ugunduzi ule kuonekana umetokea Zanzibar unatumika katika mataifa mengine. Lakini kuanzisha Sheria hii ya Hatimiliki itawasaidia wagunduzi wetu wa Zanzibar kuweza kusajiliwa na kujulikana na kupata manufaa kama yaliyotajwa katika mswada huu.

Kwa hivyo, sheria hii itakuwa mkombozi. Mimi niwapongeze sana Wizara ya Kilimo. Lakini zimetajwa hapa sababu kama tano, Waheshimiwa Wajumbe kama mtaangalia nisingependa kutumia muda mkubwa kuzisema. Lakini kuna sababu sababu hizi ni muhimu kwa sababu kwanza zitaongeza ari ya wagunduzi wetu kuona kwamba ile shughuli wanayoifanya basi inawapatia manufaa.

Lakini kuna baadhi ya vifungu ambavyo vimetaja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, humu ime-*appear* Tanzania Bara sijui kwa misingi gani sielewi, lakini ni sheria ambayo imepitishwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio inayosimamia jambo hili kuwashirikisha wenzetu katika baadhi ya maeneo sio kosa kabisa, kwa sababu wao ndio wanaosimamia suala hili katika Jumuiya ya Kimataifa. Wenzetu *UPOV* wameshirikiana na Zanzibar wakati wa kutunga sheria hii, wajumbe mbali mbali walikuja wakiangalia sheria ili iendane na matakwa ya taasisi hii.

Wamekuja na tayari Wazanzibari wameshapata nafasi ya kwenda katika taasisi mbali mbali, huku sisi tukiandaa hii sheria tayari Wazanzibari tumeshaanza kufaidika. Wameweza kushiriki katika maonesho mbali mbali yanayohusu jambo hili, ni Wazanzibari chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ninachosema kwamba sheria hii haina matatizo itawasaidia Wazanzibari, Waheshimiwa Wajumbe tuijadili, tuipitishe kwa sababu hii ni sheria ya ukombozi wa Wazanzibari hasa watafiti wetu. Na kwa sababu haina tatizo huwezi kukubali mkono mmoja halafu mkono wa pili ukakataa. Kama unakubali ukubali mikono yote. Mradi kama *COICA* unaoshughulikia masuala ya umwagiliaji maji ni mradi mkubwa tu na sisi Zanzibar tuna *billions of billions* ya pesa tumepata, sasa sisi tupate nini!

Mhe. Spika, Wazanzibari napenda tusiwe na tabia kama ya kuku, kuku ukimmwagia mtama basi atakula kisha anachakura chakura anaona hapa juu pako hivi huko chini je, kumbe chini hakuna kitu vumbi tupu mtama wote uko hapa juu. Kwa hivyo, tusione sisi tunapata hivi, lakini kumbe tukienda chini tutapata zaidi kumbe inakuwa tofauti.

Mhe. Spika, mimi kubwa kwangu kwa Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha inasimamia masuala ya kilimo kikamilifu. Bajeti inayotengwa kwa kilimo na utafiti wa kilimo haitoshelezi hata kidogo. Mwaka 2012/2013 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani ilipangiwa fedha za maendeleo milioni 400, mpaka mwaka ule unamalizika taasisi ile imepatiwa milioni 40 sawa na asilimia 10. Huwezi kufanikiwa katika kilimo bila ya kuwa na utafiti. Lakini la kusikitisha zaidi Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014 Taasisi ya Kilimo imepangiwa shilingi milioni 146 kwa mwaka huu, zimetoka zile 400 zimeshuka mpaka 146, lakini mpaka juzi Kamati yangu inakwenda Wizara ya Kilimo ambapo ni nusu mwaka mwezi wa Disemba, Taasisi ya Kilimo haijapatiwa hata senti moja na tupo nusu ya mwaka wa utekelezaji wa bajeti.

Hebu tuangalie jinsi gani tunaweza tukaimarisha kilimo hapa Zanzibar. Taasisi kama hizi muhimu ambazo ndizo zinazotakiwa ziimarishwe, ziwezeshwe kikamilifu ili ziweze kufanya shughuli zake kwa manufaa ya wakulima ambayo ndio idadi kubwa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Wizara yenyewe ya Kilimo kwa ujumla mpaka kufikia mwezi wa Disemba bajeti yake ya *other charges just* iko asilimia 26 ambazo ndio fedha za kufanyia kazi. Fedha hizo ambazo zinahitajika kwa ajili ya kununulia mbolea, kuwapa pembejeo za kilimo, kuwasaidia wakulima kulima kwa matrekta, na kununua mbegu. Lakini wana asilimia 10 ya fedha za maendeleo. Katika fedha zao za maendeleo walizopangiwa Wizara ya Kilimo wamepatiwa *just* asilimia 10 tu na sasa tupo nusu mwaka.

Hapa niiombe sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama kweli tunasema kwamba kilimo ni uti wa mgongo, kilimo kwanza, mapinduzi ya kilimo, tumeita majina mengi kutokana na umuhimu wa kilimo. Takwimu hizi haziridhishi hata kidogo kwa eneo ambalo limepewa kipaumbele. Kamati yangu haikuridhishwa kabisa na takwimu tulizozikuta katika Wizara ya Kilimo na hatuelewi ni kwa sababu gani.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nilitaka kusema hayo kuzungumza na Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi juu ya umuhimu wa mswada huu.

Mhe. Spika, mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe waziangalie sababu za kuanzishwa kwa sheria hii ili waweze kuona umuhimu wa sheria hii kwetu hapa Zanzibar. Hatuwezi kabisa kubakia nyuma, jambo lolote ambalo lina manufaa kwa wananchi wetu wa Zanzibar naamini Serikali italisimamia na kuhakikisha linatekelezwa. Hatuwezi kuitumia taasisi hii ya kimataifa katika kuwaenzi wagunduzi wetu bila ya kujiunga, na bila kuanzisha sheria hii.

Nataka kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe tayari mbali ya kwamba Zanzibar hatujaanzisha sheria lakini tumeshafaidika sana. Kwa hivyo, naamini Mhe. Spika, kama tutaupitisha mswada huu uliokuwa hauna matatizo basi tutafaidika zaidi na zaidi.

Mhe. Spika, niwaombe Wajumbe wenzangu tuunge mkono mswada huu sisi kama Kamati tumeupitia vizuri na tumetoa baadhi. Na huu mmeona umechapishwa upya Waheshimiwa Wajumbe, ule mswada wa mwanzo ni tofauti na huu kama mumeuangalia. Na sio kama ulichapishwa upya tu, baada ya kuupitia Kamati tukatoa baadhi ya mapungufu na ndio maana tunauona huu. Huu ulikuwa na mapungufu mengi tukawataka Wizara ya Kilimo wauchapishe upya.

Mimi Kamati yangu haikubali tu kuleta hapa kwenye Baraza mambo yaliyokuwa nusu nusu. Hata mswada wa karafuu tutakaoujadili kesho, utakuja mwengine mpya hapa, baada ya kupitia ule wa mwanzo tukaona una kasoro

nyingi tukamuomba Mhe. Waziri, auchapishe upya, ili mambo yetu yaende vizuri. Kwa hivyo, mswada huu hauna matatizo.

Jana nilikuwa nikizungumza na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, tulipokuwa tukipitia Mswada wa Karafuu katika Kamati yangu, nilikuwa na lugha namwambia Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na Wajumbe kwamba haya makosa mengine hebu tusiyamalize, kwa sababu tukiyamaliza yote wenzetu watakuwa hawana la kusema, hebu tuwaachie na wenzetu na wao wakasome ili tupate *inputs* zao.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono mswada huu na nawaomba Waheshimiwa wenzangu waukubali mswada huu ili baadae uwe sheria kwa manufaa ya wakulima, wagunduzi na watafiti wetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu ambao ni mswada muhimu sana kwani kilimo ndio uti wa mgongo, kwa kweli kama huna mimea huwezi ukafanya chochote katika kilimo. Pia, nichukue nafasi hii kabla sijachangia niunge mkono mswada mia kwa mia.

Mhe. Spika, lazima tukubali na sisi twende na wakati kwa sababu nchi yetu tunaijua ni nchi ndogo, lakini tunamshukuru Mwenyezi Mungu amejaalia katika Wizara hii ya Kilimo tuna wasomi tena wazuri sana, na ni wasomi ambao kwa kweli wanaweza kusaidia sana katika mambo haya ambayo tunayazungumza leo katika mswada huu.

Mhe. Spika, tukitaka tusitake kuna baadhi ya mambo lazima tukubaliane na ulimwengu ulivyo. Kuna yale ambayo hayatugusi vyema, lakini kuna yale ambayo yanatugusa vyema kwa mintarafu ya nchi yetu. Haya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa sote tunaelewa Mhe. Spika, kwamba haya ni mambo ya muungano.

Mwenzangu aliyekaa kitako ameyaeleza vizuri sana. Sasa haina maana kwamba kitu chochote kile cha muungano tupinge. Mambo mengine Mhe. Spika, ni ya muhimu katika nchi, sio ya Asha Bakari wala sio ya Fatma wala sio ya Kombo, ni muhimu katika nchi pamoja na wananchi wake.

Mhe. Spika, tusiwanyime wale ambao katika wizara hii wana haki na hata mwananchi ambaye ni *layman*, lakini anaweza akafanya ugunduzi. Mimi nitatoa mfano Mhe. Spika, samahani ingawa haihusiani na mambo haya.

Katika wizara yangu ya Habari tulikwenda Makunduchi, kuna vijana wawili ambao ni watoto wadogo sana lakini waligundua mambo ambayo huwezi ukafikiria kuhusu redio jamii na hilo darasa lao ukiambiwa Mhe. Spika, unashangaa.

Wamezindua redio jamii hiyo, tena kwa vitu vidogo tu, mpaka televisheni sasa hivi wakiunganisha unapata. Sasa ni mambo ambayo kwa kweli ni ya msingi katika nchi yetu. Sasa mimi ninasema hapa hakimiliki hii itawasaidia wale wenzetu ambao wanajua namna gani ya kufanya ugunduzi wa mimea ili kusaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, kilimo lazima kinahitaji mabadiliko tukitaka tusitake. Tuangalie miongo yetu hivi sasa inavyobadilika. Unasema mwaka huu mvua itakuwa hivi lakini matokeo yake mvua haiji, ni tofauti na wazee wetu wa zamani ambao walikuwa wanatumia miongo ya hali ya hewa. Tabia ya nchi imebadilika kabisa Mhe. Spika. Kwa hivyo, tukiangalia katika kilimo lazima tusonge mbele na kuhakikisha kwamba na sisi wenyewe tunabadilika.

Mhe. Spika, hili nimesema nilizungumze kwa makusudi tusiwanyime haki wale wenzetu wanye uwezo. Na mimi nisisitize kwamba mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa kuna mambo mengi sana Mhe. Spika, tunafaidika.

Sasa mimi niwaombe Waheshimiwa wenzangu kwamba mambo kama haya tuyathamini na tuyapokee ili kuweza kuwasaidia wananchi wetu. Mhe. Spika, kama tunavyosema kwamba kilimo ni uti wa mgongo, niiombe Wizara husika kusismamia kikamilifu sheria hii itrakapokamilika, kwani kwa kutunga sheria sisi ni mahodari lakini namna ya utekelezaji wa sheria na namna ya kuwasaidia wale tunaowatungia sheria hapo kidogo kuna walakin.

Ni imani yangu kwa sheria hii na sheria nyengine ambazo amezisema mwenyekiti wa kamati hii kwamba zikiunganishwa pamoja na zikafanyiwa utafiti na zikafanyiwa kazi ya uhakika, basi kwa kweli wananchi wanaweza kufaidika na kilimo.

Jengine Mhe. Spika, niombe wizara husika kwamba hii ni sheria na ni sheria mpya kwa kweli, watoe taaluma ya kutosha katika vyombo vyetu vya habari ili wananchi waweze kuielewa vizuri, na si lazima watoe mswada wote lakini watafute vipengele ambavyo wananchi wetu wanaweza kuvifahamu kwa ukaribu zaidi.

Mwisho niiombe wizara yale ambayo nimeyazungumza wayafanyie kazi na ni imani yangu kwa sababu wizara hii ina wasomi tena waliobebea, kila mtu na fani yake. Kwa hivyo, baada ya kusema hayo Mhe.Spika, niseme tena

ninaunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia, na ninawaomba Waheshimiwa wenzangu waunge mkono ili tuweze kuufanyia kazi mswada huu kama ulivyotoa maelekezo katika mswada.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo hii kukutana tukiwa wazima.

Pili, ninakushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mdogo katika mswada huu. Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa mdogo sana kwani mwenyekiti ametwambia wamerekebisha kila kitu na wametuachia sehemu ndogo ndogo tu ili tupate kuchangia.

Sasa Mhe. Spika, naomba nianze na mchango wangu katika madhumuni na sababu ya serikali kuuleta mswada huu. Mhe. Spika, kwanza imeelezwa ni hatua za kutambua umuhimu wa kuwaenzi na kuwazawadia watafiti na wagunduzi wetu wa Zanzibar wanaogundua aina mpya za mbegu.

Mhe. Spika, sababu hii ni nzuri sana na hawa waliotayarisha huu mswada wanahitaji wapewe pongezi. Lakini Mhe. Spika, la kujiuliza wagunduzi hawa wapo? Kwa sababu Mhe. Spika, ili uwe na wagunduzi lazima kuwepo na vituo imara vya utafiti vilivyosheheni majengo ya kisasa, nyenzo, vifaa na wataalamu.

Mhe. Spika, hivi sasa Zanzibar tuna vituo viwili vya Utafiti wa kilimo. Cha kwanza ni kituo cha Kizimbani kwa Unguja na cha pili ni kituo cha Matangatuani kwa Pemba. Mhe. Spika, hali ya vituo hivi sio nzuri, majengo ni duni, vifaa havina, na wataalamu ni haba. Na hasa kile cha Matangatuani Mhe. Spika, hamna kitu kabisa. Sasa ninajiuliza wagunduzi hawa wa mbegu wapo katika vituo vipi, ingawa jana Mhe. Spika, tumeelezwa katika semina kwamba katika kituo cha Kizimbani kuna watafiti ambao wamegundua mbegu tatu za muhogo.

Kwanza mimi ninawapongeza sana watafiti hawa. Kwa mazingira ya vituo hivyo na wakaweza kugundua mbegu tatu, wanahitaji wapongezwe. Lakini ninamuomba Mhe. Waziri, anifahamishe tokea kianzishwe kituo cha Matangatuani kumegunduliwa mbegu ngapi.

Mhe. Spika, unaposema unaleta mswada huu ni lazima hivyo vituo viwe vipo na viwe imara. Lakini ninadhani hamna hata mbegu moja iliyogunduliwa katika kituo cha Matangatuani. Sasa Mhe. Spika, nadhani mswada huu

umekuja katika hiyo hali iliyosemwa ya kuwapa uhalali baadhi ya watu fulani.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 391 *paragraph* ya pili kutoka juu imeeleza sababu ya kuletwa mswada huu ni kwamba Tanzania Bara wameshaanzisha mswada wa aina hii. Kwa hivyo, na Zanzibar Mhe. Spika, tuanzishe. Hatuwezi Mhe. Spika, kuanzisha kwa sababu tu Tanzania Bara wameanzisha. Wao Mhe. Spika, wana vituo vingi na vituo vyao wameviimarisha.

Mhe. Spika, lakini hapa Zanzibar vituo ni viwili na havijaimarishwa. Sasa ikiwa tunaanzisha mswada huu kwa ajili ya hawa wenzetu wa Tanzania Bara wapate uhalali wa kujiunga na hilo shirika la kimataifa, basi na tuanzishe.

Lakini pia mswada huu umesema lengo jengine ni kuwaenzi na kuwatunza wale watafiti wetu. Basi lazima kwanza tuimarishe hivi vituo. Mhe. Spika, ni muhimu sana kutunga sheria ambayo itakuwa na maslahi ya nchi yetu na wananchi wake.

Ushauri wangu Mhe. Spika, ikiwa kweli serikali imekusudia kuwaenzi watafiti wetu basi hivi karibuni Mhe. Spika, tumeshuhudia Waziri wa Katiba na Sheria akiwa na shughuli kubwa ya kuwazawadia wasanii katika kulinda hakimiliki ya wasanii. Kwa hivyo na hawa wafanyiwe vivyo hivyo.

Mimi hili Mhe. Spika, siungi mkono. Na baada ya maoni hayo, ninashukuru. (*Makofi*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi awali ya yote nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na kutupa nguvu na kuweza kutoka katika maeneo yetu hadi hapa; hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah na popote pale tumshukuru.

Vile vile, ninadhani nitakuwa mchache wa shukurani kwa Mhe. Spika, kama sikuyafanya mambo mawili kwako. Kwanza kukushukuru wewe kwa kuweza kutubadilishia hizi saa, kwa sababu hizi saa zilizokuwepo mheshimiwa zilikuwa hazina viwango, lakini mara baada ya kumaliza sherehe ya mapinduzi, umetuwekea na zina nembo ya Baraza. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi na majimbo mengine haya yaliyobakia hapa Zanzibar, tunashukuru sana kwa kulipa hadhi Baraza lako. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nimalizie kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ...

Mhe. Spika: Nimeziweka kwa makusudi ili tusichelewe kuja kwenye vikao. *(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Salehe Nassor Juma: Nimalizie kukushukuru kwa kunipatia na mimi hii nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu machache katika huu mswada uliokuwepo mbele yetu.

Mhe. Spika, mswada wa leo uliopo mbele yetu unazungumzia suala zima la Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu.

Mhe. Spika, kama kuna jambo ambalo sisi Wawakilishi linatupa hadhi katika medali ya kutunga sheria ya Mabunge yaliyokuwepo huku Kusini mwa jangwa la Sahara, basi ni kuupitisha huu mswada. Pindi tutakapoupitisha Mhe. Spika, tunaweza kupata hadhi kwa sababu tangu mwaka 1964 tunaitangaza Zanzibar kwamba inategemea kilimo na ni uti wa mgongo. Sasa kumbe hatujaandaa miundo mbinu ya kukifanya kilimo kuwa ni uti wa mgongo.

Sasa leo ninadhani serikali baada ya kutuletea mswada huu, tunataka kuanza sasa kuandaa *platform* ya kukifanya kilimo kuwa ni uti wa mgongo.

Mimi ninadhani mara tutakapopitisha huu mswada baada ya kuwafanya hawa wagunduzi wa mbegu kuweza kutambuliwa na kuwaenzi, basi ninadhani utafuata mswada mwengine wa kuboresha sasa maslahi ya hawa wataalamu wetu katika sekta hii ya kilimo. (*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi ninadhani mswada huu utawasaidia sana watafiti lakini vile vile utaisaidia nchi hii kwa sababu tunapenda sana kutoa *political statement*. Hivi juzi juzi wakati wa bajeti ya mwaka juzi tumeambiwa kwamba wametuletea mbegu ya Nerika ambayo uzalishaji wake utakuwa hivi na vile, lakini hakuna lililofanyika, Mhe. Spika.

Hii ni kwamba hakuna ile *scientific analysis* katika kuweza kuleta ufanisi kwenye mambo ya kilimo. Sasa mimi ninaamini tutakapopitisha mswada huu, watafiti wetu wataweza kuwa na moyo, mapenzi na hisia ya nchi yao na kufanya kazi kutusaidia sisi wakulima na wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kuwadharau watafiti wetu, watafiti wetu wengi wanakimbia nchi. Mimi hivi ninavyokwambia Mhe. Spika, kama utakwenda Afrika ya Kusini, Botswana utawakutia ma-*lecturers* wengi wanasomesha *crop production*, wanasomesha mambo haya ya *rural economy*. Sasa hawa wametukimbia kwa sababu hatuwaenzi. Mimi ninaamini mswada huu

tukiupitisha hawa waliopo hawataondoka na wale waliopo nje basi watarudi hapa kuja kutuenulia kilimo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi ninadhani katika hili niwapongeze sana taasisi ya utafiti ya Kizimbani walioweza kutuzalishia mbegu hizi, kutuletea *varieties* hizi za muhogo; yaani wameleta *varieties* nne za muhogo pale.

Lakini sasa Mhe. Spika, nilikuwa naomba hawa wataalamu wetu wanapofanya tafiti zao Mhe. Spika, wasiangalie tu ile *academic prestige* ambayo wanayoipata baada ya kujiongezea *degree*s zao, lakini mbegu zao wazilete kwa mujibu wa mabadiliko ya tabia nchi. Unaweza ukamkutia mtaalamu anatoa *varieties* kadhaa za mbegu *regardless* na ile *climatic change*.

Kwa mfano Mhe. Spika, pale Majendele, Mtwara walizalisha mbegu wanaita *high breed* 11648 ya mahindi. Hii mbegu ilikuwa *productive* kweli kweli Shinyanga, Kahama, Mwanza lakini hii mbegu ilikuwa ukiipanda Makunduchi, Vitongoji basi inakuwa ndogo na haizai.

Sasa mimi nilikuwa naomba tu wataalamu wetu wanapozalisha mbegu zao, waangalie kwamba kuna mabadiliko ya tabia ya nchi, kwamba mbegu unayoizalisha Shinyanga ukiileta Vitongoji basi uzaaji wake unatofautiana *due to the climatic change*. Hiyo ni suala la kwanza.

Suala la pili kuna hili suala la mbegu zetu, kwa mfano sisi tumezalisha muhogo Mwari, Bwana nipakulie, Twendezetu, hizi *varieties* nne mulizozitoa za hii mbegu. Lakini Mhe. Spika, sisi tulikuwa na mbegu ya asili inaitwa Ndege, kule Vitongoji pamoja na Kigoma. Mbegu hizi ilikuwa hazishambuliwi na *cassava mill bugs*. Mbegu wanazozizalisha hivi sasa ukizipeleka Vitongoji zinakuja vizuri lakini zinashambuliwa na *cassava mill bugs*, zinakuwa vumbi tu.

Sasa nilikuwa naomba sana wataalamu wetu hawa katika sekta ya kilimo, mbegu zao wanapozalisha waangalie na yale *existing diseases* yaliopo hapa. Hilo ni suala langu la pili.

Jengine Mhe. Spika, nilikuwa ninaangalia hapa kwenye ukurasa 391 katika hii ibara ya 3, "Madhumuni na Sababu za kutungwa kwa mswada huu" ni pamoja na hiki kifungu cha tatu, yaani kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza masharti ya kujiunga Shirika la *UPOV* na kupata manufaa yatokanayo na uanachama huo.

Mhe. Spika, mnasema mwaka 2010 Bunge la Tanzania limepitisha sheria ya kujiunga *UPOV*. Wasiwasi wangu tusijekuwa wanataka kututumia kama *rubber stamp*. Mimi nadhani itabidi Waziri aje atoe ufafanuzi hapa.

Tunajua kwamba ikiwa kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania suala hili lipo na imeshapitisha sheria kusingehitaji *concurrence* ya hili Baraza tena, na sheria nyingi zinapitishwa huko wakaingia katika taasisi za kimataifa bila ya kuja kwenye Baraza. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri, aniambie tutafaidika vipi sisi Wazanzibari kwa kile kitakachotoka huko kwenye taasisi za kimataifa. Lakini kama ni ile ile *4.5 percent* ambayo hayo mambo mengine hatuyapati basi itakuwa wanatudhalilisha na hatuna haja ya kuupitisha huu mswada.

Mhe. Spika, mimi si msemaji sana lakini ninataka nimalizie katika ukurasa wa 377, "Jina na aina ya mbegu". Mhe. Spika, kwenye ibara ya 21 (7).

> "Mrajis atasajili jina lililowasilishwa isipokuwa atakapoona jina hilo haliendani na mazingira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na iwapo jina hilo halipo sawa atamtaka muombaji awasilishe jina jengine"

Sasa Mhe. Spika, mimi ninadhani hii tusimuachie huyu Mrajis, atawadhalilisha watafiti wetu, atayakataa majina yao na ayaelekeze ya kwake. Kwa mfano mimi ninaweza nikakaa Vitongoji nikavumbua aina ya mbegu ya mgomba nikaita *high breed Saleh* 71 mathalani. Nikiita hivyo, atakuja kunikatalia huyu.

Sasa mimi ninadhani hii *technical team*, hili Baraza la Ushauri la Mrajis ndio likae na sio aachiwe Mrajis. Jina lisiwe *regarded* kwamba lazima lilingane na matakwa ya Jamhuri ya Muungano.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nitoe tanbihi nyengine kwa wavumbuzi wetu au wataalamu wetu kwamba kuna kitu sisi katika *botanic* tunakiita *photoperiodism*, kwamba kuna miti ambayo ina *flower* kwa sababu ya urefu wa mchana. Kwa sababu huu mti unazaa, unakuwa ni *photoperiodic control*, unatoa mauwa *due to photoperiodic control.* Sasa wakichanganya mbegu zao kututilia hii basi tunaweza tukapata tatizo. Wanaweza wakachukua *variety* moja ya mbegu ya Kigoma ambapo jua kule linatua saa 1:30 za usiku, miti inayotoa maua kule inahitaji mwangaza wa muda mrefu, lakini Vitongoji saa 12:00 jua limeshatua.

Kwa hivyo, miti hii ni *short day plants* za huku kwetu katika *coastal play are the short day plants.* Kwa hivyo, watakapochanganya mbegu zao kule

wakachukua Bara. Kwa mfano Kigoma ambapo jua linatua saa 2:00 usiku siku nyengine, ukaja ukatuletea sisi Vitongoji wakati jua linatua saa 12:00 za jioni, basi *automatically* ile *photoperiodic control* inakuwa *hindered production* ya mazao yetu inakuwa madogo.

Kwa hivyo, watuchanganyie mbegu na kutuzalishia aina za mbegu kwa mujibu wa maeneo yetu, isijekuwa kama walivyofanya wale jamaa waliotuletea ng'ombe wa jezi kutoka Ulaya, walituletea kule Vitongoji, badala ya kupata lita 20 kwa siku, basi tukawa tunapata lita 3 kwa sababu *temperature* iliopo ilikuwa inazuwia wale ng'ombe kutoa maziwa.

Sasa ninahofia mbegu wanazotaka kuzitoa Kigoma na kwengineko wakazichanganya na kutuletea Vitongoji kule, basi badala ya heka moja kutoa tani 10, basi tunaweza kupata tani 1:30.

Jambo hili litatuathiri sana. Kwa hivyo, mimi nawaomba sana wataalamu wetu kwamba mnapofanya tafiti zenu mu-*regard production* zaidi ya mazao, musi-*regard* kwamba mnatafiti kufanya *degrees* zenu na kuongeza taaluma zenu. Lakini muangalie zaidi sisi wakulima pamoja, maendeleo na mapinduzi ya kilimo hususan kwa vile tumeamua kuongeza kipato na kupunguza umaskini kama ilivyoelezwa katika MKUZA II.

Mhe. Spika, baada ya kupata ufafanuzi nitaunga mkono hoja hii. Ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili au matatu katika hili. Mhe. Spika, mimi nianze kwa kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Lakini baada ya hapo Mhe. Spika, ningeomba vile vile uniruhusu nitowe maoni yangu pamoja na kutaka ufafanuzi wa baadhi ya mambo mawili au mitatu ili Mhe. Waziri, atakapokuja hapa aweze kutusaidia na tuweze kupata taaluma zaidi kwa manufaa yetu sisi tuliomo humu ndani Wazanzibar na Watanzania kwa jumla.

Mhe. Spika, vile vile, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuleta mswada huu muhimu kwetu. Pia, kwa kushirikiana na kamati na baada ya kamati kwishakupitia, kama ambavyo Mwenyekiti amekwisha kuzungumza mwanzo na kubaini baadhi ya mapungufu na baadae kuomba mswada huu kuchapishwa upya na kuletewa mswada ambao kamati imetimiza wajibu wake kama ambavyo taratibu zinavyotuongoza humu ndani.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba kunukuu kifungu cha 132(1), (2) na (3) cha Katiba ya Zanzibar kama hivi ifuatavyo.

Kifungu cha Katiba ya Zanzibar 132(1);

> "Hakuna Sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe kwa ajili ya mambo ya Muungano tu, na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"

Kifungu cha Katiba ya Zanzibar 132(2);

> "Sheria kama hiyo ni lazima ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi na waziri anayehusika"

Kifungu cha Katiba ya Zanzibar 132(3);

> "Pale sheria ndogo inapoundwa kwa mujibu wa uwezo uliowekwa chini ya kifungu cha kwanza na cha pili cha kifungu hiki, itatumika tu pale itakapotimia sharti zote zilizowekwa kwa matumizi ya sheria mama kama ilivyoainishwa na kifungu hiki"

Mhe. Spika, nikitoka hapo nije sasa katika madhumuni. Naomba uniruhusu kunukuu Madhumuni:

> "Kutokana na manufaa yanayopatikana ya kuwa wanachama wa Shirika la *UPOV*, hususan kufikia mapinduzi ya kilimo, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi wa Februari 2010 liliridhia mkataba wa shirika hilo, ili Tanzania iwe wanachama wa Shirika la *UPOV*, inatakiwa kuandaa sheria ambayo inakwenda sambamba na mkataba wa *UPOV*.Kwa kuwa Tanzania Bara tayari ilikwishapitisha sheria ya hati miliki za wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea, Zanzibar inalazimika kuwa na sheria kama hiyo kwa ajili ya kujiunga na Shirika la *UPOV*. Kwa upande wa Zanzibar Wizara ya Kilimo na Maliasili imeandaa rasimu ya sheria kama hiyo, ili iweze kujiunga na Jumuiya ya *UPOV*"

Mhe. Spika, kwa maelezo haya ningependa kuchukua fursa hii kuwashukuru sana ndugu zetu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na kutimiza yale matakwa ya kikatiba kama ambavyo nimekwisha kukariri hapo nyuma.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa, tukiangalia kama vile ambavyo wenzangu wameanza kuchangia, sababu tano ambazo zimewasilishwa hapa. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni ambalo ndio limenisababisha

nikaweza kufika humu ndani leo hii. Nakubaliana na sababu zote tano ambazo zimewasilishwa katika waraka huu, nina ziunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba kupata ufafanuzi wa mambo mawili au matatu. Kwanza Mhe. Spika, nilipokuwa nakipitia hili kabrasha niliona eneo katika ukurasa wa 369, maana halisi ya Mrajis. Mhe. Spika, hapa maana ya Mrajis imeelezwa kuwa maana yake ni Mrajis wa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kama alivyoteuliwa kulingana na kifungu cha 4.

Mhe. Spika, nikiangalia kifungu cha 4 kinasema kwamba waziri atateuwa kwa kutoa tangazo katika gazeti rasmi la serikali mtu au afisa, mwenye vigezo vitakavyotakiwa na uzoefu wa kufanyakazi za Mrajis zilizoainishwa au kuwekwa kwa Mrajis wa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea chini ya sheria hii.

Sasa Mhe. Spika, mimi napata tatizo katika kufahamu kazi za huyu Mrajis, naomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anisaidie ufafanuzi. Kifungu cha 5(a) ambacho kimeandikwa hapa kutoa Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu na mimea. Hapa tunapata maelekezo haya, lakini ukiangalia mbele katika kifungu cha 9(3), Mrajis atakuwa Katibu wa Kamati. Sasa haya masuala ya kuwa Katibu wa Kamati na uwezekano wa kuweza kutoa zile hati, hebu naomba ufafanuzi zaidi katika hili.

Jengine Mhe. Spika, katika kifungu cha 19 maombi ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Kifungu cha 19 kinasema kwamba;

> "Mgunduzi wa mbegu mpya za mimea anaweza kupatiwa hakimiliki za ugunduzi wa mbegu hizo"

Kwa hivyo, ningeomba kufahamu, kwa sababu kipengele hiki kinahusu maombi ya hakimiliki za wagunduzi. Huyu Mgunduzi, maombi yake anayapeleka wapi, anayapeleka kwa Mrajis au anapeleka pahala gani. Atakapokuja Mhe. Waziri, nitaomba anisaidie zaidi.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa naomba kupata ufafanuzi vile vile pale ambapo kuna kipengele kinazungumzia namna ya kumteuwa mwenyekiti katika hii. Katika kifungu cha 44 cha mswada huu kinasomeka kama ifuatavyo Mhe. Spika.

Kifungu cha 44(1);

> "Waziri atateuwa bodi ya rufaa itakayojumuisha wajumbe watatu, ambapo mjumbe mmoja atakuwa ni mtaalamu wa masuala ya kisheria na wajumbe wengine wawili watakuwa ni wataalamu wanaohitimu katika sayansi ya kilimo"

Kifungu cha 44(2);

> "Waziri atateuwa mtu mmoja miongoni mwa wajumbe wa bodi kuwa mwenyekiti"

Mhe. Spika, kutokana na uzoefu wa bodi nyingi zilizopo hapa nchini kwetu tunakuta mara nyingi sana mwenye uwezo na mamlaka ya kuteuwa mwenyekiti, anakuwa ni Mhe. Rais mwenyewe. Sasa katika bodi hii anateuwa Mhe. Waziri, naomba kupata maelekezo zaidi katika hili. Lakini pamoja na maelekezo hayo nakubaliana na mswada huu, naomba nijibiwe kama ambavyo nilikuwa nimeomba na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, napenda nikushukuru kwa dhati kabisa. Niombe radhi kwa usumbufu wa mitambo yetu ya ndani ya Baraza, hiyo ni mipango ya Mwenyezi Mungu. Unajua jambo lolote linaweza kutokea wakati wowote.

Mhe. Spika, na mimi niliona nichangie mswada huu na kabla ya kuanza kuchangia na mimi niseme kwamba natoa pongezi za dhati kabisa kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa kuleta mswada huu wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea, ni suala zuri na ni suala ambalo litaweza kuwapa watu haki zao za msingi katika suala la ubunifu na kuweza kuwapa faida kwa kile ambacho wamekigundua.

Mhe. Spika, mambo ya hakimiliki kwa hapa Zanzibar kwa muda mrefu yalikuwa yanatupa mashaka, watu wengi walikuwa wakibuni mambo mengi, lakini walikuwa hawafaidiki na kile ambacho wanakibuni. Hata katika masuala ya watunzi wa nyimbo, tulikuwa na waimbaji wengi, lakini hatimaye walikuwa wanamalizia maisha yao katika hali ya umaskini kwa kutopata haki zao za msingi katika ule ubunifu walikuwa wakiubuni.
Kwa hivyo, niwashukuru ndugu zetu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa uamuzi wa busara wa kuanzisha hii hakimiliki kwa haraka, baada ya wenzetu wa Tanzania Bara kuanza kufuata sheria hii, baada ya kuridhia mikataba ya kimataifa.

Mhe. Spika, sheria ni jambo zuri sana, lakini kujua sheria na kuifuata inakuwa ni jambo zuri mara mbili zaidi. Kwa sababu tunaweza kutunga sheria, lakini kama wananchi hawakuelimishwa kujua ile sheria, basi inakuwa ni usumbufu kuweza kujua haki zao za msingi.

Kwa hivyo, niombe kwa dhati kabisa, mimi sina tatizo na kuunga mkono hoja hii, lakini baada ya kuipitisha kuwa sheria, niiombe Wizara ya Kilimo na Maliasili kufanya jitihada za kutosha, kwenda kutoa taaluma kwa wananchi ili kuweza kujua sheria hii na kuweza kufaidika na hii sheria. Hususan ukizingatia kwamba sheria hii inawagusa zaidi watu wa vijijini kwa sababu wao ndio wakulima na wao ndio wagunduzi wa suala zima la masuala ya mbegu.

Jengine Mhe. Spika, mimi nataka nije kusaidiwa na Mhe. Waziri. Mhe. Spika, sheria imeangalia zaidi mgunduzi wa mbegu na kuweza kupata hakimiliki, kufaidika na kipato na kupata nishani kwa kile ambacho wamekigundua. Lakini nilikuwa napata mashaka kujua ni namna gani wizara imejipanga kwa hawa wagunduzi katika kuwapa ile tija, kwa sababu mtu anaweza kugundua mbegu, lakini ile mbegu ambayo imegunduliwa na yule mtu kusajiliwa, napata mashaka kwamba endapo mbegu ile ambayo imegunduliwa na mtu tayari keshapata hakimiliki, tayari mbegu imeshaanza kutumika na ubora umeshaonekana.

Kwa zile mbegu ambazo zitakuja kuonekana kwamba hazina ubora na baada ya kuwapa watu tija, basi ikawa inawapa watu hasara.

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu hivi karibuni tu watafiti wetu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili waligundua mbegu ya nerika, mbegu hii ilipata sifa sana. Lakini baada ya kuigundua ile mbegu hatukuweza kujua ubora wake kwa namna inavyotumika, badala ya kuleta tija kwa watu wetu na kwa baadhi ya maeneo mengine ikaanza kuleta hasara. Kumbe mbegu ile baada ya kuondolewa ilionekana zaidi haistahiki kupandwa mabondeni na ilikuwa inastahiki kupandwa katika maeneo ya juu. Sasa hii ilikuwa ni namna moja tu ya ugunduzi wa mbegu ambayo ilikuwa ina mambo mawili.

Jambo la kwanza, haina uwezo wa ubora kwenye mabonde, lakini ina uwezo katika maeneo ya juu. Sasa nina wasi wasi ikija kugunduliwa mbegu nyengine zikawa zina matatizo zaidi ya hii ya nerika. Kwa hivyo, nilikuwa nataka kujua tu katika hii sheria, labda tunaliangalia vipi suala la wale wagunduzi ambao watagundua mbegu ambazo zitakuwa badala ya kuleta tija, basi zinaleta hasara kwa wakulima.

Jengine Mhe. Spika, nataka kusema kwamba nafarajika na suala la kuleta sheria hii ya hakimiliki na ni suala ambalo tunaunga mkono jitihada za wenzetu wa Tanzania Bara baada ya kuridhia mikataba hii ya kimataifa. Ni vyema na ninaendelea kusisitiza Mhe. Spika, kwamba katika kuridhia mikataba yetu, tuwe waangalifu zaidi na sheria zetu, kwa sababu mikataba inaangalia na hali halisi za nchi, sio kila mkataba unaoletwa, basi tukawa tunauridhia kwa kila jambo.

Kwa sababu inategemea na mazingira ya nchi katika suala zima la kuridhia hii mikataba. Kwa hivyo, ni lazima tuwe waangalifu na hizo sheria za wenzetu ambazo wameridhia na suala zima la mazingira ya nchi yetu. Kwa sababu mikataba ya kimataifa iko mingi sana, tunajaribu kuiangalia kwa hali halisi ya hapa na pale. Sina haja ya kuitolea mifano juu ya mikataba ya wenzetu ambao wanakuwa wanaipitisha na sisi kama nchi wanachama, inakuwa haina tija na faida kwa nchi yetu na huwa hatuiungi mkono.

La mwisho, Mhe. Spika, suala hili la hakimiliki, jana nilijaribu kuulizia swali na nikapata majibu juu ya suala la mgunduzi na mtafiti, ambaye kaitafiti ile mbegu na kuweza kuifanyia ubora zaidi kuliko yule mgunduzi, kwa sababu bado napata hofu kwamba aliyegundua akajakuonekana kwamba hakuwa na ubora zaidi wa kupata haki kuliko yule mtafiti.

Mhe. Spika, sababu ya kusema hivi ni kwamba tatizo hili nililikuta China Mhe. Spika, kwa sababu katika mafunzo niliyokwendea yalikuwa ni mafunzo ya hakimiliki, yalileta mzozo mkubwa sana katika kutunga sheria na kuwapa watu haki zao za msingi. Ingawa jana niliambiwa kwamba yule aliyegundua atapata haki yake ya msingi na yule ambaye kafanyiwa utafiti kwa ubora atapata haki yake ya msingi.

Lakini wenzetu sheria yao inakuja kwa mgunduzi, haiji kwa mtu ambaye amefanya utafiti na kufanya ubora. Kwa sababu ukiangaza kufanya utafiti na kufanya ubora wenzetu inakuwa sheria inawabana kwamba ume-*forge* kitu cha mtu ambaye aligundua na wewe kuleta kitu kipya kwa kile ambacho yeye amekigundua.

Tatizo hili Mhe. Spika, lilikuja kuleta ugomvi hata Tanzania Bara, kwa sababu wenzetu wa *Coca Cola* wao ndio walioanzisha ile soda ya *Coca Cola*, lakini mfanyabiashara mwenzetu kaka yetu Bakharesa na yeye alitengeneza soda ya *Coca Cola*. Sasa kukawa na mashaka baina ya kuita soda ya *Coca Cola* na kuita sijui *Azam Cola*, lakini unakuta ladha ni ile ile na wakati mwengine unakuta hata ile ya Bakharesa ladha ni nzuri zaidi kutokana na ubora kuliko ile ya *Coca Cola*. Sasa unajua ni vitu ambavyo vinafanya kuchanganya baina ya mgunduzi na mtafiti.

Mhe. Spika, sisi tulipewa taaluma kubwa zaidi ya kuhusu mgunduzi aliyegundua mbegu ya *apple* na *apple* lililogunduliwa lilikuwa ni jekundu. Lakini watu baada ya kufanya utafiti wakaanza kutengeneza zile mbegu za *apple* kuzifanya katika njia nyengine, ndio yakaanza kujitokeza ma-*apple* ya rangi nyeupe, ma-*apple* ya rangi ya manjano na ladha zake zikawa ziko tofauti. Zile ladha za yule mtafiti zikaonekana zina ubora zaidi, ile mbegu yake ikakubalika zaidi kuliko ile mbegu ya yule mgunduzi ambaye aligundua.

Kwa hivyo, mimi Mhe. Spika, nataka wizara hii watusaidie ni namna gani watakavyoweza ku-*balance*, baina ya mgunduzi na mtafiti, ili kujakuondosha sitofahamu, yule mgunduzi akasema aah! huyu hata kama kafanya utafiti na mbegu yake imekuwa bora, lakini mimi ndiye mgunduzi na hii ni haki yangu mimi ya msingi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nasema kwamba na mimi naunga mkono mswada huu ambao umeonesha matumaini kwa wananchi wetu na hususan wakulima. Kwa hivyo, naamini kwamba suala hili litaanza kuwa chachu ya watu kuanza kutumia akili zao na hekima zao kuanza kujituma katika hali halisi ya kuweza kutafuta ubunifu wa kuweza kugundua mbegu mbali mbali kwa maslahi ya nchi yetu. Baada ya hayo, Mhe. Spika, nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na tuko katika chombo chako kitukufu hiki kwa ajili ya kuchangia mswada huu muhimu kwa maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ambapo mswada huu ulipita kwetu na tuliupitia kwa kina na mabadiliko ambayo yalikuja ni matunda ya Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Awali ya yote Mhe. Spika, nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yangu Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwa kuipa hadhi kamati yetu. Nasema hivyo Mhe. Spika, kwa sababu waziri wa kila wizara ndiye anayewajibika kuwasilisha hotuba za bajeti na miswada kwenye kamati yoyote ile. Siku ambayo kamati yangu ilipitisha mswada huu, kwa bahati mbaya tulikuwa hatuna waziri. Kwa kutambua wajibu wa kamati yetu basi Mwenyekiti wangu wa kamati hiyo Mhe. Salmin Awadh Salmin, alijenga hoja na kusema kwamba kamati haiwezi kuendelea bila ya kuwepo waziri.

Kwa hivyo, hiyo ni kusema kwamba mwenyekiti wangu aliipa hadhi sana kamati yako na alilipa hadhi Baraza la Wawakilishi kwa kupitia sheria na kanuni zake.

Mhe. Spika, nasema tu kwamba kamati yangu ilifanyakazi kubwa ya kuupitia mswada huu na kile ambacho kimeandikwa humu, labda iwe ni makosa ya kiuandishi, lakini yote kamati yangu iliyakubali. Niseme kwamba wajumbe wanapochangia, wajikite zaidi kwenye mswada mpya uliochapishwa, kwa sababu huu mswada mpya uliochapishwa ni kama umezaliwa upya na una marekebisho yote ambayo wajumbe walihitaji kuonekana. Kwa hivyo, ni kusema kwamba mswada wangu ulichapishwa upya na kwamba mabadiliko haya ni mabadiliko ambayo kamati yangu iliyaridhia chini ya mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Spika, niende kwenye kile kifungu ambacho Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, alikizungumza, kifungu cha 44 cha rufaa. Mhe. Spika, kifungu hiki awali kilikuwa ni wajumbe 3, kwamba waziri atateuwa wajumbe 3 wa bodi ya rufaa na ambapo mjumbe mmoja atakuwa ni mwanasheria na wajumbe wawili watakuwa wataalamu wa kilimo. Kamati yangu chini ya busara za mwenyekiti, iliona kwamba kifungu hiki kibadilishwe na kiwe wajumbe 5. Wajumbe wawili wawe ni wanasheria, wajumbe watatu wawe ni wataalamu wa kilimo.

Hoja ni kwamba mwanasheria akikosekana kwenye kamati hii, basi itakuwa hakuna rufaa. Kwa hivyo, tukasema kwamba wajumbe 2 wanasheria wakiwepo, mmoja akidharurika, basi atabakia mmoja na ile kazi ya kisheria itakwenda vizuri na hivyo rufaa itasikilizwa kwa mujibu wa taratibu.

Kwa hivyo, niwaambie Waheshimiwa Wajumbe tu kwamba kifungu hiki kamati walikibadilisha badala ya wajumbe 3, basi watakuwa ni wajumbe 5, ambapo wajumbe 2 watakuwa ni wanasheria na wajumbe 3 watakuwa ni wataalamu wa kilimo. Tukiamini kwamba akikosekana mwanasheria mmoja, basi yule mwengine mmoja atabakia, akikosekana mtaalamu mmoja, basi wale wengine wawili watabakia na hatimaye kazi za utaalamu wa rufaa zitakwenda sambamba.

Mhe. Spika, kifungu chengine ambacho nataka nikitolee ufafanuzi ni kifungu cha 48, kuanzia *marginal note*, lipo neno "mahesabu na ukaguzi". Kwenye uandishi mzuri wa lugha na hata wataalamu wa hesabu, hakuna mahesabu. Tuseme ni hesabu na ukaguzi. Kwa hivyo, hapa imetumika mahesabu kwa kila sehemu. Kwa hivyo, napendekeza kwamba irejee ile lugha ya kihesabu na kwamba hapa isiwe mahesabu, iwe ni hesabu na ukaguzi, na kila penye

mahesabu, basi ibadilishwe na iandikwe hesabu na sio mahesabu, kwa sababu sio lugha nzuri ya kimahesabu kwenye taaluma ya mahesabu.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 48(3) naomba nikinukuu;

> "Mabuku ya mahesabu, ambayo nasema iwe ni hesabu za Afisi ya Mrajis wa Hakimiliki za ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea zitakaguliwa mwishoni mwa mwaka wa fedha na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali"

Mhe. Spika, naomba neno "mwishoni mwa mwaka wa fedha" liondoke. Mkaguzi asifungwe kwamba akaguwe mahesabu haya mwisho wa mwaka wa fedha. Nasema kwamba hesabu hizi zitakaguliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali, akiamua mwisho wa mwaka, akiamua mwanzo wa mwaka, lakini wajibu wa kukagua afisi ya *CAG* ni wajibu wake na yeye ndiye anayejua utaratibu wake wa kukagua, sio aambiwe kwamba akaguwe mwisho wa mwaka kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Spika, baada ya marekebisho haya ambayo nilitaka niwakumbushe wajumbe wenzangu, sina haja ya kuharibu ile kazi nzuri ambayo kamati yangu waliifanya. Niendelee kuwapongeza sana na kwa dhati kabisa na niunge mkono hoja ya mswada huu, na Waheshimiwa Wajumbe waupitishe mswada huu kwa maslahi ya watu wetu, lengo la mswada huu ni kuwalinda wagunduzi wetu wa Zanzibar ambayo watafanya kazi hiyo ya utafiti na kugundua mbegu za aina zote, ili na wao wapate haki ya kazi yao ya utaalamu waliyoifanya kwa maslahi ya leo na kesho.

Kwa hivyo, nawaomba wajumbe wenzangu mswada huu waupitie kwa kina na watakapoona labda hawajafahamu wawaulize wajumbe wa kamati tuwaelekeze na hatimaye mswada upite kwa ajili ya kutoa ruhusa kwa serikali twende sambamba na sheria za kimataifa na sheria za nchi yetu ya Tanzania. Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii na mimi kutia baraka zangu katika mswada huu ambao kwa kweli ni muhimu sana.

Mhe. Spika, jana tulifanyiwa semina kidogo, katika semina ile tulitajiwa faida nyingi ambazo sisi kama Wazanzibari, tutazipata tutakuwa na Sheria kama hizi. Sina haja kuzikariri ni nyingi na kila mjumbe anazijua.

Mimi nataka nianze kwa kuipongeza wizara pamoja na serikali kwa kuleta sheria hii ambayo faida zake zitatusaidia sana, ikiwa ni kweli kwa faida ya

wazanzibari. Maana kuna wenzangu wengine wameonyesha wasi wasi wao hapa kwamba isijekuwa tunawapatia wenzetu njia ya kupata manufaa, pengine wanaweza wakaona ni kikwazo bila ya Zanzibar kuwa na sheria kama hii,Kwa hivyo, tuwapelekee mpaka watunge sheria ili hatimaye tupate njia ya kupita kujiunga na taasisi za kimataifa na kufaidika. Sasa ikiwa ni kweli kwa maslahi ya Zanzibar, basi mimi naunga mkono sana kwa sababu hizi faida ni nyingi na ni muhimu sana.

Jambo jengine ni kwamba Zanzibar hatuwezi kusema kwamba ni nchi ya kilimo moja kwa moja. Lakini wazanzibar kwa asilimia kubwa wanategemea kilimo kama ndio ajira yao. Kama tunavyoambiwa katika takwimu humu kila siku, karibu ya asilimia sabiini ya Wazanzibari ajira yao ni kilimo, hawana pengine pa kushika.

Lakini tumekuwa na tatizo la wadudu wa mimea. Wale wadudu wamekuwa ni tatizo kubwa sana. Kwanza walikuwa wanaingia kwenye mihogo tu na ndio maana wakapata jina la *cassava mealybug*. Lakini kuna haja ya kupata jina jengine la kitaalamu ambalo litajumuisha mazao yote haya. Maana sasa hivi hawaishii kwenye migoho tu wanaingia na kwenye mazao mengine kama maembe, mafenesi, mapera mpaka kwenye minazi na migomba sasa hivi wapo.

Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba sheria hii ikipita, basi itawahamasisha watafiti kugundua aina mpya za mbegu za mimea. Lakini kugundua mbegu za mimea wakati tuna tatizo, hawa itakuwa ni + - = 0. Sasa nilikuwa naomba sana Wizara husika iwahamasishe hawa watafiti, kama kuna jambo muhimu kwanza ni kufanya utafiti wa kupata dawa ya kuulia wale wadudu wakaondoka hapa nchini kwetu ndio hizo mbebu ambazo watazifanyia utafiti wazilete zitakuwa na maana.

Kwa hivyo, kazi ya mwanzo muhimu sana ni kufanya utafiti wakagundua dawa ya kuuwa wale wadudu. Vijidudu vyenyewe vimekaa kama unga unga, vyeupe hivi ni hatari sana kwa maisha yetu. Hili ni ombi, naiyomba Tasisi ya Kilimo, kupitia watafiti wake, basi waangalie uwezekano wa kupata hiyo dawa.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo hili napata tabu, nadhani na wenzangu nao pia ni hivyo hivyo. Maana michango ya wenzangu ni wachache sana walioingia kwenye vifungu moja kwa moja. Hawakufanya hivyo kwa sababu ya dharura ya huu mswada. Huu mswada si mswada wa kawaida. Tuliokuwemo humu sisi ni wana siasa. Huu Mswada ni wa kitaalamu na wa kisayansi sana. Wengi wetu tunapata tabu ya kuweza kufahamu hata vile vifungu. Mimi nimetafuta sana, kulikuwa kuna kifungu nimekitafuta, lakini

sikukiona. Ama kimeandikwa sikukifahamu au hakimo. Lakini labda nikiuliza swali waziri atajua nilichokikusudia.

Mhe. Spika, kwa mfano mtafiti afanye utafiti wake atuletee mbegu mpya ya muhogo, anaileta mwanzo inaweza ikawa na udhibiti lakini kwa muda mfupi. Baadaye mbegu ile ikaenea kwa jamii. Kawaida yetu sisi Wazanzibari tunatabia ya ukarimu, mimi nikishakupanda mgomba akitokea mwenzangu akiupenda ule mgomba wangu atanambia nigaie mche, nitamgaia tena bure siku nyengine au hata nitamuuzia, lakini itakuwa mimi na yeye. Halkadhalika na muhogo na mpunga hivyo hivyo tunafanya hivyo, tunagaiyana mbegu.

Swali langu linakuja hapa. Ikiwa nataka kuuliza hatimiliki ya huyu aliyegundua ile mbegu. Na kawaida Wazanzibari tuna tabia ya ukarimu kugaiyana hizo mbegu. Hayo maslahi ambayo tunayalinda yaende kwa yule yule mgunduzi, tutaweza kuyadhibiti vipi? Mimi sikuona kifungu humu au niseme sijakifahamu. Lakini napata tabu huenda hiyo hatimiliki ikawa haina maana. Au Waziri aje atwambie kutakuwa na utaratibu gani wa kikanuni mpaka tuweze kuona mbegu ya muhogo niliyoipanda miye, akaja jirani yangu huko huko kondeni nikaja nikamgaiya na yeye akamgaiya mwengine, basi maslahi yale yatarudi vipi kwa yule muombaji wa ile hatimiliki. Naomba Mhe. Waziri, akija atueleze ufafanuzi wa namna hii.

Jambo jengine ambalo nataka nilizungumze wenzangu wameligusa sana hapa. Lugha yetu ya Kiswahili sijui kama ni lugha masikini, sidhani kama ni masikini, lakini tuna tabia ya kutohowa maneno ama ya Kiingereza au ya Kiarabu zaidi na wakati mwengine hata maneno ya Kijerumani yamo katika lugha yetu ya Kiswahili, katika kutohowa tuwe waangalifu kidogo. Hili nazungumzia hili suala la urajisi, ukienda kwenye kifungu cha 2 cha ufafanuzi katika hii *copy* ya pili, *copy* ya kwanza ilikuwa halimo hili neno. Ukiangalia maana yake imeandikwa "Rajisi" maana yake ni rajisi ya hakimiliki". Sasa hapo kwanza hujafanya tafsiri. Mimi neno rajisi maana yake siijui, halafu na wewe unanambia kwamba "Rajisi" maana yake rajisi. Ilitakiwa liwepo na neno jengine hapa, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alisema labda liwekwe daftari. Maana "Rajisi" ni rajisi pengine ilivyokusudiwa.

Hoja yangu ipo kwamba hili neno tunalinyambua nyambua, kuna mnyambuliko wa maneno hapa. Asili ya neno hili ni la Kiarabu. Katika Kiarabu ukilinyambua neno tarjis au rajasa, yarjus, tarjisi, rajisi halimo katika mnyambuliko huu. Kwa hivyo, tukitaka kulinyambua, tunyambue maneno yetu ya Kiswahili sio haya, tutapoteza maana. Wenzetu watu wenye lugha hii watatucheka. Neno rajisi ukimwambia Muarabu atacheka maana yake hakuna neno hili katika myambuliko wa lugha yao.

Tunayo maneo yetu ya Kiswahili kwa nini hatusemi kama daftari, japo ni neno la Kiarabu, lakini limezoeleka zaidi na sio la kitaalamu sana, kwa nini hatuiti daftari, tunajaribu kutia maneno, halafu yatatupa tabu. Tena limerudiwa mara nyingi sana katika huu mswada kila pahali. Mimi nilikuwa naomba kila lilipo neno rajisi tulifute tuandike daftari, litaleta maana nzuri zaidi ambayo kila mtu akiisoma atafahamu. Nilikuwa naomba hivyo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 4 *subsection one*, pale pana uteuzi wa mrajis, kile kifungu kidogo cha 1, kinasema Waziri atateuwa kwa kutoa tangazo kwenye gazeti. Sasa maneno haya yanayofuata naomba yafutwe "mtu au afisa mwenye vigezo vinavyotakiwa na uzoefu wa kufanya kazi za mrajisi zilizoainishwa au kuwekwa" nilikuwa naomba mpaka hapo yale maneno yafutwe. Iandikwe tu kwamba "Waziri atateuwa kwa kutoa tangazo katika gazeti, mrajis wa hatimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea chini ya sheria hii."

Hichi kifungu maneno haya niliyosema yatolewe, haya yako katika kifungu cha 3, *subsection three* ya kifungu hichi, ndio yanaeleza sifa na mambo mengine. Kwa hivyo, hii ni *repetition*. Nilikuwa naomba ielezwe tu kuwa Waziri atamteuwa mrajis wa mbegu hizo. Hata ukiangalia kifungu kidogo cha 2 vile vile kuna maneno kama hayo.Pia, naomba nayo yatolewe vile vile.

Kwa mfano "Waziri anaweza kumteua" kwanza hapa asiweze, kama tushakusudia kuwa na naibu mrajis, basi waziri asiweze. Kwa hivyo, isomwe moja kwa moja kwamba waziri atamteuwa naibu mrajis na maafisa wengine. Sasa hayo maneno yanayofuata hapo wenye vigezo vinavyotakiwa na uzoefu ambao watatekeleza baadhi ya kazi mpaka mwisho. Hayo maneno yatolewe yote halafu paongezwe maneno haya ninayojaribu kuyaangalia kama wanasheria watayaona yanafaa watayatia.

"Waziri atamteuwa naibu mrajis na maofisa wengine watakaohitajika kufanya kazi katika ofisi ya mrajisi wa hakimiliki ..." mpaka mwisho.
Haya maneno niliyopendekeza yatolewe haya yanakuja kwenye kifungu cha 3 nacho kinasema: "Kwa madhumuni ya kifungu hichi, vigezo vinavyotakiwa vitajumuisha angalau Shahada ya Kwanza Chuo Kikuu, kutoka katika taasisi yoyote inayotambulika ...."

Kifungu hichi kina *represent* haya maneno niliyosema yafutwe huku ni *repetition* hayana haja.

Mhe. Spika, baada ya marekebisho hayo mafupi, naomba nimalizie kwa kukitaja kifungu cha 9(2) wenzangu wamekigusa, lakini na mimi naomba

nikiguse kwa umuhimu wake. Kama ilivyoandikwa kwamba kilimo si jambo la Muungano. Sasa unapotunga sheria na ukaweka sharti kwamba aje mtu kutoka Jamuhuri ya Muungano au Tanzania Bara na *Inshaallah* itakuwa hivyo.

Tanzania Bara keshokutwa watakuwa Tanganyika, watakuwa na nchi yao na sisi tuna yetu. Halafu kutakuwa na serikali ya tatu ya Jamuhuri ya Muungano. Sasa ikiwa wao watakuwa na nchi yao kuna haja gani ya kutia mtu kutoka Tanganyika au Tanzania Bara, aje hapa katika Serikali ya Zanzibar kwamba aje kwenye Kamati hii, mimi sioni mantiki.

Mhe. Spika, kwa msingi huo, naomba mrajisi wa hatimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbebu za mimea kutoka Tanzania Bara afutwe katika Kamati hii asiwemo kabisa. Baada ya mapendekezo ya marekebisho hayo Mhe. Spika, mimi naendelea kusema ikiwa mswada ni kwa maslahi ya Wazanzibari na *Inshaallah* iwe hivyo, naunga mkono na kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Chonga. Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika mswada huu wa Sheria ya Kuanzisha Sheria za Hatimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza kabisa naomba kwa asilimia 100 kuungana na paragrafu ya mwanzo kabisa ya madhumuni na sababu ya kuwa na mswada huu. Naomba niseme kwa ruhusa yako kama ifuatavyo: Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea imetayarishwa ikiwa ni katika hatua za kutambua umuhimu na kuwaenzi na kuwazawadia watafiti na wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kutokana na kazi ngumu na ya miaka mingi.

Mhe. Spika, ili tuendelee katika kilimo hapana budi na sisi ni lazima tuingie katika uso wa dunia wa kubadilika kutokana na hali ya mazingira inavyobadilika. Bila ya hivyo hatuwezi tukaendelea na kilimo, tukanufaika, tukapata mazao ya kutosha, yakasaidia katika chakula na biashara na kuondoa umasikini katika nchi hii.

Mhe. Spika, kufikia huko kuna kazi kubwa sana na kazi yenyewe ni kazi ya kitaalamu. Bila ya kuwa na utaalamu uliobobea katika fani iliyokusudiwa hili lengo la uvumbuzi au ugunduzi wa mbegu mpya za kilimo haliwezekani. Kwa sababu hili si jambo la kimasihara ni jambo la kimaumbile, ni mabadiliko ya kimaumbile, ni kuleta mbegu mpya kuna masharti yake na utaalamu wake.

Sasa Mhe. Spika, mimi ambalo kidogo limenipa wasi wasi na nataka nipate maelezo ya kutosha hasa kutokana na wenzangu waliokwisha tangulia kuchangia, ni ukurasa wa 391 ya mswada huu wa sheria unasomeka kama ifuatavyo:

> "Kutokana na manufaa yanayopatikana ya kuwa mwanachama wa Shirika la *UPOV*, hususan kufikia Mapinduzi ya Kilimo, Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Februari, 2010, liliridhia Mkataba wa Shirika la *UPOV* inatakiwa kuandaa sheria ambayo itakwenda sambamba na Mkataba wa *UPOV*. Kwa kuwa Tanzania Bara tayari washapitisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya wa Mbegu za Mimea, Zanzibar inalazimika kuwa na sheria kama hiyo kwa ajili ya kujiunga na Shirika la *UPOV*. Kwa upande wa Zanzibar, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeandaa Rasimu ya Sheria kama hiyo ili iweze kujiunga na Jumuiya ya *UPOV*"

Hii Mhe. Spika, inanionesha kuwa kama Bunge la Muungano halikupitisha sheria hii kwa maana hiyo ilikuwa hakuna ulazima wa sisi kujadili mswada huu leo.

Mhe. Spika, ninavyozungumza ni kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na hakuna asiyejua na kwa maana hiyo faraja inayopatikana ya kimuungano na sisi hupewa sehemu sio *privilege* ni haki yetu. Kwa hivyo, tusisifu kwa kupewa haki zitokanazo na Muungano kwa sababu na sisi ni wadau wa muungano huo.

Kwa hivyo, kupata pesa kutoka katika miradi gani iliyotajwa hapa pesa zile ukizitizama ni haki yetu japokuwa tunapewa asilimia ndogo sana kabisa. Lakini ninavyoona Mhe. Spika, kutokana na uwezo wetu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili ilivyo hivi sasa si dhani kuwa tuna uwezo wa kuvumbua mbegu mpya *as such*. Kwa sababu unapovumbua mbegu ikiwa ni mpya ujue ina mambo mengi ambayo ya kujieleza mpaka iweze kukubalika na kuuzika.

Hapo zamani nilipokuwa mwanafunzi (Mhe. Spika, kwa taarifa yako mwaka 1971 nimemaliza darasa la kumi na nne linaitwa *Form VI* hivi sasa). Niliposoma mambo kama haya tuliambiwa kuna kitu kinaitwa *International Board of Nomenclature*, yaani kule mtu anavumbua kitu chake iwe ni mbegu, iwe ni chochote kipya kinapelekwa, kinakwenda kuchunguzwa sifa zake halafu kinapewa jina kutokana na kile kitu chenyewe kilivyo. Kwa mfano hapa Tanzania palitoka aina mpya ya madini na hakuna dunia nzima na ilipokwenda kuchunguzwa ikapata jina la *Tanzanite*.

Hii Mhe. Spika, inamaanisha kwamba mvumbuzi anapogundua kitu kipya, basi kinakuja na heshima zake. Tukiachilia mbali mbegu hizi za kilimo, lakini hata mambo mengine. Kwa mfano kuna Bwana Lamarck alikaa akaangalia viumbe wanavyokua na kubadilika akaleta *theory* yake na akasema *a change in condition create new needs, these new needs lead to development of certain parts of the body, and the ... develop organs are inherited.* Hii *theory* ikaitwa *Theory of Lamarckism.* Japokuwa Charles Darwin alikuja akaipinga baadae kwenye *acquired characters,* lakini inaleta ile dhana ya kuwa mvumbuzi ni lazima ijulikane sifa yake. Sasa kuvumbua zaidi ya kichwa kujaa, ni mambo makubwa sana ya kisayansi ni pamoja na vifaa husika vinavyohusiana na unapoleta mbegu mpya pia inahitaji jina lake.

Sasa kimazingira ninavyoona hivi sasa kama kweli kwa masuala ya ugunduzi wa mbegu mpya kwa Zanzibar bado ingali mapema sana hatujajitayarisha, huko Kizimbani kunavumbuliwa vumbuliwa tu, lakini hatujajitayarisha, bado hali haijawa *so scientific* na huko Pemba ndio kabisa. Kwa hivyo, tuchukulie mswada huu usingelikuja hapa isipokuwa ni wenzetu ambao washatuzidi katika teknolojia hii wameridhia na sisi tunalazimika ili wafaidike wao na sisi watugawie wanachotaka ikiwa ni 4% or $4^1/_2$% sijui huko.

Jengine Mhe. Spika, nitakupa mfano, kuna wanyama wengi duniani mfano kama simba, chui, paka, ukiwatizama wana fanana fanana, lakini kabila ni tofauti. Kwa sababu hizo kutokana na sifa ya yule kiumbe alivyo, sifa za paka, chui na simba ni za aina moja, kuna kitu kinaitwa *generic name,* yaani tukisema hivyo wote ni jamii moja. Sasa katika jamii hiyo japo ikiwa wanafanana kisifa, lakini ni viumbe tofauti hawawezi wakachanganyika na kuzaa kwa pamoja, simba na chui hazai, wala chui na paka hazai.Kwa hivyo, wakawatafautisha, wanaozaa na kundi moja wakawa na jina lao na kundi jengine wakiwa na jina lao. Simba wakamwita *felis* leo, chui wakamwita *felis tigris* na paka wakamwita *felis cat.*

Sasa basi kama utavumbua kitu na kitu kile kikawa si endelevu, kikazaana na tukapata kizazi baina ya kizazi, uvumbuzi ule huwa haujakamilika, kwa Zanzibar bado hatujafika huko. Tunakwenda kwa kubahatisha katika *cross breeding* na tunashindwa kuvumbua kitu kipya.

Mfano Mhe. Spika, tokea mwezi wa 80 Zanzibar kulikuwa na kopa ng'ombe, lipa ng'ombe, waliletwa ngo'mbe kutoka nchi za nje hapa, makubwa, yanatisha, mazuri, kukawa na viwanda vya maziwa. Kwa sababu wale wanatoka katika mazingira yao ambayo wanaweza kuendelea. Wetu sisi pia hapa na wao wanaweza kuendelea. Tukafanya hiyo *cross breeding,* hakuna ng'ombe aliyelipwa, mradi haukuendelea na kiwanda kikafungwa na mpaka leo tunaendelea hivyo hivyo. Vyenginevyo tungekuwa matajiri wakubwa sana

tokea miaka hiyo. Sijui mbegu ya safari hii iliyochukuliwa Kenya mazingira yetu yanafanana.

Tuliingia katika kilimo cha mbegu fupi, ni kweli zilikuwa zikizaa sana, mpunga ni mfupi, lakini uzazi wake ulikuwa ni mkubwa sana, lakini hatukuangalia mazingira. Tukalima mbegu zile mpaka sasa hivi mbegu za zamani zimetutoka na zidi hakuna la kuendelea. Hapa karibuni katika awamu hii ya Baraza kulikuwa na mbegu hapa zinaitwa nerika, zikasifiwa kuliko chochote.

Sasa tunaambiwa kama hazikupata maji kama vuli haziwi, lakini mwanzo tuliambiwa popote tu zinaota. Kwa hivyo, uvumbuzi ni lazima uangalie je, hichi kinachovumbuliwa kinaweza kikatoka kutoka *generation to generation*. Nakusudia tupate *species* na *species*, ni viumbe ambavyo wanaweza wakazaana ovyo na kile kinachozaliwa kikaweza kuzaa wenzake na kikawa endelevu. Neno ni rahisi kuvumbua, lakini ndani yake neno *scientific* naamini Zanzibar bado atujawa tayari. Tumefanya msaada huu kwa sababu ya kuwasaidia watu wapate manufaa yao.

Mhe. Spika, ushauri wangu ikiwa hili linapitishwa hivi, sisi tumeungana na iliyokuwa Serikali ya Tanganyika tukafanya Serikali ya Muungano, mambo mengi ya Muungano yamo ndani ya muungano. Naomba nijibiwe kila kile kilichokuwa cha muungano sisi tulilazimika kufanya sheria kama hii na kuupitisha ndio ikawa sawa sawa. Vyenginevyo kama kweli tunathaminiana.

Kwa hivyo, wenzetu wa Bunge kabla ya kukaa walikuwa waje walete na sisi tujadili halafu tuwe na kauli ya pamoja. Muungano wa haki sawa kwa wote, ndio muungano katika sekta zote sio kwa majina tu. Kwa hivyo, wenzetu wametupiga bao na sisi nasikitika hatukufikiri tukasema Zanzibar inalazimika. Sasa tuseme kama hatukuupitisha tutakuwa tuna kosa gani? Hilo ni moja.

Jengine Mheshimiwa, tunapovumbua kitu tunatoa majina yake pamoja na kuwa ikiwa ni mpunga *generic name* ipo, ikiwa ni muhogo *generic name* ipo, ndio mimea hiyo, lakini ile *species* inayogundulika inakuwa na jina lake, sisi hatuna uwezo huo. Wala lugha ya Kiswahili haijawa lugha rasmi ya kutumika kwa vitu vya sayansi *as such*. Nitatoa mfano Mhe. Spika, hivyo kweli inaelekea *sperm* ni kitu kidogo hukioni hata kwa jicho labda utumie darubini, ukakiita dudu mimba. Mdudu ni mdogo, ukisema dudu ni kubwa, hiyo ndiyo hatari ya kutafsiri mambo kwa Kiswahili.

Sasa lugha yetu ni ndogo na hakuna mambo yoyote ya kisayansi ambayo lugha yetu inatumia, tunachukua mambo ya watu na sisi tukifananisha.

Nataka nijue hivyo vitakavyogunduliwa vipya, vitatumia lugha gani, ya Kiswahili, Kiingereza au Kitaliana ikiwa ndio kubwa inayotumika au vipi. Kwa mfano, mtu yeyote anayejua sayansi kama Mhe. Saleh Nassor Juma, ukimwambia *manihot esculentum*, atajua huu ni muhogo, yeye ni mwanasayansi ndio majina yanavyotolewa. Ukija kwenye *generic name* ina sifa zake na *esculentum* ina sifa yake, mpaka vile viliomo katika ule muhogo mwenyewe. Ukisema *carica papaya*, kila mtu atajua huu ni mpapai, lakini huku kwenye *species' name* kunaweza kukawa na aina mbali mbali kutokana na zile mbegu zenyewe zilivyo.

Sasa sisi baada ya mpunga hatuna jengine, tunajua jina moja tu. Leo tunataka kuvumbua na hakuna kitu kinachovumbuliwa ambacho *binomial*, yaani kiwe na majina mawili. Hivyo kweli Zanzibar hii na wataalamu tulionao tumeshafika huko?

Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati namaliza suala langu la mwisho, nijibiwe mpaka niweze kuridhika. Ni namna gani tumejitayarisha kuingia katika mkataba huu wa kulazimika ili sisi tusiwe ni kuwafanikishia watu mambo yao tu, lakini tuingie katika madhumuni hasa yaliyokusudiwa. Mhe. Spika.nashukuru.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kuendelea na shughuli zetu leo siku ya kwanza ya mkutano wetu wa kumi na tano, Mswada utaendelea kujadiliwa hapo jioni na Waheshimiwa Wajumbe, wafuatao na kwa ujumla tufike mapema, lakini wafuatao wameomba nafasi kwa hiyo tutawaita mara tu tukiingia katika ukumbi huu nao ni Mhe. Dokta Mwinyi haji Makame, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Abdalla Muhammed Ali, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Muhammed Haji Khalid na Mhe. Suleiman Hemed Khamis. Kwa hivyo, tujitahidi tufike mapema ili tuendelee na shughuli zetu.

Waheshimiwa Wajumbe mara baada ya kuondoka humu ndani tukimaliza kikao hichi, basi Waheshimiwa Wajumbe wa upande wa CCM watakuwa na mkutano mdogo mara baada ya kuahirisha kikao hichi. Baada ya hayo sasa Waheshimiwa wajumbe sasa niakhirishe kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na shughuli zetu nimearifiwa na mafundi wa mitambo kwamba kumekuwa na matatizo ya

mkatiko wa *microphone* zetu hizi na ikawa nyengine hazifanyi kazi. Na wanatufahamisha kwamba hii inatokana na *vibration* kubwa ambayo inatokezea tunapopiga meza kwa nguvu sana.

Kipindi cha asubuhi *row* hii ya pili kutoka nyuma *microphone* zetu zilikuwa hazifanyi kazi na wakati mwengine hata Mhe. Ali Salum Haji, alikuwa anahangaika kutafuta *microphone* itayofaa kwa sababu nyengine akizi-*test* kule ili kumpa mawasiliano hayapatikani. Hiyo inatokana na *vibration* kubwa inayotokana na kupiga mabao sana ambayo kwa kweli inafikia kiwango cha kuvunja nidhamu.

Sasa niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe, pia na kwa kufanya meza zetu zidumu kwa muda mkubwa zaidi nadhani panapohaja kufanya hivyo tufanye kwa utaratibu ili kiasi cha kwamba ieleweke tu kwamba hapa tumefurahia, hapo tunamuunga mkono mwenzetu au sehemu fulani inaleta msisimko juu ya mchango ambao mwenzetu anautoa. Lakini tunapopiga mabao haya kama vile ngoma hata wakati mwengine wageni wetu wanapokuja wanatustaajabia, wanaona sasa hii ni nidhamu ya aina gani iliyomo humu ndani.

Niwaombe basi Waheshimiwa Wajumbe, kwa heshima zote makofi yanaruhusika kwa utaratibu wa kupiga mabao lakini iwe si kwa nguvu kiasi cha kuharibu mitambo yetu kwa upande mmoja, lakini pia hata umadhubuti wa meza zetu nao unaweza ukatetereka kama tutaendelea kufanya hivyo. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe turudishe nidhamu katika chombo chetu hiki ili na wanaotuangalia waone kwamba kweli tunafanya kazi na sio tunakuja kucheza.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe, niombe radhi sana kuyasema hayo, nimelazimika niyaseme hayo ili kuona kwamba shughuli zetu zinakwenda vizuri. Ninawashukuru sana.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea, na kama tulivyosema pale kipindi cha mchana kwa sasa naomba nimkaribishe Mhe. Wanu Hafidh Ameir, ambaye baada ya hapo atafuatiwa na Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na wahai na kukutana hapa kujadili Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria za Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za Mbegu za Mimea na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuendelea na majadiliano ya mswada huu.

Mhe. Spika, napenda nimpongeze Kaimu Waziri kwa uwasilishaji wa mswada wake lakini pia nimpongeze mjumbe ambaye amewasilisha hotuba ya mswada huu kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati kwa kuiwasilisha hotuba ile kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba niishukuru serikali kwa kuona kwamba sasa ipo haja ya kuwazawadia wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea; yaani *plant breeders*, kwa kulinda hakimiliki zao na baadae wagunduzi hao kufaidika na jasho lao ambalo wamelifanyia kazi.

Lakini pili, Mhe. Spika, naomba nitoe wito kwa wananchi ambao ni wagunduzi na watafiti kujitokeza kwa wingi ili kufanya ugunduzi wa mbegu mpya za mimea na pale wanapogundua wasisite kusajili kazi zao ili hatimaye wafaidike na kazi hizo, lakini pia wananchi wafaidike na zile mbegu mpya za mimea ambazo zinagunduliwa kama ilivyoelezwa katika madhumuni ya mswada huu.

Mhe. Spika, mswada unazungumzia kuanzisha sheria za Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za Mbegu za Mimea na mambo yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, mimi nataka nimuulize Waziri kwamba mswada umekuja hivi sasa na hili ni jambo jipya ambalo linatambulishwa kwa wananchi, lakini kabla ya mswada huu kuja kuna wagunduzi wale wa zamani ambao nao wamefanya utafiti na wapo hapa Zanzibar, kuna wagunduzi wamegundua mbegu mpya za muhogo, mbegu za mpunga.

Sasa Mhe. Waziri, mimi nataka aniambie kwamba sheria hii inawa-*accommodate* vipi wale wagunduzi ambao waligundua nyuma, ambapo sheria hii itakuja kutumika baadaye, kabla ya sheria hii kutumika.

Mhe. Spika, pili kwa kujua jambo hili ni jipya na ndio kwanza serikali imeamua kulii-*introduce* jambo hili kwa wananchi, ningeiomba serikali kutoa elimu sana kwa wananchi, elimu ya kutosha ili wakajua ni jinsi gani sheria hii itawanufaisha wananchi ambao ndio wagunduzi, lakini pia katika kutoa elimu hiyo ndio pale serikali itafanikiwa kutoa hamasa kwa wananchi ambayo sheria imekusudia kuleta kwa wananchi ili kuona kwamba wananchi wanafanya hii kazi ya ugunduzi, lakini pale wanapofanya pia wasiache kusajili mbegu zao mpya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa niingie katika vifungu vya sheria hii.

Sehemu ya tatu, kifungu cha 18 kinazungumzia kuhusu uthabiti wa mbegu na naomba Mhe. Spika, ninukuu kifungu hicho. Kifungu kinasema kwamba,

“aina za mbegu zitatambulikana kuwa thabiti iwapo sifa maalumu za uzalishaji wake hazitabadilika baada ya marudio ya uzalishaji au katika mzunguko maalumu wa uzalishaji, sifa zake zinafanana katika kila mzunguko".

Mhe. Spika, nataka kujua kwamba ni mara ngapi hasa huyu mgunduzi ambaye atagundua hii mbegu mpya, itatoa nafasi ni kwa muda gani huo mzunguko utatoa nafasi kwa hao wagunduzi ili wazalishaji wa hiyo mbegu wajue kwamba sasa hii mbegu ipo *stable* na inaweza kusajiliwa kama mbegu imegunduliwa. Na sababu ya kusema hivi Mhe. Spika, ni kwamba, siku hizi kuna *environment*, sasa mgunduzi anaweza akapanda mbegu yake kwa mara ya kwanza, mara ya pili, ikaja kama ilivyo, lakini mara ya tatu kutokana na mabadiliko ya *environment* au *weather changing* ile mbegu isije kama alivyoipanda mwanzo. Sasa nataka kujua je sheria imezingatiaje changamoto kama hizi kwa wale wagunduzi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka kusema tu kama sheria ipo kimya kuhusu changamoto hizi au haiku-*cover* haya mambo ambayo labda wagunduzi wangetakiwa kuyazingatia, ningeomba kwamba sheria hii basi changamoto hizi zingetizamwa vizuri katika kanuni za sheria hii.

Pia, sehemu ya 12 Mhe. Spika, kifungu cha 58 inazungumzia kuhusu kanuni za mswada huu na kifungu kinasema kwamba;

> “Waziri anaweza kutunga kanuni kuelezea chochote ambacho sheria hii inaweza kueleza”

Sasa Mhe. Spika, mimi hii sentensi ya Waziri anaweza kuelezea chochote ambacho sheria hii inaweza kueleza naona kama haijakaa vizuri, ingeandikwa tu kama tulivyozoea kwamba waziri anaweza kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya mswada huu na naomba Wajumbe wenzangu waujadili na waunge mkono. Ahsante.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Spika, na mimi ninashukuru jioni hii kunipatia fursa ya kusema machache kuhusiana na sheria hii. Mimi Mhe. Spika, naona kama tunataka kuruka kabla ya kujifunza kutembea.

Mhe. Spika, tunatunga sheria mimi mawazo yangu kwa kubahatisha, kwa sababu hilo tunalolitungia sheria hivi sasa hatuna uhakika wa kwamba litapatikana au halitopatikana. Nina wasiwasi kwamba tunaweza tukachukua miaka kumi mpaka 15 ikawa hawa wagunduzi hawajapatikana. Sasa labda angenieleza tu tunatunga sheria hii kwa kuangalia kwamba tunao watu ambao

wameshafanya mambo hayo, na labda kwa hivi sasa wana-*deserve* kwamba wapewe na wasajiliwe rasmi au inakuja kwa wale ambao labda watafanya ugunduzi na kugundulikana na inabidi tuwatambue.

Mhe. Spika, sheria hii pia katika madhumuni yake makubwa ni kuwatunza na kuwaenzi ambao watakuwa wamegundua. Mhe. Spika, mara nyingi kwa kuwatunza na kuwaenzi inatumika kitu ambacho kitakuwa ni *recognition*, aidha *national* au *international*. Sasa sijui hawa wetu ambao cheti chetu ambacho tunataka kukitoa hapa kitakuwa na utambuzi upi, tutachukua utambuzi huo wa kimataifa au utakuwa ni cheti cha utambuzi hapa petu tu ndani ya nchi.

Mhe. Spika, sasa niendelee kidogo katika kuchanganua sheria hii. Mhe. Spika, kifungu cha 9 ninaelewa kwamba kuna wajumbe ambao wakiangalia kwa jicho jengine na kifungu hiki hasa sehemu yake ya (i) inatambua uwepo kwa Mrajis wa Hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea kutoka Tanzania Bara.

Mhe. Spika, nafikiri katika kuundwa kwa Kamati mara nyingi huwa kuna vigezo fulani tunavyovihitaji ili mtu yule awemo katika Kamati hii. Hapa tunawataja wengi ambao watahitajika kuunda Kamati hii. Na ni imani yangu kwamba hawa waliomo katika kamati hii, waliokwishaainishwa wanatosha kufanya kamati hii itambulike na ifanye kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Sasa labda nimuulize Mhe. Waziri, hiki kipengele cha (i) kimekuja kwa zingatio gani hata tukalazimika tumuweke mtu huyu. Kwa sababu imani yangu ni kwamba kutokuwepo kwake hii kamati itafanya kazi na zitakuwa za ufanisi zaidi. Sasa uwepo wake sijui umekuja kwa maana gani au kwa umuhimu gani kwa kuwa sisi tuwajibike kumuweka mtu huyu.

Lakini Mhe. Spika, sehemu nyengine ambayo kidogo ningetaka nipate maelezo ni kuhusu mfuko wa maendeleo ya haki miliki. Mfuko huu kama ilivyoelezwa katika sheria hii Mhe. Mwenyekiti, utakuwa unapata ruzuku kutoka serikalini, na bila shaka ruzuku hii haitakuwa kwa uendeshaji tu kwamba wale watakaokuwepo katika ofisi kuendesha ofisi yao, isipokuwa ruzuku hii itatumika kwa ajili ya kuwapa watu motisha au kuwawezesha watu kufanya utafiti ili hatimaye watambulikane kwamba ni wagunduzi.

Sasa je, ni katika hatua gani ikifikia mtu huyu ambaye atakuwa anafanya utafiti, sasa ataingia katika ule utaratibu wa kuwa na yeye awezeshwe ili apate kupatiwa nyenzo za kufanya utafiti huo. Hatua gani akishafikia, lakini Mhe. Spika, suala hili nafikiri tunalifanya la upande mmoja, lakini tusiweke wigo ukawa mpana zaidi, ikawa na watu tofauti tofauti, kwa sababu mimi imani

yangu kwamba ugunduzi hauji kwa kusoma kwamba utakuwa umesoma sana, hauji kwa utaalamu kwamba utakuwa ni mtaalamu, inawezekana ukawa ni mtu wa kawaida tu, lakini ukafanya jambo la kuwa na wewe utambulike au lile jambo likawa ni geni katika nchi yako bila ya kuwa wewe umesoma.

Sasa hawa na wao tutawapa labda fursa gani kwa sababu ni imani yangu kwamba hawa ambao watakuwa wanapewa nyenzo na serikali ni wale ambao watakuwa wanatambulika kwa mfano wao labda wamesoma. Kwa hivyo, tuwawezeshe kwa vile wameshafikia hatua fulani, lakini ugunduzi hautaki hivyo; mtu yeyote anaweza akawa mgunduzi na mvumbuzi, sasa je, kuna kipengele ambacho na hawa watu ambao watatokea huko katika kada hiyo na wao wakaingia katika kuwezeshwa kama ilivyoelezwa katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kifungu cha 31ambacho kinaweka masharti au malengo ya usambazaji. Sheria hii inampa mgunduzi kuwa na mamlaka pekee ya kuwa yeye ndiye apewe idhini au ruhusa ya kwamba sasa kazi yake iuzwe, kazi yake isafirishwe, kazi yake isambazwe.

Mimi nafikiria sasa kwa vile yeye ameshapewa cheti na ameshatambulika kwa ugunduzi wake, basi tungetoa fursa sasa kwa ile kamati iliyoundwa kuwa na uwezo sasa wa kuchukua hati ile na kuweza kuifanyia biashara, kwa madhumuni ya kwamba mtu yule akipewa mamlaka yeye peke yake, basi anaweza akazuia haki ile ya matumizi ya alichokigundua kutumika sehemu nyengine au kutotumika, kikabakia kwamba yeye kwa vile tayari keshapata utambuzi kwamba ni mgunduzi asitoe ruhusa ya jambo lile kutumika vyenginevyo na libakie vile vile.

Kwa hivyo, mimi nahisi kwamba itakapofika hatua ya kwamba mgunduzi keshapatikana basi hatua ya kufanya biashara na hatua ya kusafirisha basi iwepo mikononi mwa hiyo bodi itakayoundwa.

Mhe. Spika, labda nirejee kidogo katika mazungumzo yaliyokuwepo asubuhi, Mhe. Spika, nilisikia baadhi ya Wajumbe wakinukuu kwamba baada ya Mjumbe mmoja kutoa maelezo kuhusu hoja hii kuwa ya muungano au si ya muungano. Sasa mimi nilipata wasiwasi kwamba Mhe. Spika, kuna baadhi ya Wajumbe wako ambao labda Katiba yetu hatujaifahamu.

Ninachokielewa mimi kwamba katika katiba kifungu cha pili kimetamka wazi wazi kwamba Zanzibar ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hilo ndilo ninalolifahamu mimi. Na naomba Wajumbe wengine kwa Katiba hii ambayo mpaka hivi leo tunaitumia basi wafahamu hivyo. Zile kauli nyengine zinazotoka ya kusema kwamba hii ni

sehemu ya Jamhuri ya Muungano naomba maneno haya Mhe. Spika, kuanzia leo yakemee kwa nguvu zako zote.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Spika ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu mswada wa sheria ya kuanzisha hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza niunge mkono mswada huu asilimia mia kwa mia kwa sababu mswada huu utatupelekea hawa wagunduzi ambao kuwa tunawatarajia kuwepo hapa Zanzibar na sisi kugundua mambo muhimu ambayo kuwa ni moja ya maslahi ya wazanzibari ambayo asilimia haipungui 70 basi ni wakulima. Kwa hivyo, kuletwa sheria hii nadhani itatusaidia kama itatekelezwa vile inavyokusudiwa.

Mhe. Spika, kwanza niseme kwamba Zanzibar wanaweza wakatokea wavumbuzi, lakini Zanzibar ina moja ya kuwadharau wale watu wake kuwaona ni watu waliokuwa hawajui kitu, lakini mimi naamini kwamba watu kama hawa wanaweza wakatokea. Lakini serikali inahitaji kuwawezesha watu hawa ili kufanya shughuli zao hasa wale watakaotokea katika kisiwa chetu. Tusitegemee kwamba wavumbuzi hawa wote wanatokea nchi nyengine, tuamini kwamba na sisi Zanzibar iwe ni sehemu ya kutoa watu kama hawa ili ule wigo wetu ukamilike.

Mhe. Spika, mimi nikianza kuchangia nitahitaji ufafanuzi katika baadhi ya vifungu ili niweze kuifahamu sheria hii.

.

Sehemu ya kwanza ambayo nataka nipatiwe ufafanuzi ni sehemu hii ya kwanza katika kifungu cha pili hiki, kinachoandikwa ufafanuzi ambao kuwa ina tafsiri ya wakala inayohusiana na muombaji au mmiliki wa haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea, lakini kisha akasema maana yake ni mtu ambaye amepewa mamlaka na muombaji au mmiliki kufanya kwa niaba ya muombaji au mmiliki.

Lakini muombaji amesema hapa kuwa ni mgunduzi mwenye haki ya kufanya maombi ya kupatiwa haki miliki ya ugunduzi kulingana na maana ya mgunduzi. Sasa huyu wakala katika kifungu hiki naomba Mhe. Waziri, akija anieleze ina maana ya huyu mtu anayepewa mamlaka na muombaji wa mmiliki kufanya kwa niaba ya muombaji. Kwa sababu ukisema kufanya kuna maana pengine kifungu hiki kimempa uwezo wa kufanya mpaka kumuombea

ile haki miliki. Sasa nitahitaji ufafanuzi zaidi ili nipate kuelewa maana halisi ilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, jambo la pili katika kifungu cha 6(2) taarifa zitakazoorodheshwa katika Rajisi kwa kila aina itakayosajiliwa zitajumuisha aina za mbegu na jina la bidhaa, jina kamili na anuani ya muombaji au mmiliki wa haki miliki za wagunduzi. Sasa huku Rajisi katika kifungu hicho hicho cha 6 kasema kuwa Rajisi itakuwa ni ushahidi wa awali kwa jambo lolote litakaloingizwa. Sasa kama itakuwa ni ushahidi kwa nini katika kifungu hiki isiwekwe wakala au mwakilishi na yeye kuwa ni miongoni mwa hiyo neno la tafsiri ya Rajisi? Hilo naomba Mhe. Waziri, atakapokuja anipe ufafanuzi ili nipate kufahamu.

Lakini la tatu, Mhe. Spika, kifungu cha 9 kamati ya ushauri wa hakimiliki za wagunduzi, kasema wajumbe wa kamati watateuliwa na Waziri kwa kushirikiana na mamlaka husika angalau watatu miongoni mwao wawe wanawake na watakaojumuisha. Sasa hapa nina swali watakaojumuisha wawe ni watatu wanawake wanaotoka upande mwengine watakaojumuisha pamoja na taasisi hizi au watatoka miongoni mwa hizi taasisi zinazotajwa.

Hilo Mhe. Spika, nalo pia naomba nipate ufafanuzi, na kama ni hiyo mamlaka husika basi pia nayo Mhe. Waziri ,ninavyoomba hapa katika angalau watatu miongoni mwao wawe wanawake basi pafanyiwe marekebisho mamlaka husika wasiozidi watatu miongoni mwao wawe wanawake. Naomba lisomeke hivyo Mhe. Spika, au tupate ufafanuzi zaidi kakusudia nini.

Lakini jengine kifungu cha 4(3) kwa madhumuni ya kifungu hiki vigezo vinavyotakiwa vinajumuisha angalau Shahada ya Chuo Kikuu kutoka taasisi yoyote inayotambulika katika fani ya sayansi ya kilimo, sheria au fani inayofanana pamoja na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano.

Mhe. Spika, mtu yeyote aliyekuwa na fani basi si lazima awe na uzoefu usiopungua miaka mitano, hii miaka mitano ni mingi. Ikiwa ana uzoefu kweli au ana fani ile iliyokusudiwa basi japo miaka miwili anaweza kufaa mtu huyu katika miongoni mwa hao watu watakaotakiwa. Lakini ukisema miaka mitano basi miaka hiyo ni mingi.

Kwanza Mhe. Spika, tuna wanafunzi wengi waliosoma kutoka Vyuo Vikuu walio na fani mbali mbali, sasa hili suala la uzoefu wa kazi pia nalo si lazima lipewe kipaumbele, kinachotakiwa ni ile fani inayokusudiwa. Mtu yeyote, jambo lolote lile kama hajajifunza basi hawezi kuupata uzoefu. Kwa hivyo, tuwaone na wale wanafunzi wetu wanaotoka Vyuo Vikuu ili waweze kupata hizi nafasi za ajira.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kifungu cha 24(1), muombaji anaweza kufanya marekebisho katika mambo yake kwa ajili ya kupatiwa hakimiliki na aina ya mbegu kwa wakati wowote bila ya kuathiri tarehe ya maombi itakayozingatiwa, kwamba marekebisho hayo hayaathiri aina ya mbegu zinazofanyiwa maombi hayo.

Mhe. Spika, hiki kifungu kilichoko pembeni ni marekebisho ya maombi. Sasa kama ni marekebisho ambayo pengine huyu mtu keshafanya makosa halafu wewe unakwenda kumwambia kuwa muombaji anaweza, mimi ningeomba tukiangalie iwe ni muombaji atafanya marekebisho katika maombi yake kwa ajili ya kupatiwa hakimiliki. Kwa sababu kishaandikwa kwamba ni marekebisho ya maoni, sasa kama ni marekebisho usimwambie anaweza ina maana kama ni marekebisho lazima afanye ili marekebisho yale yawe sahihi.

Baada ya hayo mimi naiomba serikali kuwa mswada huu wa kutafuta hawa wavumbuzi utaendana sana na vyuo vya utafiti. Mhe. Spika, la kusikitisha kuna Vyuo vya Utafiti ambavyo hata hudhanii ukifika pale kwenye chuo ukaambiwa kuwa hiki ni Chuo cha Utafiti. Kwa hivyo, tunahitaji kuona wenzetu wanapiga hatua mbele lakini na sisi tunatakiwa tujirekebishe katika lile tunalolitafuta, tuwe na moyo wa dhati katika kutafuta hili lakini vyuo vyetu vya utafiti basi tuvifanyie marekebisho makubwa, si hivyo watatafutwa wavumbuzi tu kwa kutegemea sehemu nyengine tuletewe hapa, watakapokuja kwetu Zanzibar sisi hatuna utafiti wowote tutakaofanya na watu wale hatufiki pahali na tutashindwa.

Kwa hivyo, naiomba serikali kama inataka kuiga mambo ya watu basi na wao angalau wajitutumue kidogo, vile vyuo vyao vya utafiti vilivyopo waweze kuviwezesha na viwe vina sifa hasa ya vyuo vya utafiti, lakini kwa vile vilivyo sidhani kama tutafikia pahali tupige hatua kwa hayo maendeleo tunayoyataka.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami jioni hii kupata nafasi na kusema machache sana kuhusu mswada huu ulioko mbele yetu. La msingi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa jioni hii kuendeleza kazi zetu, pia na wewe kunipa nafasi hii.

Vile vile, nimpongeze Mhe. Kaimu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuwasilisha kwake vyema, tumemfahamu. Pia waandalizi wa mswada huu ili kuja kufika hapa kwa kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi na hatimaye jioni hii au kesho asubuhi pengine kuwa ni sheria.

Mhe. Spika, mara nyingi tunaletewa miswada kuijadili na hatimaye ikawa sheria, lakini pia tunaambiwa kuwa sheria bila kanuni mara nyengine huwa haitekelezeki, sheria inapita leo au kesho kanuni ya kutekeleza sheria hii itachukua muda gani ili huu utafiti na mambo mengine yaliyokusudiwa katika sheria hii yaweze kutekelezwa mapema. Kwa sababu sheria hii kwa vyovyote leo, kesho itapita, na Mhe. Rais au yeyote atayehusika na kuweka saini ataweka saini yake ili mswada huu uwe sheria. Lakini kanuni zake zitachukua muda gani na kuwa tayari kuanza kutumika pamoja na sheria hii.

Mhe. Spika, mimi nianze na Sehemu ya Pili kifungu cha 3 kuanzishwa kwa ofisi. Hapa tumeambiwa kwamba itaanzishwa ndani ya wizara inayohusika na kilimo ofisi itakayojulikana kama ofisi ya hakimiliki na kuendelea mpaka mwisho. Sasa najiuliza, tunaanzisha ofisi hizo nafasi tunazo? Mara nyingi Mhe. Spika, tunapotembea katika mawizara tunakuta baadhi ya taasisi baada ya kuwa na ofisi wana vituturi tu, je hawa watakuwa na ofisi au watakuwa na kituturi ndani ya kilimo? Kama hii ni ofisi kweli basi wawe na ofisi kwa sababu hii ni taasisi muhimu wasiwe na kituturi kama tulivyoona wengine.

Mara nyengine kichwa kikiwa ndani ofisini mguu uko mlangoni, tunaita ofisi hiyo mbona tunajidumaza wenyewe; tunaunda ofisi pa kuziweka hatuna lakini na sisi tuwemo tu, kwanza tungetafuta hiyo ofisi ikawepo na hatimaye ndio tukaanzisha mambo mengine.

Mhe. Spika, hofu yangu kuwa tunaanzisha taasisi kubwa na nzuri ambayo tunataka iwe na kiwango cha kitaifa na kimataifa, lakini kuja ikaundwa hii taasisi na hatimaye ofisi yake ikawa ni kituturi kama tulivyoziona ofisi nyengine kituturi au jumba bovu si vizuri. Taasisi mpya lakini kama kuna jua linapenya, kama kuna mvua karatasi zinaogelea. Hivi ndivyo taasisi zetu nyingi zilivyo sijui hii watu wa kilimo tayari wanayo ofisi ya kweli au wana kituturi wanapotaka kuwaweka hawa.

Mhe. Spika, jengine ni Sehemu ya Nne kifungu cha 3 kuhusu mrajisi na uzoefu wake wa kazi. Mwenzangu kasema miaka mitano ni mingi, mimi namuunga mkono kuwa miaka mitano ni mingi ya uzoefu wa kazi. Kwa sababu huyo aliyefanya kazi kwa miaka mitano hapo mwanzo alikuwa ana mwaka *zero* akaanza ndio ikafika hiyo mitano. Sasa mimi ningependekeza angalau mwenye uzoefu wa miaka mitatu, miaka mitano ni mingi sana na hii ni taasisi na ni mpya ambayo inataka kuanzishwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi ningependekeza badala ya uzoefu wa miaka mitano basi iwe angalau uzoefu wa miaka mitatu au miwili.

Mhe. Spika, niende katika kifungu cha 9 ukurasa wa 372 kuhusu hii kamati ambayo muundo wake itakuwa na mtu wa kwanza. (a) Afisa Mwandamizi

mwenye elimu ya sayansi ya kilimo kutoka katika wizara ambaye atakuwa mwenyekiti wa kamati. Mwenye elimu ya sayansi ya kilimo hiyo elimu yake ya kiwango gani, ya cheti, *diploma, degree, PhD au Professor*. Kwa sababu kaambiwa tu awe na elimu ya sayansi ya kilimo lakini haikutajwa ya kiwango gani.

Halafu hapa kafanywa huyu mrajisi kuwa atakuwa ndio katibu. Katibu mara zote anakuwa ni karani wa ile kamati, katika ofisi mrajisi ndiye bosi kwa hivyo kuna wakati atakuwa yeye ndiye kiongozi, kuna wakati atakuwa yeye ndiye mtumishi mkuu. Mimi mawazo yangu au pendekezo langu huyu mwanasheria wa wizara aliyemo katika muundo wa hii kamati ndiye awe katibu wa kamati na mrajisi awe ni kama mjumbe tu katika kamati hiyo.

Halafu huyu mrajisi mwengine anayetoka upande mwengine Tanzania Bara, lakini hakuna Tanzania Bara anayetoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa hii taasisi ni yetu Wazanzibari tunaunda kamati yetu kwa nini tumpenyeze mtu pahala ambapo hapenyi? Kwa nini tumtie mtu pahala ambapo haingii? Au tujaalie sisi wenyewe bado hatujawa na uwezo wa kuiongoza hii kamati yetu mpaka atoke mtu huko aje atuongezee nguvu.

Kama ni hivyo basi hatuko tayari, kwanza tusomeni mpaka tufikie kiwango cha kuweza kujitegemea ndio tuanze hizi kazi zetu, lakini tusiunde kamati halafu tukapenyeza mtu pahala ambapo hapenyi au pahala ambapo haingii ilimradi tu na sisi iwe tumeunda hilo jambo. Mhe. Spika, taasisi hii ni yetu, kwa hivyo lazima iwe na Wazanzibari wenyewe na waiongoze wenyewe.

Sasa niende katika uwezo wa kamati kifungu cha 12(b), kutoa ushauri kwa mrajisi juu ya masuala maalumu na ya kawaida, haya masuala maalumu ni masuala gani, masuala ya kawaida itakuwa ni masuala ya kawaida ya nyendo zao za kazi na mipango yao ya kawaida, lakini haya maalumu ni yepi hayo. Kwa sababu tumezoea kila jambo sisi tuna maalumu, tuna kazi maalumu, tuna idara maalumu, hii maalumu karibu itatawala sana katika kila taasisi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ningeliomba kuuliza haya masuala maalumu ni masuala gani.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba mimi sina mchango mkubwa kuhusu suala hili, lakini niende kidogo katika ukurasa wa 391 kwenye *paragraph* ya pili inayozungumza hivi ambayo sitaki niisome yote. “Kutokana na manufaa yanayopatikana ya kuwa mwanachama wa Shirika la *UPOV* hususan kufikia Mapinduzi ya Kilimo, Bunge la Jamhuri ya Muungano limetunga lilivyotunga”. Sasa nije sehemu ya mwisho huku, “kwa upande wa Zanzibar; Wizara ya Kilimo na Maliasili inaandaa rasimu ya sheria kama hii ili iweze kujiunga na Jumuiya ya *UPOV*.

Sasa Wizara ya Kilimo kila mtu ana yake lakini Mhe. Spika, *letter head* ya wizara zote za Tanzania hata zile ambazo si za Muungano wanatumia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa kama hawa wamejiunga na sisi ni Tanzania kama wao, sasa sisi tukienda kule iko nafasi au tunajipenyeza tu kwa nguvu? Uzoefu kwa kule sehemu ambayo Tanzania ishajipeleka Zanzibar ikitaka kujiingiza haiingii tunaambiwa hapa nyinyi nafasi yenu ni Tanzania. Sasa inasemekana tangu huko mwanzo kuwa tutapata mafao makubwa sana tutasaidiwa. Mimi ningependa kusema Mhe. Spika, watu wasione ile misaada inayotoka kwenye Jamhuri ya Muungano kuwa tunasaidiwa ni haki yetu kwa sababu na sisi ni Watanzania.

Hapa asubuhi zilitajwa taasisi mbali mbali za kimataifa ambazo zinakuja Tanzania na Zanzibar wanasema kuwa tunasaidiwa, kama ni jambo la kimataifa la Tanzania kupewa Zanzibar si kusaidiwa ni kupewa haki yake, watu wasiseme kuwa Zanzibar tunasaidiwa ni haki ambayo imekuja Tanzania na sisi ni sehemu ya Tanzania.

Kwa hivyo, hatusaidiwi itakuwa ni haki yetu sijui kwa nini watu wanasema tunanufaika kwa kusaidiwa, hatusaidiwi, tunapewa ile haki ambayo na sisi tunahitaji tuipate.Sasa kama katika jumuiya hii tayari Tanzania ni mwanachama Mhe. Spika, kwa Zanzibar tungelingojea mpaka Bunge la Katiba likamalizika tukawa na serikali tatu tukajiunga tukawa kama Zanzibar, iwe ile ya mwanzo Tanganyika wamejiunga, na sisi Wazanzibari tunajiunga kwa upande wetu. Kwa sababu hii taasisi au Wizara ya Kilimo na Maliasili ni wizara ambayo si ya kimuungano, lakini wenzetu kule wanatumia *letter head* ya Muungano na hatimaye wananufaika wao. Mhe. Spika, huo ndio muono wangu mimi kuhusu hilo.

Halafu karatasi nyengine chini nambari 20 imesema kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza masharti ya kujiunga na Shirika la *UPOV* na kupata manufaa yanayotokana na uanachama huo. Je, ina maana huu uanachama wa Jamhuri hautimii mpaka na sisi tujiunge? Kama ni hivyo tusiwatimizie tungojee na sisi tujiunge kwa upande wetu. Mhe. Spika, kama sijaelewa vyema kuhusu vifungu hivi nilivyovisema wakati huu ningeomba mtoa hoja anielimishe ili nami nielimike vizuri.

Mhe. Spika, tunasema tunafanya utafiti wa mbegu mpya, tujaalie sisi katika kufanya utafiti tukagundua mbegu au mmea tukahisi ni mpya, lakini sehemu nyengine duniani pengine tayari ile mbegu au mmea ule tulioufanyia utafiti sisi hapa kuwa ni mpya imegunduliwa, tutapofanya kuisajili kupata hakimiliki yule mgunduzi wa mwanzo hatoweza kutushtaki kuwa tumechukua utafiti wake au mbegu yake kuifanya kuwa ni ya kwetu. Kwa sababu pengine kaigundua mwanzo kuliko sisi.

Halafu hivi karibuni miaka miwili nyuma tulikuwa na mbegu ya mpunga sina hakika kuwa tumegundua sisi au vipi, *NERICA*. Ilivuma hapa ikawa zogo kubwa *NERICA*, *NERICA*, lakini baada ya mwaka ule sasa kimya. Mbegu ile Mhe. Spika, imefikia wapi, ilikuwa ni ugunduzi wetu au iligunduliwa pahala tukaletewa tu, imefeli au vipi? Kwa sababu zogo lililokuwepo juu ya mbegu ile lilikuwa halina mithali, mimi nilidhani kuwa nitajigomboa kwa kilimo cha mpunga lakini hatimaye naona kimya. Ningeiomba Wizara ya Kilimo na Maliasili Mhe. Spika, itueleze mbegu ile imefikia wapi.

Baada ya hayo machache ahsante sana nitaunga mkono hoja pindi nikijibiwa yale niliyoyaeleza. Ahsante.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi kwa upande wangu nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika masuala mazima ya mswada huu wa sheria ya Kuanzisha Sheria za Hakimiliki za Wagunduzi na Aina mpya za Mbegu za Mimea na mambo yanayohusiana na hayo.

Kwanza Mhe. Spika, napenda nichukue nafasi hii ya kumshukuru Waziri wa Kilimo na Maliasili pamoja na watendaji wake wote kwa kuleta mswada huu ambao ni mswada muhimu. Hivi ndivyo inavyotakiwa tuwe kwa sababu kama ni watu ambao wanaendelea hatuwezi kubakia nyuma, kila jipya linalokuja kwa maslahi na faida ya watu wetu ni lazima na sisi tuwe mbele. Na ni lazima twende kwa mujibu wa wakati, haiwezekani sisi Wazanzibari tukabakia nyuma, haidhuru elimu yetu bado ni ndogo na watu wetu hawajajua sana, lakini ni moja katika mambo ya kuweza kujifunza. Kwa hivyo, mimi namshukuru Mhe. Waziri, kwa kuleta mswada huu kwa sisi Wazanzibari tukaweza nasi angalau kupiga hatua.

Mhe. Spika, sheria ya hakimiliki za ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea zina mambo mawili, wanaohusika katika suala hili ni watu wa aina mbili au wataalamu wawili. Mtaalamu mmoja ni mtafiti na mtaalamu wa pili ni mgunduzi. Inawezekana mtafiti na mgunduzi wakashirikiana pahala pamoja wakaleta kitu kipya, au inawezekana mtafiti akatafiti akatoa maelezo yake akamalizia baadae mgunduzi kutokana na utafiti wa yule bwana akaweza yeye kugundua kitu. Hapa tunazungumzia masuala mazima ya ugunduzi wa mbegu.

Mhe. Spika, mimi ninachomuomba Mhe. Waziri watu wawili hawa watafiti na wagunduzi katika kugundua masuala mazima ya mbegu za mimea basi kwanza watambuliwe, wizara hii iwatambue. Lakini vile vile watunzwe na wizara na wanapofanya vizuri wazawadiwe. Haya ni mambo ya msingi na ni mambo muhimu, kila kitu kina *motivation* yake na ndio maana katika kazi

zetu za kisasa tunasema neno la *appraisal,* mtu akifanya vizuri afanyiwe *appraisal,* apewe *increment,* apewe bahashishi.

Kwa hivyo, ikiwa tutakuwa na wagunduzi wetu wa hapa Zanzibar basi tusiwaweke legelege tuwe nao pamoja, tushirikiane nao, tuwatunze, tuwalinde na halafu tuwazawadie. Hivi ndivyo inavyotakiwa, kwa sababu hata mtoto unakwenda safari ukirudi ukimpa pipi unasema si anafurahi, hata mke na mume.

Mke na mume wanasema, *"Almar-atu Sui ala baaliha, Fadhwalla swaalihi Ala baaliha".* Yaani mwanamke *bashashatul- mar-uu*, yaani bashasha ya mwanamke *afdhwalu minal-atwaa, fakaifa idhaa hadha lbashashatul-atwaa.* Hii inakuja, iko hiyo inasema usemi wa Kiarabu, *bashashatul-mar-uu akhyaruu minal atwaa, fakaifa idhaa hadha lbashashatul wal-atwaa*. Yaani ile bashasha tu ya mwanamke basi ni kikubwa kwake yeye kabla hujampa kitu, jee ikawa ile bashasha na kile kitu viwili vimechanganyika itakuwaje?

Mhe. Spika: Mheshimiwa mimi sisikii kitu huku, lugha unayoitumia mimi sisikii. Kwa hivyo, jitahidi kama unafanya *quotation* fulani basi tupe maana yake kidogo.*(Kicheko)*

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Sasa yaani ile furaha tu baina ya mume na mke katika nyumba ni kitu kikubwa sana, baina ya watu wawili sikwambii katika zile furaha zenu za watu wawili siku ile ukasema mke wangu leo nakuletea hiki mambo yatazidi *marratain*. (mara mbili)

Kwa hiyo na hawa kuwazawadia si kitu kibaya ni jambo zuri, *motivation* na sisi tunasema katika utumishi wa umma watu wetu wazawadiwe hakuna ubaya ndani yake.

Mhe. Spika, kwa hivyo, suala la ugunduzi huu wa mbegu ni suala muhimu sana na tunao watu wetu hawa ambao ni wataalamu wadogo wadogo na ambao wamesoma masomo ya sayansi. Kwa hivyo, tuna wajibu wa kuwahifadhi watu hawa na ni watafiti wazuri na wanayo elimu ya kufanya hivyo. Sasa kwa suala hili mimi ninachomuomba Mhe. Waziri, baina ya watu wawili hawa au kikundi cha watafiti na kikundi cha wagunduzi wawekwe mahala pamoja shughuli zao zifanywe.

Mimi nilikuwa nasema zamani hapa kila wizara ina sera na masuala ya utafiti yamo, lakini nikasema mwisho wake hebu tuwe na kitu cha kitaifa huu utafiti uwe wa kitaifa, ni muhimu sana kwa sababu pale mtakuwa mnajua mambo yote ya kitaifa, lakini sasa hapa itakuwa kila mmoja na sehemu yake ya utafiti

ndio sawa katika kila wizara, lakini tuwe nayo moja ya kitaifa utafiti wa kitaifa.

Sasa hili ni muhimu nalo likatambulika kitaifa, utafiti huu hatuwezi kuacha watu hawa legelege, hawa watu wanahitajika na huko mbele katika mazungumzo yao utaona jinsi gani hawa wanavyotaka kutambuliwa na dunia. Kwa hivyo, mtu kwanza unaanza kwako, *charity begins at home* au sivyo? Mambo mazuri kwanza yanaanza pale nyumbani, *minal akrabina*, kwa wale walio karibu. Ndio sasa watafiti wetu na wagunduzi sisi kama ni wizara basi tuwahifadhi, tuwalinde na tuwape kila fursa zinazohitajika.

Mhe. Waziri, tuwe nao watu hawa. Tuwe na *union* yao wajulikane, watambulike, watambulishwe, wawe *recognized***,** utambulisho ni kitu muhimu watambuliwe wasifichwefichwe, watolewe nje wajulikane waelezewe katika magazeti kwamba hawa ni wagunduzi wetu na wanatusaidia katika ugunduzi wa mambo ya mimea. Hili ni suala la msingi.

Jambo jengine Mhe. Spika, kuna kitu ambacho kinaibuka, kuna Shirika la Kimataifa limesaini mkataba wa wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Sasa Mhe. Spika, mimi nataka kumuuliza Mhe. Waziri, hili Shirika la Kimataifa kiasi gani linatambulika kwa hapa Zanzibar? Yaani hili shirika ni shirika la kimataifa na sisi tuko Unguja tunataka watu wetu na wao wawe katika shirika hili wajulikane wawe *recognized*, hakuna mtu aliekuwa hapendi *recognition*.

Mimi kama nakuja hapa mmoja wenu, jambo la mwanzo mtapenda mnitambue au kila mtu katika dunia au hata katika Katiba yetu hutambulika. Sasa hii *recognition* sisi katika Shirika hili la kimataifa ambao limesaini mkataba wa hakimiliki, sisi tuna kitu gani cha kusema juu ya mkataba huu au kuna masharti gani ya mkataba huu. Kwa sababu sisi hapa Zanzibar tuna tabia ya kuchukuwa mikataba tukasaini, *without any adequate ground.* Wewe unasaini mkataba tu hujui masharti ya mkataba ule.

Tumeshawahi kuona baadhi ya mikataba mingi inakuwa *signed* hapa lakini baadae tunagundua kwamba mikataba hii sisi haitufai. Lakini kwa sababu tunataka twende pamoja na wakati basi haya tunasaini tu, hivyo hivyo. Lakini sasa mimi ningelipenda kujua hapa katika Shirika hili la Kimataifa lilosaini mkataba huu wa hakimiliki je, nini masharti ya mkataba huu wenyewe wanaita *International Union for the Protection of New Varieties of Plants*.
Mhe. Spika, watafiti hawa pamoja na wagunduzi wanahitaji kuendesha majaribio, yaani wanahitaji kufanya *experiment* . Mimi ninachokiona sio kitu kibaya, hii ni moja katika kazi zao wanapofanya utafiti, ni lazima wafanye

majaribio. Na katika kufanya *experiment* wanahitaji kupata nyenzo, lazima wawe nazo.

Je, Mhe. Waziri, umewaandaa vipi hawa, sio kusema tu humu katika karatasi. Hawa watu ni masikini, ni elimu yao tu ndio inayofanya kazi. Lakini hawana nyenzo.

Mhe. Spika, haya ni Mapinduzi ya Kilimo na sisi tunafurahi kwamba watu wamo katika majaribio mazuri na katika dunia kuna hichi kitu tunaita *International relation.* Hakuna duniani nchi ya peke yako, ni lazima uweze kuishi nchi na nchi. Ukitaka kufanya biashara unasema mimi nafanya biashara baina ya hapa na hapa. Yaani mahusiano baina ya nchi na nchi kibiashara, mahusiano baina ya nchi na nchi katika ugunduzi wa mbegu za mimea. Na hapa ndipo tulipochukua watu wetu wa Zanzibar kuwaweka kimataifa. Sasa mimi ninachosema tunahitaji hapa mashirikiano kwanza ya humu ndani ya nchi yetu ya Zanzibar (a) na (b) tunahitaji *International relation* .

Nitaingia katika vifungu vya Katiba humu vinavyozungumzia humu ndani, ya kuonesha dhahiri kwamba hili halitokei hapa Unguja ni ya mtu mwengine, sie tumeingia kati kati tu. Kwa hivyo, niseme tu humu ndani ya sheria tumeitaja. Kwa hivyo, tukifanya hivi kwanza tunapata faida halafu watu wetu wanapata kujifunza kwa nchi za wenzetu. Unapoingia nchi ya mwenzako unapata kujifunza na hawa watu wetu wa utafiti na hawa Wagunduzi watakapokuwa wa kimataifa watakuwa ni watu ambao wamepata uzoefu mkubwa wa kukaa na watu, kuishi na watu na kujua kazi zao zinataka zifanywe vipi. Sasa wewe kama ni wiziri, haya mahusiano baina ya nchi yetu na nchi yengine, wewe nini *contribution* yako?

Kwa hiyo, Mhe. Spika, mimi ningesema tu ni muhimu kuwa nayo na sisi tulifanya hivi tukapata *recognition*. Hili jambo kama kweli tunalifanya kwa moyo mmoja ni sifa kwa Zanzibar na sisi Wazanzibari tutatambulika katika mataifa. Kwa hivyo, waziri isiwe mambo haya ndani ya makaratasi tu. Lakini lazima *step by step* ya watu hawa uwe nao mpaka wafikie hatua kubwa na tutajikane sisi Wazanzibari kwamba tuna watafiti na wagunduzi wazuri wa mbegu mbali mbali za mimea, hili ni jambo la msingi.

Mhe. Spika, katika mengineyo yaliyobakia nilitaka nimwambie Mhe. Waziri kwamba katika yote yaliokuwepo kwamba elimu ni suala la msingi. Hawa watu wanahitaji kuelimishwa si kila mtu kama ni mtafiti au mgunduzi anaweza kuelewa hii sheria hii. Lakini vile vile, wajue kwamba katika masuala haya kuna suala linamalizikia mwisho elimu ya msingi ya usajili ambayo wataipata na wajue kwamba katika kazi zetu mwisho tunamalizia adhabu, mtu atakapofanya makosa katika ugunduzi wake au katika utafiti

wake kama ikiwa utafiti wa uongo; hakuna ushahidi wowote yaani utafiti wa kibabe babe uliokuwa hauna msingi maalum si wa kielimu au wa kitaalamu maana yake anasema uongo.

Sasa Mhe. Spika, kwa hayo mimi nataka niingie katika maelezo yaliomo ndani.

Mhe. Spika, mimi nitagusia baadhi ya maeneo ambayo mimi kidogo yananipa wasi wasi hapa katika kifungu cha 22 (3a) kinasema:

> "Maombi yoyote yaliofanywa kwa Mrajisi wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea wa Tanzania Bara yatatambilika kama ni maombi, kwa aina sawa ya mbegu yaliyofanywa kwa mrajis"

Sijui kama hapa tunafahamu yaani tunaambiwa sisi katika mswada huu kwamba maombi yote kwa mrajis wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea, Watanzania Bara yatatambulika kama ni maombi kwa aina sawa ya mbegu yaliyofanywa kwa mrajis. Huyu *Register* si wa Zanzibar, *Register* huyu ni wa huko huko katika hiyo *Union* ambao kutokana na sheria za kimataaifa na sisi tunaingia ndani ya Jamhuri wa Muungano. Mimi nasema kama ni hivyo mbona katika mswada huu hakuna mahusiano wa *Register* wetu wa Zanzibar. Kifungu hiki kinasema:

> "*Whereby the Variety is already proctected by member of International Organization, dealing with the Plant breeders, price must matters to which United Republic ofTanzania is a Part of an Application for the Protection"*

Mimi hili suala ningetaka maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri kwa sababu mambo haya yanakwenda *direct* katika *Union*.

Pili katika masuala haya niliyoyazungumza Mhe. Spika, mimi nilitaka nijue vile vile ikiwa ni *matter of Union* na *Relation* yake iko Tanzania Bara. Je, katika masuala haya ya Katiba yamo ndani ya katika ya Zanzibar. Kwa sababu kuna mambo ambayo ni ya Muungano na kuna mambo ambayo si ya Muungano. Sasa na sisi tunasema kama jambo halikuletwa Zanzibar likazungumzwa katika Baraza la Wawakilishi likakubalika basi mjadala ule au sheria ile haikubaliki, itakuwa ni batili. Sasa hapa mimi nataka maelezo, maana sijafahamu kama ni letu wenyewe au linakwenda moja kwa moja kwa serikali ya muungano.

(c) Inasema mgawanyo wa ada za usajili wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu wa mimea, mgawanyo wa ada. Huu mgawanyo wa ada unakwenda wapi mbona hatujauelewa.

Mhe. Spika, nafikiri haya yanatosha, kwa hiyo nashukuru kwa hayo. Naunga mkono Mswada. (*Makofi*).

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu kuhusu mbegu mpya za mimea. Kwa kweli lazima tujipongeze kwa kufika mswada huu ambao umeletwa na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu ni mzuri kwa Zanzibar kwa sababu ni wakati wake wa kujiendeleza katika maendeleo ya kisasa twende na wakati kama zilivyo nchi nyengine. Ni wakati muhimu sana wa kujua hawa wenzetu ambao watakaopata kuchunguza mbegu hizi ndio wahusika hasa wa kuweza kuwa na hakimiliki.

Kwa kweli, Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri, huu utafiti wa mbegu hizi ni za dunia nzima ama zile za Zanzibar tu? Kwa ajili ziko sehemu nyingi ambazo mbegu nyengine hazioteshwi hapa Zanzibar wala hazina maendeleo makubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa mfano ni kwa nini mdoriani hauzalishi sehemu za Kusini kama Makunduchi na Jambiani.

Utafiti huu hauhusiani kabisa na wale wengine wanaozungumzia kwamba utafiti huu wa Tanzania Bara au wa serikali ngapi. Ningelipenda kwamba Mhe. Waziri akatuhakikishie tutapoanza kufanya utafiti huu unasaidia sana nchi yetu ya Zanzibar. Kwa sababu msaada huu umekuja kwa ajili ya Serikali ya Zanzibar na sio kwa ajili ya Serikali ya Muungano, kama kilivyosema kifungu hiki namba 6 kwamba:-

"Tunaweza kusaidia huko Tanzania Bara"

Lakini huu sio muongozo wa kusema gazeti hili rasmi ni la Muungano hili ni gazeti kwa ajili ya Zanzibar na ndio tukaweza kuuzungumzia mswada huu.

Mhe. Spika, kifungu namba 5 wagunduzi watakaogundua watapewa hakimiliki za ugunduzi wao wenyewe, ama utakuwa utafiti huu wa wizara nzima ama ushirika wenyewe hapo naomba Mhe. Waziri, atufafanulie.

Mhe. Spika, kwa vile hivi sasa tunaendelea na kutafuta mbegu za aina zote hasa za mazao ambazo zinawezekana zikasaidia Zanzibar kwa mambo ya chakula na mambo ya biashara, Ingelikuwa vyema utafiti huu wahusika wakapatiwa kitu maalumu ambacho kinaweza kusaidia kama cheti.

Mhe. Spika, sitokuwa na mchango mkubwa sana kwa leo isipokuwa kumpa nafasi Mhe. Waziri, atakapokuja aweze kutusaidia uhakika wa mbegu hizo. Ahsante sana (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe inaelekea kama vile karibu tutafika mwisho na kama hivyo ndivyo, basi naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na baadae Mhe. Dr. Mwinyi Haji Makame.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia mswada huu wa Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, nachukuwa nafasi hii kumpongeza Mhe. Kaimu Waziri pamoja na watendaji wake wote kutuletea mswada huu.

Mhe. Spika, sheria hii imekuja wakati muafaka tukizingatia mabadiliko ya hali ya hewa katika nchi yetu. Lakini kabla sijaingia katika vifungu naomba kumuuliza Mhe. Kaimu Waziri, kwamba mswada huu kama nilivyosikia Wajumbe walivyokuwa wakichangia kuhusiana na serikali tatu. Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri, anambie kwamba mswada huu una uhusiano gani na masuala ya serikali tatu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka ufanunuzi katika vipengele viwili kipengele cha 5 (a) kinachosema kutakuwa na hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Mhe. Spika, kipengele hiki nilikuwa naomba nipendekeze baada ya mbegu ifatane pamoja na mbolea.

Pia,nije katika kifungu hiki cha 5 (b) kinachosema:

> "Kusimamia rajisi na kutoa taarifa juu ya masuala ya hakimiliki za ugunduzi wa aina mpya za mbegu na mimea zitakazotolewa Zanzibar"

Nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri, mbegu hizi zilikuwa zinahusika na Zanzibar au na sehemu nyengine. Pia nije kifungu hiki hiki mabano (d)

> "Kushirikiana na taasisi za Kitaifa na za Kimataifa ambazo kazi zao zinawiana na masuala ya hakimiliki za ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea na kadhalika"

Namuomba Mhe. Waziri, kwamba kipengele hiki atakapokuja kuwasilisha, aje kunipa ufafanuzi mzuri kuhusu kitaifa na kimataifa.

Mhe. Spika, mimi pia napongeza wizara kwa kutuletea mbegu ya *NERICA*. Mhe. Spika, mbegu hii kusema kweli ilikuja wakati muafaka na wakulima wakalima na wakavuna na wakala. Kwa hivyo, mimi naipongeza wizara kwa kufanya kazi uzuri na wajitahidi kuendelea kutuletea mbegu nyengine zitakazoweza kutusaidia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwa vile nilianza kwa kusema kwamba mimi sitokuwa na mengi, naunga mkono mswada huu mia juu ya mia. (Makofi).

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kupata wasaa huu kutoa machache ya kuhusiana na Mswada wetu huu wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kwanza nizungumzie tu kidogo jinsi ya huu ugunduzi wa mbegu au mbegu kwa ujumla vipi zinavyozalishwa kwa kifupi tu. Mhe. Spika, ugunduzi wa mbegu au uzalishaji huu wa mbegu kitaalamu siku hizi umegawika sehemu mbili, kwanza kuna njia zile za kiasili za ugunduzi wa mbegu, hizi za kiasili kwa kizungu tunaziita *traditional planting method,* au zile tulivyozoea zamani kama ku-*cross* mipunga, ku-*cross* mihogo, zile mbegu za muhogo sio vigongoro. Zile mbegu zenyewe hasa tunaita mbarika, zile ndio zinapandishwa unapata mbegu mpya. Mipunga inafanywa hivyo hivyo, na mazao mengine hivyo hivyo. Kwa hivyo, hiyo ni njia mojawapo.

Lakini siku hizi wataalamu wamegundua kwamba njia hiyo ni ya kizamani na inachukua muda wa miaka nane, kumi, mpaka kumi na tano. Sasa tumebuni njia za kisasa ambazo zinaitwa *bio-tech* au kwa jina maarufu *GMO* yaani *Genetic Modified Organism.* Hizi kwa utaalamu mpya huu tunaita *bio-technology,* na utaalamu huu au uzalishaji mbegu hasa za chakula kwa njia hii nchi nyengine Mhe. Spika, wamepiga marufuku hawazitaki, na hata kwetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado sheria hii haijasimama vizuri kwa sababu ya wasiwasi wake.

Na zaidi kwa utaalamu, huu hao wenzetu wanatumia viumbe hai au sehemu za viumbe hai kuweza kupata mbegu mpya. Kwa kweli njia hii ndio njia ya kisasa ambayo inakubalika na ni ya haraka zaidi, na wataalamu wake wengi wanafanya kazi kwenye maabara ambazo kama Kizimbani tunayo sehemu mojawapo hiyo, tumezichukua mfano labda West Africa kule Ivory Coast, au wamechukua Nigeria tunakuja tunazikuza zaidi ili tuweze kuwapa wakulima.
Lakini kubwa ninalotaka kusema kwamba katika mgawanyiko huu wa pili ndio unaotumika kisasa na ndio unaotumika mwingi na ni wa haraka, hasa kwenye mbegu za mipunga, mahindi, ngano na kadhalika. Ulimwengu mzima hii njia ya *bio-tech* ndio inayotumika sana.

Sasa Mhe. Spika, ugunduzi huu ukishakuzipata zile mbegu zinakuwa ni kama biashara, kila mmoja anadhibiti ile mbegu yake. Na hata mfano mbegu ukiona kama zile za mboga mboga nazo wana siri zao, ni ugunduzi wao ule, makampuni mbali mbali ya Kenya, wenyewe wale wanadhibiti siri zile na

hujui, wenyewe ni *patent* yao ile au ni hakimiliki yao. Wamegundua kwa hiyo wenyewe wanadhibiti na huipati, ile ni siri zao wenyewe wanakwambia.

Sasa Mhe. Spika, katika ugunduzi huu wa mbegu matumizi yake haya si ya nchi moja, ni ya kimataifa. Na ndio maana hii sheria au huu mswada au hili Shirika la Kimataifa la Hakimiliki la Wagunduzi *(The International Union for the Protection of New Varieties of Plants (UPOV)* ndio likaja na utaratibu huu kuwa mbegu hizi kule unajitambulisha, zinaandikwa na wameanza zamani hii kazi kama walivyosema kwenye mswada. Wameanza zamani, lakini wakawa wanaiboresha au wanaiendeleza miaka 72, 78, 91 na nchi nyingi zikaridhia.

Sisi Tanzania bado tulikuwa hatujaridhia, sasa wenzetu Jamhuri ya Muungano wameridhia. Lakini kama wameridhia wao na haya ni masuala ya kilimo sio suala la Muungano, inatupasa na sisi kama sehemu mojawapo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sasa bado hatuna *sovereignty,* bado ni Tanzania ndio yenye *sovereignty* na wao ndio wamesharidhia. Lakini kutumia kwao wale wenzetu hawawezi bila ya Zanzibar. Na hiyo ni heshima kwetu kwamba vyombo mbali mbali vya kimataifa hasa vya kilimo, ingawa si vya kilimo tu, lakini hata *UNDP, WFP, UNFPA*, hivi vyombo vyote vya kimataifa wanatutambua na sisi Zanzibar na hii ni juhudi yetu.

Tulikuwa na matatizo kweli hapo zamani, ilikuwa *FAO* hata ofisi yao hapana hapa, *UNFPA* hapana, *IFAD* hapana, hata hao *WHO* walikuwa Dar es Salaam tu. Lakini tukafanya juhudi na sisi tutambulikane, sasa tunatambulika ndani ya Tanzania na mpaka mikutano tunakwenda nchi za nje na misaada *alhamdulillah! IFAD* wanatusaidia Zanzibar kwenye maendeleo ya kilimo kweli kweli. *UNFPA* kwenye afya na mambo yale ya *population, UNDP* nao wanasaidia kweli kweli.

Ninachotaka kusema tunashukuru haya mashirika ya kimataifa yanatutambua Zanzibar na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar na misaada mingi wanaileta. Lakini sasa tunapokwenda kuzungumza nao ile *sovereignty* lazima tufahamu, ule u-nchi bado tunakwenda kwenye *umbrella* ya *United Republic of Tanzania,* na hili tumeshalizungumza mara nyingi sana.

Sasa mimi lazima niwasifu Wizara ya Kilimo kwa juhudi hii, na kwa kweli Wizara ya Kilimo wana miradi mingi sana inayofadhiliwa au inayosaidiwa na nchi za nje. Na hii yote kwamba tumekubalika hatujiungi moja kwa moja, lakini tumekubalika kwenye haya mashirika ya kigeni, na yanatusaidia sana katika kuendeleza kilimo nchini mwetu.

Sasa tunaposema kwamba Bara wao wamejiunga kwa hiyo sisi tu muafaka wao si kweli, kuna mambo mengi sana kwenye kilimo tunafaidika sisi wao

hawafaidiki. Mfano mzuri kwenye *IFAD*, tumepata *phase* zote zile au miradi mingine tofauti wao wamefaidika na sisi tumefaidika. Na haimaanishi kwamba tunawafuata wao na sisi tuna wataalamu wetu na wanajua wanachokifanya. Kuna baadhi ya Waheshimiwa wamesema huu utafiti au ubunifu huu Zanzibar utafika lini?

Tayari umeshafika mwenyewe Mhe. Waziri, atakuja kusema, tayari mbegu wameshazizalisha na wameshazitoa kwa majina tofauti. Na hapo zamani ilikuwa hawana cha kuwalindia labda anaweza kuja mtu mwengine nae akasema mbegu yangu hii. Sasa tumeshaizalisha kama Kizimbani, wameizalisha basi wao watatoa jina la Kizimbani. Wanazo mbegu za muhogo, za viazi, na naamini karibu watakuja kwenye mbegu za mipunga na mengineyo.

Kwa hiyo, tukiuliza kwamba wataalamu hao tunao mimi nasema tunao Mheshimiwa, tunao wataalamu Zanzibar wanaoweza kuzalisha au kubuni mbegu za mpunga, mbegu za mihogo, viazi na mbegu nyengine. Labda Mhe. Waziri, atakuja kutoa mifano kwa majina kabisa.

Tumeendeleza vituo, Kizimbani sasa ndio kituo chetu kikuu cha utafiti wa mazao. Maabara tumezijenga pale mpya, tumeanza kidogo kidogo, juzi Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, kwenye Sherehe za Mapinduzi amekwenda kufungua maabara nyengine.

Mhe. Spika, Matangatuani ilivyokuwa tunavyoikumbuka sio ilivyo sasa, umeme pale tuliuvuta kutoka Konde kwa pesa za *IFAD*, nakumbuka tulikata pori kabisa Mhe. Suleiman Hemed Khamis, maji ilikuwa hapana pale, kulikuwa na kidimbwi chini bondeni kule, tutafanyaje utafiti bila ya maji, ikachimbwa *bore hole* pale. Mhe. Asaa Othman Hamad, alikuwa *incharge* pale kachimbisha yeye maabara zikajengwa.

Kwa hiyo, nataka kusisitiza tu Mhe. Spika, kwamba juhudi za kuendeleza miundo mbinu ya utafiti zinaendelea, maabara hizo, ujenzi unaendelea na wataalamu pia wanasomeshwa. Sio kama hakuna, wapo kabisa, labda wakati mwengine zile nyenzo tu za kufanyia kazi nazo zinakwenda kidogo kidogo.

Kwa hiyo, nataka kusema ushirikiano huu ni wa kimataifa. Sasa mbegu tukiizalisha hapa na sisi kama hatukujiunga itatambulika vipi? Haitotambulika. Kwa hiyo, lazima na sisi tujiunge, haimaanishi kwamba Bara wamejiunga na sisi tukae tu hivi hivi, hizo mbegu tukizalisha tukibuni watazi-*register* wapi? Ndio maana na sisi lazima tufuate utaratibu huu uliowekwa kisheria. Kwa hiyo ninalotaka kusisitiza Mhe. Spika, ni utaratibu wa kimataifa. Na ukisoma *version* ya kizungu nilijaribu kuisoma kwa kifupi yale

malengo, yanaeleza vizuri zaidi kuliko ya Kiswahili, ni yale yale, lakini yamekwenda kwa urefu tu.

Mhe. Spika, kwenye madhumuni na sababu wameelezea kwamba lengo kuu la kuanzishwa kwa mfumo huu ni kuhakikisha kuwa nchi zinazoridhia zinakuwa na utaratibu wa hakimiliki unaofanana. Unaona unatakiwa *uniformity,* ule utaratibu ufanane sio kila mmoja na utaratibu wake. Ndio kikawekwa chombo hiki sote tufuate kwenye chombo hiki. Sasa ikiwa Tanzania Bara anafanya yeye kivyake, sisi kivyetu, Kenya kivyake, mwengine kivyake itakuwa sio ya kimataifa hiyo! Ndio maana wakasema tuweke utaratibu unaofahamika kote na unaokubalika kote, hiyo ndio sababu hasa.

Mhe. Spika, kwenye madhumuni na sababu nazidi kusisitiza kwamba aidha mkataba huo unaweka utaratibu wa kutoa na kulinda hakimiliki. Kuna wengine wanaiba, baada ya muda wanasema hii mbegu niliizalisha mimi au niliibuni mimi. Sasa hii sheria inawalinda inakuwa *registered* unaiweka unailinda. Kulinda na kumiliki kwa wagunduzi wa aina ya mbegu na hivyo kuweka mazingira ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kutafiti mbegu bora na hivyo kuleta mapinduzi ya kilimo hapa nchini.

Lakini zaidi Mhe. Spika, nataka kusema kwamba ugunduzi huu wa mbegu pamoja na hakimiliki yake siku hizi ni biashara. Kama nilivyosema, wale wanaozalisha hizi mbegu kwa njia ile ya *bio-technology* wanazalisha kwa wingi sana, kwa haraka sana, sasa wanauza ndio zinapatikana hizo *high-breed.* Na *high breed* kila mwaka inabidi uizalishe tena, usiseme mwaka huu nimepata mbegu ya kitunguu *high breed* mwakani niitumie ile kuzalisha, utaona mazao yameanguka tu.
Kwa hiyo, wenyewe wana taratibu zao, wana siri zao wale wanazalisha vipi. Sasa hili Mhe. Spika, ningeomba sana tulifahamu na kulizingatia tu kwamba ni suala la kibiashara na kila mmoja analilinde. Kwa hiyo, na sisi tukigundua mbegu zetu, tukazilinda, tukazizalisha huko mbele tunaweza tukapata utajiri mkubwa sana kwa mbegu hizo. Na mifano nimetoa, hizi mbegu tunaziona tu za mboga mboga, tunauza kwenye vikopo na vipakti ni biashara kubwa sana. Kwa hiyo, wana hakimiliki wale na wanalinda wenyewe.

Mhe. Spika, naomba nimalizie tu kwa kusema kwamba hili suala si la kitaifa, ni la kimataifa. Kuna mbegu za mahindi Kenya mfano Kitale, wanatuletea, lakini wenyewe wana jina lao *Kitale Variety No. 1, Kitale No. 2.* Au pale Mwanza kuna Ukiliguru *No. 1, No. 2,* kila mwaka Ukiliguru 70, Ukiliguru 80, Ukiliguru ngapi. Sasa zile mbegu hata ukenda Mombasa, ukenda Nairobi nako unazipata. Kwa hiyo, si suala la ndani tu. Kwa hiyo, hili kwa kweli na

sisi tuna kila sababu ya kushiriki kuungana na utaratibu huu kwa kujitayarisha na matumizi ya siku za mbele.

Kwenye *copy* hii ya kizungu ameeleza tu kwamba *"However the UPOV conventions is not self executing."* Haiko pekee tu hii, haijitegemei pekee tu lazima inafanya kazi na wenziwe. *"Each member state must adopt legislation consistent with the requirements of the conventions"*

Mhe. Spika, nilisema nizungumze haya machache tu kwamba kwa kweli lazima tuwapongeze sana Wizara ya Kilimo kwa juhudi wanazofanya na miradi mbali mbali tunayopata kwa wafadhili *alhamdulillah.* Na tuna-*comply* na matakwa yao na tunajitahidi sana. Wakija ku-*check* matumizi yetu ya pesa wanakuta mazuri sana, na kila siku tukenda tunawapa maombi yetu ya miradi mipya wanatukubalia. Hii inaonesha vipi tunajitahidi kuona sisi tuko mstari wa mbele katika miradi hii. Kwa hiyo, si kama wanafanya Tanzania Bara na sisi tufanye aa, hili ni suala la kimataifa na sisi wajibu wetu tu-*stick* kwenye taratibu za Umoja wa Mataifa.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja na nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe kwa maendeleo ya kilimo ya nchini mwetu tuupitisheni mswada huu uweze kutusaidia. Hili ni suala la kimataifa na pia hao wenzetu wataona kweli na sisi tumesha-*comply*, watatusaidia tena, pengine baada ya *nerica* itakuja nyengine na wao watatusaidia kuzizalisha hapa hapa. Mhe. Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri tufikie tamati kwa michango, ila Mhe. Waziri, ameniomba mapema kwamba apate muda kuweka mambo vizuri kwa kuzungumza na wataalamu wake. Hivyo, yafaa tusitishe shughuli zetu hadi kesho, ili kesho tuanze na Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, na baadae tumsikilize Mhe. Kaimu Wazir, ambaye atatufanyia majumuisho rasmi kesho. Basi baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe tusitishe shughuli zetu na kwa maana hiyo naakhirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Alkhamis tarehe 23 saa tatu barabara za asubuhi.

(Saa 1:17 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 23/01/2014 saa 3:00 asubuhi)